# MTINDO KATIKA *UTENZI WA VITA VYA UHUD*

**NA**

**OBWOGI DICKENS BONYI**

**REG. NO. C50/5376/2017**

**KISWAHILI**

**KITIVO CHA SANAA**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2021**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine chochote.

OBWOGI DICKENS BONYI  Tarehe

(Mtahiniwa)  14/11/2021.

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Prof. RAYYA TIMAMMY  Tarehe

14/11/2021

Prof. KINEENE WA MUTISO  Tarehe

14/11/21

Prof. TOM OLALI

Tarehe  15/11/2021

**TABARUKU**

Namtabarukia kazi hii baba yangu mpenzi Lawrence Obwogi. Baba nakushukuru kwa kunifungua macho kuhusu umuhimu wa elimu ya juu. Ulinipatia nasaha ambazo zitabakia milele moyoni mwangu. Nakuombea afya na uzima maradufu.

Kwa mama yangu mzazi Loice Moraa, nashukuru kwa yote mausia na malezi mazuri tangu utotoni hadi sasa. Umekuwa wa msaada mkubwa katika maisha yangu. Mungu akuneemeshe zaidi.

Kwa mke wangu mpendwa Marieh Nyatichi na watoto wangu ninaowaenzi Michael na Kelsey, nashukuru kwa kunivumilia katika safari hii ndefu ya masomo. Nawapenda sana.

Kaka zangu Cliff Ooga na Meshack Mogere nawapenda sana na Mungu awaweke ulimwenguni kila wakati muwe wa msaada kwa wengine. Dada zangu Olpha, Callen, Magret, Ruth, Isabellah, Eznah na Vivian pia nawapa heko kwa kunipa moyo kila wakati. Hebu na Mungu awajalie mema na aila zenu kila wakati.

## SHUKRANI

Ningependa kuanza kwa kutoa shukurani kwa Mungu Muumba kwa kuniwezesha kufanikisha ndoto yangu ya kuhitimu katika shahada hii. Namshukuru kwa afya na uhai wakati wote tangu kuanza kazi hii hadi nilipo sasa. Ahsante kwa ustahamilivu ulionipa nilipokuwa nikiona ugumu wa kuendelea na kozi hii.

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Prof. Rayya Timammy, Prof. Kineene wa Mutiso na Prof.Tom Olali kwa juhudi zao za kunielekeza vyema kila wakati tangu nianze safari hii mpaka sasa imefika kikomo. Mlinipa mawaidha na maoni ambayo yalinifaa katika hatua zangu zote za utafiti huu. Nawaombea mbawazi za Mterehemezi ziwafuate tangu leo hadi milele. Inshallah.

Ningependa pia kuwapa pongezi wahadhiri wangu wote ambao waliweza kunifundisha katika shahada hii nao ni: Prof. Iribe Mwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Prof. Evans Mbuthia, Dkt. Prisca Jerono, Mw.  Leo Sanja, Prof. Mwenda Mbatiah na Prof. John Habwe kwa mafundisho yao ambayo yameniwezesha kuhitimu kozi hii bila balaa yoyote. Mungu awape rehema zake tumbi tumbi katika maisha haya.

Natoa shukrani za dhati kwa wanafunzi wenzangu tulioshirikiana kwa kila jambo katika kukamilisha kozi yetu ambao ni pamoja na Jomo, Ng'ang'a, Mosiori, Nyoike, Njane, Nancy, Lucy, Ann, Ruth, Violet, Jacinta, Ireene, Calvin, Njoroge, Rehema, Dorcus, Muteti, Mercy, Tom, Robert na Tunu. Nawatakia kila la kheri mwendapo Mungu awe nanyi.

Nisingependa kusahau kuwashukuru waalimu wangu waliokuwa wa karibu pia katika msururu wote wa yaliyohitajika kuhusu kazi zangu nao ni Pamoja na: Dkt. Florence Okari, Bw. Otwere Samson, Bw. Nixon Migiro na Dkt. Peter Nyansera. Asante sana kwa mawaidha na misaada yenu ya kila wakati. Mungu awabariki.

**ORODHA YA VIFUPISHO**

| | |
|---|---|
| khj. | kama hapo juu |
| mh. | mhariri |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| wah. | wahariri |

## IKISIRI

Tasnifu hii inahusu uhakiki wa kimtindo wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* nakala ya Haji Chum 1970. Tumehakiki namna vipengele vya kimtindo vimetumika katika utenzi huu kama vile: wahusika na uhusika wao, muundo, tamathali za usemi, mbinu rejeshi, taswira, mandhari na usimulizi. Nadharia ya umtindo imetufaa katika kuhakiki namna vipengele hivyo vimetumika kuufanikisha utenzi wetu. Katika utafiti wetu tumeongozwa na malengo matatu ambayo ni pamoja na kubainisha vipengele vya kimtindo vinavyotumika katika utenzi huu, pili tumechunguza nafasi ya vipengele hivyo katika kufanikisha utenzi wetu na mwisho tumebainisha namna muundo umejitokeza katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Tumehakiki sifa za wahusika zinazowatambulisha na uhusika wao katika utenzi huu. Tumegundua kuwa tamathali za usemi zimetumika kumsaidia msanii kuwasilisha dhamira na maudhui ya utenzi huu. Vile vile, katika utenzi huu kuna mandhari ya kivita, kidini na kijiografia ambamo utenzi wenyewe umefumbatwa. Muundo wa utenzi huu pia umejitokeza wazi wazi pamoja na aina tatu za usimulizi zimeangaziwa. Maswali yetu ya utafiti yamepata majibu kikamilifu kwani tumeweza kubainisha wazi vipengele vya kimtindo ambavyo vimetumika katika utenzi huu na kubainisha nafasi zao. Tumefafanua changamoto tulizopitia na kuelezea namna tulivyozisuluhisha. Mwisho tumetoa mapendekezo kwa watafiti wa baadaye kuhusiana na *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

## YALIYOMO


UNGAMO ... ii
TABARUKU ... iii
SHUKURANI ... iv
ORODHA YA VIFUPISHO ... v
IKISIRI ... vi
SURA YA KWANZA ... 1
1.0 Utangulizi ... 1
1.1 Tatizo la utafiti ... 3
1.2 Madhumuni ya utafiti ... 3
1.3 Maswali ya utafiti ... 4
1.4 Sababu za kuchagua mada ... 4
1.5 Upeo na mipaka ya utafiti wetu ... 5
1.6 Msingi wa nadharia ... 6
1.6.1 Mihimili ya nadharia ya umtindo ... 8
1.7.0 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii. ... 9
1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu mtindo ... 9
1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu uhakiki wa kimtindo. ... 11
1.8.0 Mbinu za utafiti ... 18
1.8.1 Mbinu za ukusanyaji data ... 18
1.8.2 Mbinu za uchambuzi wa data. ... 19
1.8.3 Mbinu za uwasilishaji wa data. ... 20
1.9 Hitimisho ... 20
SURA YA PILI ... 21
UFAFANUZI WA DHANA MBALIMBALI KATIKA UTAFITI WETU ... 21
2.0 Utangulizi ... 21
2.1 Ushairi ... 21
2.2 Utenzi ... 23
2.3 Mukhutasari wa Utenzi wa Vita vya Uhud ... 24
2.4 Mtindo ... 24
2.5 Muundo ... 25

2.6 Tamathali za usemia ........................................ 26
2.6.1 Taswira ........................................ 27
2.6.2 Tashbihi ........................................ 28
2.6.2 Takriri ........................................ 28
2.7 Wahusika ........................................ 28
2.8 Mandhari ........................................ 29
2.9 Usimulizi ........................................ 30
2.10 Hitimisho ........................................ 32
SURA YA TATU ........................................ 33
WAHUSIKA NA UHUSIKA WAO NA MUUNDO KATIKA *UTENZI WA VITA VYA UHUD.*
3.0 Utangulizi ........................................ 33
3.1.0 Wahusika binafsi ........................................ 33
3.1.1 Mungu Muumba ........................................ 34
3.1.2 Mtume Muhammad ........................................ 35
3.1.3 Munsabu bin Omari ........................................ 38
3.1.4 Bwana Khalid mwana wa Walid ........................................ 38
3.1.5 Ukirima bin Abii Jahl ........................................ 38
3.1.6 Amir Ibn Alyas ........................................ 39
3.1.7 Sufian Ibn Banu Umayya ........................................ 39
3.1.8 Hindu Binti Ustadh ........................................ 39
3.1.9 Abdillahi bin Shihabi Kabihi ........................................ 40
3.1.10 Abdalla bin Ubayya bin Sululi ........................................ 41
3.1.11. Abu Sufiani ........................................ 42
3.1.12 Ubayyi bin Khalafu ........................................ 42
3.1.13 Utuba Al Ukasi ........................................ 43
3.1.14 Abdalla Khuberi ........................................ 44
3.1.15 Seyyida Fatima ........................................ 44
3.1.16 Abu Ubeid ........................................ 45
3.1.17 Talha ........................................ 45
3.1.18 Ali ........................................ 45
3.1.19 Bwana Sadi ........................................ 46

3.1.20 Bwana Hamza ........ 46
3.1.21 Sayyid Umari ........ 47
3.2.0 Wahusika wa kimakundi ........ 47
3.2.1 Seyyidati Esha na Seyyidati Batuli ........ 47
3.2.2 Masahaba wa Mtume ........ 47
3.2.3 Wanawake Makureshi ........ 48
3.2.4 Jeshi la Makureshi ........ 49
3.2.5 Jeshi la Waislamu ........ 51
3.2.6 Wanawake wa Kiislamu ........ 52
3.3.0 Muundo ........ 52
3.3.1 Muwala ........ 52
3.3.2 Bahari ........ 53
3.3.3 Ubeti ........ 53
3.3.4 Kina cha bahari ........ 53
3.3.5 Mishororo ........ 54
3.3.6 Vina ........ 54
3.4.0 Uhuru wa kishairi ........ 54
3.4.1 Inkisari ........ 54
3.4.2 Mazida ........ 55
3.4.3 Tabdila ........ 55
3.4.4 Ukiushi wa kisarufi ........ 56
3.5 Hitimisho ........ 57
SURA YA NNE ........ 58
TAMATHALI ZA USEMI, MBINU REJESHI NA TASWIRA KATIKA UTENZI WA VITA VYA UHUD ........ 58
4.0 Utangulizi ........ 58
4.1.0 Tamathali za Usemi ........ 58
4.1.1 Takriri ........ 58
4.1.2 Tashbihi ........ 63
4.1.3 Maswali ya balagha ........ 65
4.1.4 Istiari ........ 66

4.1.5 Chuku ... 67
4.1.6 Kinaya ... 68
4.1.7 Uhaishaji ... 69
4.2 Mbinu rejeshi ... 69
4.3 Taswira ... 71
4.4 Hitimisho ... 73
SURA YA TANO ... 75
MANDHARI NA USIMULIZI ... 75
5.0 Utangulizi ... 75
5.0 Mandhari ... 75
5.1.1 Mandhari ya kidini ... 76
5.1.2 Mandhari ya kivita ... 77
5.1.3 Mandhari ya kijiografia ... 79
5.2 Usimulizi ... 80
5.2.1 Usimulizi nafsi ya tatu ... 81
5.2.2 Usimulizi nafsi ya kwanza ... 82
5.2.3 Usimulizi penyezi ... 83
5.3 Hitimisho ... 85
SURA YA SITA ... 86
6.0 Utangulizi ... 86
6.1 Mukhutasari wa yaliyoshughulikiwa katika utafiti wetu ... 86
6.2 Matokeo ya utafiti wetu ... 87
6.3 Changamoto zilizotukumba kipindi cha utafiti wetu na suluhisho. ... 87
6.4 Mapendekezo kwa tafiti za baadaye ... 88
MAREJELEO ... 89

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Katika utafiti wetu, tumehakiki namna mtunzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* ametumia mtindo kuwasilisha ujumbe wake. Kwa madhumuni ya kutambua jinsi mtindo ulivyotumika katika utenzi huu, tumechambua vipengele mbalimbali vya kimtindo ambavyo ni pamoja na: wahusika na uhusika wao, muundo, tamathali za usemi, taswira, mbinu rejeshi, mandhari na usimulizi. Vipengele hivi vimetumika pamoja kikamilifu ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe katika utenzi huu. Hii ina maana kuwa kwa minajili ya kufanikisha utenzi huu, sharti vipengele hivi kujengana na kukamilishana kwani hamna kipengele ambacho kitajitosheleza peke yake bila mchango wa chenzake.

Katika kazi za kisanii, watunzi hutunga kazi zao kwa njia maalum ili kuwasilisha jumbe zao kwa hadhira zao. Katika utafiti wetu, tumeangazia jinsi mtunzi wa utenzi huu ametumia vipengele vya kimtindo kuwasilisha dhamira na maudhui yake katika utenzi huu. Kulingana na Senkoro (1982) mtindo ni jinsi ambavyo msanii yeyote huamua kufinyanga kazi yake ya kisanaa kwa lengo la kuwasilisha ujumbe wake kwa njia ya kitaalamu na inayovutia msomaji. Naye Wamitila (2002) anapambanua mtindo kama namna ya kipekee ambayo msanii huwasilisha maoni yake kupitia fasihi.

Bila shaka maelezo hayo hapo juu yamedhihirisha waziwazi maana na umuhimu wa mtindo katika kazi za kifasihi. Kulingana nasi, ni kweli mtindo hudhihirisha namna ya kipekee ambayo kila msanii hutumia kuwasilisha mawazo yake kwa hadhira yake. Mbinu za lugha pamoja na misamiati huenda vikawa ni hazina wanayoitegemea wasanii wote, lakini uteuzi na utumiaji wa vipengele hivyo katika kazi za wasanii huleta upekee fulani katika kazi zao. Katika utafiti wetu tumebainisha kwamba mtunzi wa utenzi huu pia amejitambulisha kwa njia ya kipekee kwa namna ambavyo ametumia mtindo katika kazi yake.

Ijapokuwa mtunzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* hajulikani pamoja na tarehe kamili ya utunzi wake, tunaelezwa kwamba utenzi huu ulikusanywa na kuwekwa pamoja katika nakala na Haji Chum. Nakala hii ndiyo tuliisoma, tukaichanganua na ndiyo tumerejelea katika utafiti wetu. Chum (1970) anatueleza kuwa utenzi huu ulihifadhiwa kwa kupokezwa kizazi hadi kizazi kupitia masimulizi ya midomo. Kwa sababu hiyo, aliamua kuuandika kwa lengo la kuuhifadhi usije ukapotea. Bila shaka

Haji Chum alifanya kazi nzuri ya kuukusanya na kuuhifadhi utenzi huu. Utenzi huu ni mojawapo ya tenzi ndefu, kwani una beti mia saba thelathini na tisa. Kwa kiasi kikubwa tunaweza kusema kuwa utenzi huu ni wa kihistoria. Historia yenyewe ni ya uhasama wa kivita baina ya Mtume Muhammad na watu wa ukoo wake (Makureshi). Mwanzo, tunasoma katika utenzi huu, japo kwa kifupi kuhusu vita vya Badri ambavyo Mtume Muhammad alipata ushindi mkubwa dhidi ya Makureshi kwa vile Mtume Muhammad na jeshi lake dogo waliwaua Makureshi sabini na kupeleka wengine sabini mateka wakiwemo maamiri wakuu kama vile Abu Jahl, Uthbah, Shaiba, Walid, Umayya bin Khalafu na Hanzala bin Abu Sufyan. Kushindwa huku kwa wapinzani hawa wa Mtume Muhammad kukawafanya kuweka ahadi ya kulipiza kisasi baada ya takriban miezi tisa. Baada ya Makureshi kujiandaa vya kutosha kupigana na Mtume Muhammad, wakatuma habari kwake kuwa walikuwa tayari kushiriki vita. Hapo ndipo pigano katika mlima Uhud lilifanyika. Pigano hili ndilo linaloitwa vita vya Uhud. Katika pigano hilo, Mtume Muhammad alipanga vyema kikosi chake na kuwapa masharti waliyopaswa kuzingatia wakiwa katika mapambano ya kivita dhidi ya maadui zao. Kwa sababu kikosi kilichochunga njia za milimani kilikosa kufuata ushauri wa Mtume Muhammad, Makureshi wakawavamia na kuwajeruhi vibaya sana.

Maudhui makuu katika utenzi huu ni ya kivita ambavyo vilitokea mahali panapoitwa Uhud. Vita hivi vilipewa jina Uhud kwa sababu vilipiganwa karibu na mlima Uhud. Kama vile tumekwishaeleza hapo awali, katika vita hivi kulingana na msimulizi wa utenzi huu, Mtume Muhammad na jeshi lake walipata pigo kubwa, kwa sababu jeshi lake halikuzingatia mwelekeo wa Mtume Muhammad wa kuchunga njia za milimani kwa vyovyote vile. Badala yake, walipoona walikuwa wamewafukuzia mbali Makureshi, wakarudi kung'ang'ania mali na rasilimali wapinzani wao walizowacha baada ya kulemewa na vita. Baadaye, wapinzani wao walipogundua njia za milimani zilikuwa wazi wakarejea kwa uvamizi mkubwa na kuwapiga vibaya sana hadi Mtume Muhammad akapata majeraha makubwa.

Kama vile tulivyoeleza hapo awali kuhusu umuhimu wa mtindo katika fasihi, bado tunasisitiza kuwa msanii yeyote akiwemo mtunzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* hulenga kuwasilisha kikamilifu dhamira na maudhui yake kwa hadhira yake. Hivyo basi, ni jambo la lazima kwake kutambua mikakati itakayomfaa kuafikia azimio lake. Mtunzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* basi bila shaka ametumia mtindo fulani kutuwasilishia dhamira na maudhui yake. Katika utafiti huu, tumechanganua na kubaini ni vipengele vipi vya kimtindo ambavyo msanii huyu amevitumia

kufinyanga dhamira na maudhui yake katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Vile vile, tumeonyesha uhusiano uliopo baina ya vipengele hivyo kimatumizi kwani vipengele hivi sharti vitegemeane na kujengana ili tuweze kupata kazi ya kifasihi inayoafiki hali halisi katika jamii.

Ni muhimu pia kutambua kuwa vipengele vya kimtindo katika fasihi ni vingi navyo ni kama vile: lugha, toni na sauti, mandhari, usimulizi, taswira, wahusika, muundo, tamathali za usemi, na vinginevyo. Katika utafiti huu hata hivyo, tumehakiki baadhi ya vipengele kama vile: wahusika, mandhari, tamathali za usemi, mbinu rejeshi, taswira, usimulizi na muundo ili kubaini namna vimetumika na athari vinayozua katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*.

**1.1 Tatizo la utafiti**

Tatizo letu la utafiti ni kutambua nafasi ya mtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*Tumetathimini namna mtindo umetumika katika *Utenzi wa vita vya Uhud* kwa kuchambua vipengele mbalimbali vya kimtindo vikiwemo: wahusika na uhusika wao, muundo, tamathali za usemi, mbinu rejeshi, taswira, mandhari na usimulizi ili kubainisha namna vipengele hivyo vimefanikisha dhamira na maudhui katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Katika uelewa wetu, dhima kuu ya mtindo katika fasihi ni kudhihirisha upekee wa kazi ya kila msanii.

Katika hali halisi, watu wengi hupendelea kusoma kazi zinazochangamsha na kuvutia. Hili ni dhihirisho kuwa kipengele cha mtindo ni muhimu kuzingatiwa na kila msanii iwapo analenga kufaulu katika utunzi wake. Msanii ni sharti awazie namna ya kutumia vipengele mbalimbali vya kimtindo kikamilifu ili kupamba kazi yake. Vile vile, ni muhimu kwa msanii yeyote kuhakikisha ameshughulikia masuala ambayo yanaikumba jamii kwa lugha yenye mnato na mvuto.

**1.2 Madhumuni ya utafiti**

Lengo kuu la utafiti wetu ni kuchunguza jinsi mtunzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* ametumia vipengele vya kimtindo ili kuwasilisha ujumbe wake kikamilifu. Malengo ya utafiti wetu ni kama yafuatayo;

*i.* Kubainisha vipengele vya kimtindo vilivyojitokeza katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* na namna vilivyotumika.

ii. Kuchunguza nafasi ya vipengele hivyo vya kimtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* katika kufanikisha dhamira na maudhui lengwa.

iii. Kuhakiki namna kipengele cha muundo kimejitokeza katika *Utenzi wa* V*ita vya Uhud.*

**1.3 Maswali ya utafiti**

Katika utafiti wetu tumeongozwa na maswali yafuatayo:

i. *Utenzi wa Vita vya Uhud* una vipengele vipi vya kimtindo na vimejitokeza namna gani?

ii. Vipengele vya kimtindo vina umuhimu gani katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*?

iii. Je, muundo umejitokeza vipi katika *Utenzi wa Vita vya Uhud?*

**1.4 Sababu za kuchagua mada**

Tulichagua kuhakiki mtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* kwa sababu mbali na kazi za tafsiri za utenzi huu kutoka Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza, kutokana na ufahamu wetu ni Kithuku (2017) pekee aliyeuhakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud* kimaudhui na kimtindo. Kwa sababu kati ya makala na tasnifu ambazo tumesoma, kazi za wataalamu waliohakiki utenzi huu ni haba. Katika utafiti wetu tumehakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud* kimtindo kwa kuangazia aina ya vipengele vya kimtindo ambavyo msanii ametumia kusuka utenzi huu.

Msukumo wetu wa kuutafiti utenzi huu ulitokana na vipindi vya darasani, ambapo tuliusoma na kuuchambua utenzi huu kama mojawapo ya kazi ambazo tulipaswa kushughulikia. Katika kupitia huku, nikavutwa na ujumbe wa suitafahamu baina ya Mtume Muhammad na watu wa nasaba yake (Makureshi). Katika kule kutaka kutambua kiini cha suitafahamu hiyo nikavutiwa zaidi na hivyo kuamua kuuhakiki utenzi wenyewe kimtindo.

*Utenzi wa Vita vya Uhud* ni mojawapo ya tenzi ndefu ukiwa na beti mia saba thelathini na tisa (739) kama ambavyo tumeeleza hapo awali. Wahakiki wengi huenda wamechelea kuuhakiki utenzi huu kwa sababu ya urefu wake. Kwa hivyo, katika utafiti huu tumelenga kuwatia motisha watafiti wa fasihi kuangazia uhakiki wa tenzi zaidi kwani hii pia ni sehemu muhimu ya fasihi katika jamii zetu. Katika utafiti huu tumelenga kuwarahisishia wanafunzi pamoja na waalimu wa fasihi kazi ya uhakiki kwa kuwapa misingi ya kuhakiki tenzi nyingine kimtindo. Utafiti huu vile vile utakuwa muhimu kwa wataalamu na wasomi wengine kwa kuwapa msingi muhimu ili kuendeleza tafiti za tenzi nyingine ambazo labda hazijatafitiwa kimtindo. Sababu nyingine ya kufanya utafiti huu ni kuwa, utaongeza idadi ya kazi za uhakiki wa tenzi za Kiswahili. Huenda

ikawa huku kuandikiwa kazi nyingi ndiyo sababu vipera vingine vya fasihi vina umaarufu ikizingatiwa kuwa vipera hivyo vina idadi kubwa ya kazi za uhakiki ukilinganisha na tenzi. Kazi hizo ni kama riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Ingawa hivyo, hatukatai kwamba tenzi hazijatafitiwa kwani kwa mtazamo wetu tumegundua kuwa kuna baadhi ya tenzi zilizotafitiwa sana kama vile *Utenzi wa Fumo Liyongo, Utenzi wa Mwanakupona, Utenzi wa Al Inkishafi,* na kadhalika. Hata hivyo tungependa kusema kuwa, baadhi ya tenzi hizo tulizozitaja hapo juu ingawa zimehakikiwa sana bado zinaweza kuhakikiwa upya kwa lengo la kuziboresha zaidi. Hili linawezekana kwani kila mtafiti huwa na mtazamo wake binafsi na hivyo basi ingawa tafiti zitarejelea mada moja bila shaka lazima kuwe na tofauti baina ya tafiti hizo ambayo huwa na lengo la kuboresha utafiti wa awali.

Utafiti huu umechangia kuelewa jinsi mtindo unavyotumika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Katika utafiti huu, tumebaini uhusiano uliopo baina ya vipengele vya kimtindo tunavyohakiki katika utenzi huu kwa kuonyesha namna vinavyotumika kuwasilisha dhamira na maudhui ya mtunzi wa utenzi huu.

**1.5 Upeo na mipaka ya utafiti wetu**

Katika utafiti huu tumechunguza vipengele vya kimtindo ambavyo vimetumika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Vipengele hivyo vya kimtindo ni kama vile: taswira, mbinu rejeshi, usimulizi, wahusika na uhusika wao, muundo, mandhari na tamathali za usemi kama vile: tashbihi, istiara, takriri, maswali ya balagha, chuku, kinaya na uhaishaji na jinsi vimetumika kufanikisha dhamira na maudhui katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Tuliteua vipengele vichache miongoni mwa vingi vilivyopo katika utenzi wenyewe kwa sababu ya ukosefu wa muda wa kutosha kutafiti vipengele zaidi. Katika utafiti huu tumejikita katika nadharia ya umtindo. Tuliteua nadharia hii kufanyia utafiti wetu kwa vile kwa maoni yetu, ndiyo pekee tuliona kuwa ingetusaidia kuhakiki vipengele vya kimtindo kwa ufasaha katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Mihimili ya nadharia ya umtindo pia tumeitaja na kuilezea chini ya nadharia na mihimili yake. Ingawa hivyo, mihimili ile ambayo imeafiki utafiti wetu ndiyo tumeizingatia. Katika utafiti wetu hatujashughulikia dhamira na maudhui kwa undani ila tu kuonyesha kwa kutumia vipengele vya kimtindo namna dhamira na maudhui hujitokeza kwa uwazi zaidi.

**1.6 Msingi wa nadharia**

Nadharia ya Umtindo ina misingi yake Urusi ilikoasisiwa (1904). Nadharia hii iliongozwa huko Moscow na Roman Jakobson pamoja na Victor Shklovsky, mwanzoni mwa karne ya ishirini. Lengo kuu la wasomi hawa lilikuwa ni kukuza uhakiki wa kazi za kifasihi kisayansi ikiwa na maana ya kutathimini vijenzi vya fasihi yenyewe. Kutokana na mchango wa wasomi hao, nadharia hii ikafanikiwa sana Uingereza na Marekani katika miaka ya 1960. Nadharia hii iliasisiwa kwa lengo la kudhihirisha kwamba mtindo ni matumizi ya kipekee ya lugha. Bradford (1997), Katikiro (2018), Leech (1979) na Mbatiah (2001) wanakubaliana kuwa nadharia ya umtindo ilichipuka katika karne ya ishirini na iliasisiwa huko Moscow mwanzoni mwa karne ya ishirini kwa lengo la kusisitiza kuwa fasihi ndiyo pekee iliyoweza kudumisha upekee wa lugha ya msanii kinyume na lugha ya kawaida. Kulingana na maoni ya wataalamu hawa ni wazi kuwa katika fasihi, msanii ameruhusiwa kupotoka kutokana na uhalisia kwa sababu fasihi imetengwa na aina ya mijadala ambayo huenda ikawa na athari kwa hali halisia za wahusika. Hata hivyo, ni muhimu kuelewa kuwa ingawa lugha ya kifasihi na lugha ya kawaida zaweza kuwa na vipengele vya kimtindo sawa, matini zote mbili haziwezi kuwa katika kiwango sawa kimatumizi. Kwa mtazamo wetu, maoni ya wasomi hao ni ya kweli kabisa kwa sababu lugha ya kawaida na ya kifasihi hazina hadhi sawa. Sababu kuu ni kuwa, lugha ya fasihi imesheheni uteuzi na mpangilio wa misamiati kwa ufundi ulio wa juu. Pili, lugha ya kifasihi hulenga kutoa mawasiliano maalum kwa hadhira maalum.

Kwa maoni yetu, lugha ya kawaida ni tofauti na lugha ya kifasihi kwa sababu katika fasihi, msanii hutumia ufundi wa kuandika kazi ambayo huishia kuwa yenye mnato yaani ya kuvutia msomaji. Wakati mwingine lugha ya kifasihi hupangwa kwa njia maalum ili kukidhi malengo ya msanii. Ni muhimu pia kutambua kuwa, lugha ya kisanii wakati mwingine hukiuka sheria za lugha ya kawaida haswa mpangilio wa maneno katika sentensi. Kwa mfano, katika ushairi, miundo iliyozoeleka ya mpangilio wa maneno katika sentensi wakati mwingine huwa haizingatiwi. Katika ushairi, mbinu hizi huitwa uhuru wa mshairi. Katika uhuru huo msanii ameruhusiwa kukata na kurefusha maneno na pia ana kibali cha kutarakanya mpangilio wa sentensi kinyume na inavyokubaliwa katika sarufi ya Kiswahili. Ingawa hivyo, lengo la lugha zote ni mawasiliano ijapokuwa lugha ya kifasihi huzingatia namna mawasiliano hayo yatapendeza zaidi ikilinganishwa na lugha ya kawaida. Lugha ya kifasihi ikifinyangwa kwa ustadi na weledi hutambuliwa kama iliyo na ubunifu wa hali ya juu na hivyo kuthaminiwa zaidi. Iwapo hayo hayajatimilika katika kazi

ya kifasihi basi kazi hiyo hubakia kuitwa kazi iliyo ya thamani ya chini. Ubunifu katika kazi za kifasihi hutokana na matumizi ya vipengele mbalimbali vya kimtindo kikamilifu.

Boakes na Halliday (1972) wanaelezea kuwa fasihi kimsingi haitokani na mfumo wa lugha tu, iwe ni fonolojia au sintaksia. Wanasisitiza umuhimu wa semantiki katika uchanganuzi wa mtindo huku wakisema kuwa ndiyo njia pekee itakayomsaidia mtafiti kutambua na kuelewa nadharia mbalimbali zinazozingatia matumizi ya lugha na umuhimu wake. Leech na Short (2007) nao wakirejelea maoni ya Boakes na Halliday (khj), wameyashadidia na kuyatambua kama mwongozo ambao utamuongoza msemaji na anayesemezwa iwapo watazingatia mawasiliano, uwakilishi na maandishi. Wanazidi kueleza kuwa hakuna muachano wowote kati ya mawasiliano ya kila siku na fasihi kwa vile mbinu sawa na kanuni za tafsiri hutumika. Maoni ambayo tunatofautiana nayo kwa misingi kuwa ni vigumu lugha ya kawaida kudhihirisha ufundi unaodhihirika katika lugha ya kifasihi katika mawasiliano ya kawaida. Sababu ni kwamba, lugha ya kawaida wakati mwingine huzingatia viziada vingi na hivyo wakati mwingine huwa si kamili haswa kwa anayetegemea sauti.

Kwa maoni yetu, vipengele vya kimtindo vinatumika kutekeleza wajibu muhimu wa kuzifanya kazi za kifasihi kuwa na mnato unaovutia na kuburudisha hadhira. Ni kweli kwamba bila mtindo hatuwezi kuwa na kazi ya kifasihi kabisa. Sababu ni kwamba, ni mtindo tu ambao hutumiwa na msanii kuibadilisha lugha ya kawaida hadi lugha ya kifasihi. Lugha hii ya kifasihi huleta mawasiliano maalum katika jamii husika. Makali ya mtindo hufanya kazi za kifasihi kupendeza na lugha yenyewe huwa yenye mnato.

Mtindo katika fasihi ni ile hali ya msanii kujieleza kwa hisia za ndani kwa kutumia lugha ya mnato. Lugha hii huwa yenye mnato kutokana na utumiaji mzuri wa tamathali mbalimbali za usemi, matumizi murua ya wahusika, muundo, taswira, usimulizi, mandhari na kadhalika, haya ni kulingana na Riffaterre (2008). Maoni hayo ni kweli kwa sababu, hii ndiyo njia pekee ambapo lugha ya kawaida hutofautiana na ile ya kifasihi. Tamathali za usemi pamoja na vipengele hivyo vingine vya kimtindo tulivyotaja sharti vitumike kikamilifu ili kazi ya kisanii iweze kufaulu. Lazima msanii ateue misamiati na mbinu muafaka kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake kwa njia inayovutia. Bila kufanya hivyo kazi yake huenda ikakosa wasomaji wengi.

Kwa mtazamo wa Wamitila (2003) uhakiki wa ufasihi unaodhihirika katika kazi ya kifasihi ndio unapaswa kupewa kipau mbele na msomaji matini au mhakiki ili kubaini mafanikio ya kazi

yenyewe bali si historia wala mtunzi binafsi. Kulingana na Wamitila, huu ndio uhakiki wa fasihi kisayansi. Unaitwa hivyo kwa sababu unalenga kutathimini vijenzi vya kazi binafsi. Ukweli wa mambo ni kuwa, ufasihi wa kazi ndio unapaswa kuhakikiwa bali si vipengele vingine vilivyo nje ya kazi ya kifasihi. Kipengele cha historia na msanii havipaswi kuangaziwa katika uhakiki kwani, baada ya msanii kuandika kazi yake huwa hana jingine ila huwaachia wasomi na wahakiki kuitolea kauli. Iwapo uhakiki utakuwa ukizingatia ufasihi wa kazi, bila shaka misingi ya kuitathimini kazi itakuwa rahisi na wazi.

Kwa mtazamo wetu, mtindo ni namna ambavyo msanii huamua kupanga kazi yake ikiwa ni pamoja na uchaguzi wa msamiati unaofaa, tamathali za usemi zinazovutia, mada inayosisimua na kuvifinyanga kwa ufundi na ubunifu unaochochea hadhira kupenda kuisoma kazi yake. Ingawa hivyo, ni vyema kuelewa kuwa msomaji hana haja na mtindo bali ujumbe. Hata hivyo, mtindo hutumika kama chambo atumiacho msanii kuwanasa wasomi wengi kuipenda kazi yake. Iwapo msanii atatumia mtindo unaovutia wengi bila shaka ujumbe wake utazagaa mbali zaidi. Katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo kwa sababu inatuelekeza katika uhakiki wa vipengele vya kimtindo kubaini namna vimetumika katika *Utenzi wa* V*ita vya Uhud* kufaulisha dhamira na maudhui lengwa. Vipengele hivyo ni kama vile; taswira, mbinu rejeshi, usimulizi, wahusika na uhusika wao, mandhari, muundo na tamathali za usemi.

### 1.6.1 Mihimili ya nadharia ya umtindo

Kuna fafanuzi aina mbalimbali za mitindo katika fasihi ukizingatia idadi ya wanamitindo ilivyo. Katika utafiti wetu tumeongozwa na mawazo ya wanamitindo kama vile; Halliday na Leech. Kulingana na Halliday (1971) kuna mihimili mitatu ambayo imetusaidia kuchanganua kazi ya utenzi wetu kimtindo kama vile:

Lugha hutumiwa kama chombo cha mawasiliano kwa lengo la kufanikisha ujumbe unaokusudiwa katika mawasilano. Mawasiliano haya hurejelea vitu halisia au vitu dhahania. Nguzo hii imetuelekeza kuelewa namna vipengele vya kimtindo teule vimetumika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* kwa lengo la kuwasilisha dhamira na maudhui. Maudhui makuu hapa ni pamoja na vita, dini na kadhalika. Kwa jumla, lengo kuu la lugha katika jamii yoyote ile ni kuwasiliana. Mawasiliano ya kawaida hufanywa kwa lugha ya kawaida ilhali mawasiliano ya kisanii hufanywa kwa lugha ya kifasihi. Lugha tunayoirejelea katika utafiti wetu ni ya kisanii ambayo aghalabu hutumiwa na wasanii katika ufinyanzi wa kazi zao.

Pili, kuna mhimili unaodokeza kuwa kazi ya sanaa huwa na vipengele kama vile ploti, wahusika, dhamira, maudhui lakini iwapo hamna lugha vipengele hivyo haviwezi kujitosheleza kimaana kwani kila wakati vinapata maana kupitia lugha. Lugha imejikita katika sarufi kimfumo na kimuundo hali ambayo hudhihirisha namna ilivyojengwa. Nguzo hii imetuelekeza kuelewa muundo na mtindo wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* kwa jumla. Lugha imekwezwa hadhi hapa kwa sababu ndiyo kitovu cha mawasiliano yoyote. Ingawa mtindo ni muhimu katika fasihi, huwezi ukafaulu bila lugha. Ni jambo muhimu kujua kuwa vipengele vya mtindo haviwezi kuleta maana yoyote kiupweke. Ni lazima viunganishwe pamoja ili kuchangia kuleta maana kusudiwa. Ili kuvileta pamoja basi ni lazima lugha itumike. Ni dhahiri shahiri kwamba lugha ndio msingi wa fasihi yoyote ile. Ili ufasihi wa fasihi utathiminiwe, sharti lugha ihusike kwa kufinyanga vipengele hivi vya kimtindo ili kuleta maana hitajika.

Tatu, kuna mhimili ule ambao unasisitiza kuwa lugha pamoja na ujumbe ni sharti viwe na uwiano iwapo kazi ya sanaa itafaulu kwa sababu mawili hayo ndiyo chanzo cha ubunifu katika fasihi. Lugha ambayo tunaitegemea kuwasilisha hisia zetu, vile vile ndiyo tuitumiayo kushawishi hisia za watu wengine. Nguzo hii imetusaidia kubaini ni jinsi gani ujumbe umetiririka katika utenzi wetu. Maana ya mhimili huu ni kuwa masuala ambayo fasihi hushughulikia ni sharti yawe yenye mashiko katika lugha ambayo itayawasilisha katika jamii husika. Lengo kuu la fasihi lieleweke kuwa ni kuangazia masuala yanayoathiri jamii husika kwa namna yoyote ile iwe ni kwa njia hasi au chanya. Msingi ni kuwa fasihi hiyo ni sharti ihusishwe na jamii kwa kuangazia yanayowahusu binadamu hao. Yote haya ni kwa vile lugha ni sehemu ya utamaduni wa watu. Ili kuelewa utamaduni wa watu basi lazima uelewe lugha yao kwa vile ndiyo sehemu kuu ya utamaduni wao.

### 1.7.0 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii.

Katika sehemu hii, tumeelezea yale ambayo yameandikwa kuhusu mtindo ambapo tumejadili kwa kifupi maoni ya baadhi ya wasomi kuhusu dhana mtindo. Vile vile, tumejadili yale ambayo wasomi waliotangulia wameandika kuhusu uhakiki wa kimtindo.

### 1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu mtindo

Kwa kweli mtindo ni dhana ambayo huenda ikawa na maana nyingi kulingana na wasanii mbalimbali. Ingawa tumeangazia baadhi tu ya maoni kuhusu mtindo, usisahau kuwa mtindo kwa kawaida ni namna ya kutekeleza jambo ama shughuli fulani. Maelezo yote kuhusu mtindo sharti

yazunguke kauli hii. Katika sehemu hii tunalenga kutathimini baadhi ya maelezo kuhusu maana ya mtindo kwa kurejelea maoni ya wasomi mbalimbali.

Kwa maoni ya Kazungu (1982) kuwa ingawa kuna maelezo mengi kuhusu maana ya mtindo, yote huzunguka tu dhana moja ambayo ni lugha. Kulingana naye, anakubaliana na dhana kuwa mtindo humaanisha ukiukaji wa ukawaida wa mawasiliano. Anaendelea kufafanua maoni ya wataalamu wa Prague kuwa, mtindo ni ule utumiaji wa lugha unaokiuka ukawaida wake. Anasisitiza kuwa mtindo ni vile vipengele ambavyo humtofautisha msanii na mwingine. Maoni hayo ya Kazungu hayamaanishi kuwa vipengele hivyo vinavyotofautisha wasanii huwa tofauti. La, vipengele hivi huwa sawa ila tu namna ya kuvitumia ili kusuka kazi ya kifasihi ndiyo hutofautiana kutoka msanii mmoja hadi mwingine. Kazungu (khj) anazidi kuelezea kuwa mtindo waweza ukachukuliwa kama njia ya msanii ya kujieleza katika kazi yake au njia ambayo msanii hutumia ili kuteua misamiati yake, namna ya kupanga maneno yake, sentensi na kisha kazi yake nzima. Mipangilio hii yote huwa ni kwa lengo la kujitambulisha katika kazi yake. Msimamo wa Kazungu ni kuwa, ni vipengele vya kimtindo peke yake ambavyo hudhihirisha ufasishi wa kazi za kifasihi. Maelezo haya ya Kazungu tumeyaunga mkono katika utafiti wetu kwa sababu kwa maoni yetu, sanaa haiwezi kuitwa sanaa bila kipengele cha ubunifu. Ubunifu wenyewe ndio hutokana na namna ambavyo msanii huteua misamiati yake, kuitumia na kuupamba ujumbe wake kwa tamathali za usemi mbalimbali. Kutokana na hayo katika utafiti wetu tumelenga kuhakiki mtindo wa mtunzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* ili kubainisha ubunifu wake. Kwa kifupi, katika utafiti wetu, tumelenga kubainisha umuhimu na nafasi ya mtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

Akihakiki mtindo wa lugha katika mashairi ya watungaji wateule wa Zanzibar Hamad (2017) anaeleza kuwa mtindo ni njia ya uwasilishaji au ufanyaji wa jambo au kitu. Kulingana naye, mbinu hizi hujitokeza katika fani zote za maisha ikiwemo mazungumzo, sanaa ya uchoraji na ushonaji wa mavazi. Hata hivyo maelezo haya ni ya kijumla mno kwani katika utafiti wetu dhana mtindo imenasibishwa na utumiaji wa lugha. Kulingana na Hamad (khj) kila utanzu wa fasihi pamoja na kila msanii huwa na mtindo wake wa kutumia lugha. Anaendelea kuelezea kuwa muundo wa lugha huelekeza mtindo wa lugha unaohitajika kutumika katika kazi ya kifasihi. Anasisitiza umuhimu wa mtunzi wa ushairi kutumia mitindo mbalimbali ili kuvutia wasomi wengi. Maelezo haya ni kweli kwa sababu, katika usanii wa lugha, mtindo ndio hupewa kipau mbele. Msanii yeyote ni sharti afinyange lugha yake katika matini yake kikamilifu ili kazi yake iweze kuvutia.

Wazo kuwa lugha ndio msingi wa fasihi ni dhihirisho kwa kauli kuwa lugha ni sehemu ya utamaduni wa watu. Hivyo basi iwapo fasihi itafaulu, ni sharti izingatie lugha na tamaduni za jamii lengwa. Ni ukweli usiopingika kuwa fasihi haiwezi ikaandikwa katika ombwe tupu bali inabidi ifumbatwe ikirejelea jamii fulani. Hamad (khj) katika utafiti wake, amebaini kuwa wasanii wote wametumia viambajengo vya lugha katika ngazi ya kifonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki katika utunzi wa kazi zao. Utafiti huu umehakiki matumizi ya vipengele vya kimtindo kama vile: tamathali za usemi, taswira, muundo, ambavyo tumevihakiki katika utafiti wetu.

### 1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu uhakiki wa kimtindo.

Uhakiki wa tenzi nyingi umefanywa na watafiti tofauti tofauti kwa malengo mbalimbali chini ya nadharia tofauti tofauti. Vile vile, kipengele cha mtindo pamoja na tamathali za usemi vimehakikiwa si tu katika tenzi bali hata katika vipera vingine vya fasihi kama vile riwaya, tamthilia, novela, hadithi fupi na ngano. Kwenye utafiti huu, tumehakiki vipengele vya kimtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Vipengele hivyo ni pamoja na usimulizi, mandhari, wahusika na uhusika wao, muundo, tamathali za usemi, mbinu rejeshi na taswira. Tumesoma misururu ya tafiti zinazohusiana na utafiti wetu zilizofanywa na watafiti wa awali. Tumetathimini matini zilizotafitiwa na nadharia zilizotumika katika kila kazi. Kisha tumetaja kwa kifupi umuhimu wa kila utafiti tuliorejelea katika utafiti wetu. Mwisho tumebainisha jinsi kila utafiti umelingana na kutofautina na utafiti wetu.

Akichanganua kipengele cha maudhui na mtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud,* Kithuku (2017) anafafanua jinsi mtindo na maudhui yamefanikisha utunzi wa utenzi huu. Utafiti huu ulitufaa kwa kutupa ufafanuzi wa baadhi ya vipengele vya kimtindo ijapokuwa katika utafiti wake amevifungamanisha na kipengele cha maudhui katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*, kama vile: wahusika na tamathali za usemi. Katika utafiti huu mtafiti amejikita katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* kama sisi. Ingawa hivyo, tafiti hizi ni tofauti kabisa kwani mtafiti huyu amehakiki maudhui na mtindo nasi tumehakiki mtindo peke yake. Pili, katika utafiti wake ametumia nadharia mbili ambazo ni umuundo na uhalisia ilhali katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo. Hata hivyo utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwetu kwa sababu ulituelekeza jinsi ya kuhakiki baadhi ya vipengele vya kimtindo ambavyo amevishughulikia kama vile wahusika na tamathali za usemi ambavyo ni baadhi ya yale tunayoshughulikia katika utafiti wetu. Katika utafiti wetu, tumehakiki

kipengele cha wahusika na tamathali za usemi ni baadhi ya vipengele vya kimtindo kwa sababu katika utafiti wa Kithuku vipengele hivyo vimeshughulikiwa kijuu juu.

Mazrui na wengine (2016) wanatuelekeza kuelewa jinsi lugha inavyotumika katika utunzi wa fasihi. Katika utafiti huu wametuelekeza kuelewa jinsi ya kuchambua na kuwasilisha data kimaelezo na kimaandishi kama mbinu iliyotufaa katika utafiti wetu. Watafiti hawa wameshughulikia baadhi ya vipengele vya kimtindo kama vile: tamathali za usemi na wahusika vipengele ambavyo tumehakiki vinavyojitokeza katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Vile vile, tafiti hizi zimetofautiana kinadharia ambapo katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo ilhali wao wametumia nadharia mbili ambazo ni fasihi ina kwao pamoja na ile ya uamilifu. Utafiti huu umetofautiana na wetu kwa vile watafiti hawa wamehakiki kazi ya kidini inayohusu tafsiri za kisiasa katika tamaduni za Waislamu wakirejelea Qurani takatifu nasi tumehakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

Kulingana na Faki (2015) akizamia vipengele vya fani kama vile: muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha katika utendi wa Kiswahili akirejelea *Utenzi wa Fumo Liyongo*, anaeleza kuwa tenzi za Kiswahili zina sifa sawa za kifani. Kutokana na utafiti huu, tuliongozwa na namna mtafiti huyu ameshughulikia muundo, mtindo, wahusika na mandhari kwani vipengele hivi ni baadhi ya vipengele vya kimtindo ambavyo tumevishughulikia katika utafiti wetu. Tofauti ni kuwa mtafiti huyu ameshughulikia *Utenzi wa Fumo Liyongo* ilhali katika utafiti huu tumeshughulikia *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Utafiti huu unatofautiana na wetu kinadharia kwani mtafiti huyu ametumia nadharia ya umuundo na ile ya ujumi wa Kiafrika ilhali katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo.

Kwa maoni ya Ali (2013) akihakiki vipengele vya fani katika mashairi ya Kiswahili kwa kulinganisha na kulinganua mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji, anaeleza ya kwamba mashairi ya watunzi hao yametofautiana katika matumizi ya mizani, kibwagizo, vina na muundo wa tarbia katika mashairi ya Haji Gora Haji dhidi ya mashairi ya Euphrase Kezilahabi ambayo ni huru. Hata hivyo kulingana naye, mashairi haya yamefanana kwani wote wametumia lugha ya mkato, taswira, wahusika pamoja na ucheshi. Utafiti huu umekuwa wa manufaa kwetu kwa sababu tulipata mwongozo wa namna ambavyo amehakiki kipengele cha mandhari katika ushairi, taswira, muundo katika ushairi na matumizi ya wahusika vipengele ambavyo tumevihakiki katika utafiti wetu. Tofauti ni kuwa mtafiti huyu amelinganisha na kulinganua ushairi wa arudhi

na ushairi huru ilhali katika utafiti wetu tunahakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud* kimtindo. Katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo ilhali katika utafiti wa Ali amejikita katika nadharia ya simiotiki na nadharia ya umaksi.

Naye Karanja (2014) katika uhakiki wake wa matumizi ya istiari, tashbihi na taashira katika *Diwani ya Sauti ya Dhiki* amebainisha wazi kwamba Abdilatif Abdalla ametumia istiari na tashbihi kwa lengo la kuafikia dhamira na maudhui katika mashairi yake. Vile vile, ametumia vipengele hivyo kuumba kazi yake kwani vilimsaidia kuunda misamiati mbalimbali iliyofanikisha diwani yake. Utafiti huu umekuwa muhimu kwetu kwani kutokana nao tulipata mwongozo wa kuhakiki vipengele vya kimtindo kama vile; istiara na tashbihi. Utafiti huu unafanana na wetu kwani nasi katika uhakiki wetu tumejikita katika nadharia ya umtindo. Tofauti ni kwamba katika utafiti wetu tumehakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud* ilhali Karanja amehakiki mashairi katika *Diwani ya Sauti ya Dhiki.*

Kulingana na Hamad (2017) akimnukuu Karanja (2014) anafafanua kwamba tamathali za usemi zimetumika kupamba lugha ya mashairi katika *Diwani ya Sauti ya Dhiki.* Vile vile, amebainisha nafasi ya tamathali za usemi zinavyotumika kwa ufundi wa hali ya juu kwa lengo la kufinyanga dhamira na maudhui kuhakikisha kuwa ujumbe haujitokezi wazi wazi kwa hadhira labda kwa kuhofia zogo. Katika utafiti huu, aligundua kuwa watunzi wa diwani mbili alizoshughulikia wametumia vijenzi vya lugha katika viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki kufanikisha kazi zao. Utafiti huu ulitupa mwongozo wa kuhakiki vijenzi vya kimtindo katika utenzi wetu. Utafiti huu unafanana na wetu kwani tamathali za usemi ni mojawapo ya vipengele ambavyo tumehakiki katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* kama kipengele cha kimtindo. Tofauti baina ya tafiti hizi ni kwamba mtafiti huyu amehakiki muundo wa lugha katika mashairi ya watungaji wateule wa Zanzibar ilhali katika utafiti wetu tumehakiki mtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Pili, Hamad (khj) katika utafiti wake ametumia nadharia ya umuundo na umuundo leo ilhali katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo.

Momanyi (1991) amehakiki *Utenzi wa Al- Inkishafi* kwa kuangazia matumizi ya taswira kama kielelezo cha uhalisia. Katika utafiti huu tulipata mwangaza wa kuelewa namna ya kuhakiki kipengele cha taswira katika utunzi wa kisanaa. Utafiti huu umetofautina na wetu kwa vile Momanyi amehakiki *Utenzi wa Al- Inkishafi* ilhali katika utafiti wetu tumehakiki *Utenzi wa Vita*

*vya Uhud*. Tofauti ya pili ni kuwa, tunaelekezwa na nadharia ya umtindo ilhali Momanyi ametumia nadharia ya Uhalisia.

Kwa mtazamo wa Gichamba (2005) katika uhakiki wake wa sifa za mashujaa na umuhimu wao kwa jamii zao akimlinganisha Fumo Liyongo na Shaka Zulu, amegundua kuwa wahusika hawa wana sifa zilinganazo kwa kiasi kikubwa. Tofauti zilitokea pale penye utabiri wa kuzaliwa kwao pamoja na kupata jiko. Vile vile, amegundua kuwa mashujaa hukuzwa na jamii husika. Utafiti huu kwa hivyo ulikuwa wa msaada mkubwa kwa utafiti wetu kwani mashujaa wameshughulikiwa kama wahusika katika utafiti huu kipengele ambacho tumeshughulikia katika utafiti wetu hivyo basi tumetathimini jinsi ambavyo amewasawiri mashujaa wake. Tafiti hizi zimefanana kwani zote zimejikita katika uhakiki wa tenzi za Kiswahili. Tofauti ni kwamba mtafiti huyu amehakiki *Utenzi wa Shaka Zulu* na *Utenzi wa Fumo Liyongo* ilhali katika utafiti wetu tumehakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud.*Tofauti nyingine ni kwamba mtafiti huyu amejikita katika nadharia ya umuundo ilhali katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo.

Kiptum (2017) amehakiki uyakinifu wa maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Katika utafiti wake, Kiptum aligundua kuwa maudhui yanajengwa kutokana na vijenzi vya kifasihi kama vile mtindo ambao unarejelea wahusika, msuko, mandhari, usimulizi, fani na kadhalika. Kutokana na utafiti huu tumeelewa namna ya kuhakiki vipengele vya kimtindo mtafiti huyu anavyohakiki kama vile: mandhari, usimulizi na wahusika. Tofauti na utafiti wetu ambapo tumetumia nadharia ya umtindo, mtafiti huyu katika utafiti wake amejikita katika nadharia ya uyakinifu wa kijamii. Matokeo ya Kiptum (khj) kuwa vijenzi vya kimtindo huwa na sehemu kubwa katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui katika kazi za kisanaa tunayaunga mkono katika utafiti wetu kwani mtindo ndio uti wa mgongo wa kazi ya kifasihi.

Naye Mbayi (2009) amehakiki fani katika *tenzi za Howani na Mwanakukuwa* za Zaynab Himid Mohamed. Mbayi, amehakiki vipengele vya fani zikiwemo methali, chuku, jazanda, sitiari, sadfa, tabaini, taswira, taharuki na kadhalika. Katika utafiti wake aligundua kuwa katika *Utenzi wa Howani na Mwanakukuwa* mtunzi ameufumbata utenzi huu akizingatia viambajengo vya muundo. Vile vile, amebainisha kuwa mtunzi huyu amezingatia kanuni za utunzi wa mashairi kulingana na wanamapokeo. Utafiti huu umetupa mwanga zaidi kuhusu uchambuzi wa tamathali za usemi, taswira, usimulizi, wahusika na uhusika wao na mandhari vipengele ambavyo tumevihakiki katika utafiti wetu. Utafiti huu umetofautiana na wetu kinadharia kwani Mbayi ametumia nadharia ya

umuundo ilhali katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo. Tofauti nyingine ni kwamba katika utafiti wetu tumehakiki vipengele vya kimtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* kinyume na utafiti huu ambapo Mbayi amerejelea kipengele cha fani katika *tenzi za Howani na Mwanakukuwa* za Zaynab Himid Mohamed.

Kulingana na Aloo (2018) katika uhakiki wake wa tamathali za usemi teule katika *Utenzi wa Qiyama* alibaini kuwa mtunzi wa utenzi huu ametumia takriri, tashhisi, na balagha kuwasilisha picha ya siku ya kiyama. Vile vile, alitambua kuwa mtunzi huyu alifanikiwa kutumia tamathali za usemi kwa weledi mkubwa akilenga kuweka wazi ujumbe wake kwa wale wasioelewa. Utafiti huu umetufaa kwa sababu tumepata mwongozo kuhusu namna kipengele cha tamathali za usemi kimeshughulikiwa kwani ni mojawapo ya vipengele tumehakiki katika utafiti wetu. Utafiti huu ni sawa na wetu kwani nadharia ya umtindo imetumika kuuhakiki nasi tumeitumia kuuhakiki utenzi wetu. Tofauti ni kwamba mtafiti huyu amejikita katika *Utenzi wa Qiyama* ilhali katika utafiti wetu tumehakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Pili, Aloo amehakiki matumizi ya tamathali za usemi teule ilhali katika utafiti wetu tumehakiki vipengele vya kimtindo ambapo tamathali za usemi ni mojawapo.

Makiri (2018) amehakiki wakati na uwasilishaji usemi kama vipengele vya usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Isa.* Katika utafiti wake amejikita katika vipengele viwili vya usimulizi kama vile wakati na uwasilishaji usemi. Mtafiti huyu alitambua kwamba usimulizi una dhima kuu katika ufinyanzi wa utenzi wake. Amegundua kuwa mbinu mbalimbali za wakati na uwasilishaji zimetumika. Kutokana na utafiti huu tumepata uelewa wa jinsi ya kuhakiki kipengele cha usimulizi kwani ni mojawapo ya vipengele tunavyohakiki katika utafiti wetu. Vile vile, tumepata mwelekeo wa kuhakiki mtindo na muundo kutokana na uhakiki wa Makiri. Utafiti huu unafanana na wetu kwani mtafiti huyu amejikita katika utenzi nasi pia. Pili, mtafiti huyu amehakiki baadhi ya vipengele vya kimtindo ambavyo tumevihakiki katika utafiti wetu kama vile: muundo, mtindo na usimulizi. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwani katika utafiti huu nadharia ya naratolojia imetumika kuuhakiki ilhali katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo.

Kwa maoni ya Ndumbu (2013) akihakiki matumizi ya takriri na sitiari katika *Utenzi wa Rasi'l ghuli*, takriri na sitiari zimejengana kusuka dhamira na maudhui ya *Utenzi wa Rasi' l ghuli.* Pili, mbinu hizi zimemsaidia msanii wa utenzi wenyewe kuafikia mtindo wa kazi yake. Utafiti huu ulikuwa mwelekeo kwetu kwa kutuelekeza jinsi ya kuhakiki takriri na istiari katika *Utenzi wa Vita*

*vya Uhud.* Tofauti baina ya tafiti hizi ni kwamba utafiti huu umeongozwa na nadharia ya umuundo ilhali katika utafiti wetu tumeongozwa na nadharia ya umtindo. Tofauti nyingine ni kuwa mtafiti huyu amehakiki *Utenzi wa Rasi'l ghuli* ilhali katika utafiti wetu tumehakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud*.

Naye Ilomo (2017) akiwa ameshughulikia mbinu za ujenzi wa wahusika na usawiri wa sifa zao katika *Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo* alitambua kuwa, kipengele cha wahusika hushirikishwa na vipengele vingine vya kifani ili kufanikisha dhamira na maudhui ya kazi yoyote ya kifasihi. Vile vile, alitambua kuwa msanii huwajenga wahusika wake kikamilifu kwa lengo la kufanikisha sanaa yake. Utafiti huu umekuwa muhimu kwetu kwani tumepata mwelekeo wa namna ya kujenga wahusika mojawapo ya vipengele vya kimtindo ambavyo tumeshughulikia katika utafiti wetu. Tofauti ni kwamba mtafiti huyu amehakiki *Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo* ilhali katika utafiti wetu tumehakiki *Utenzi wa* V*ita vya Uhud*.

Chaniro (2017) amehakiki matumizi ya lugha katika *Maulidi ya Jambeni*. Katika utafiti wake amegundua kuwa lugha ni uti wa mgongo katika usukaji wa kazi za kifasihi. Ametambua kuwa mtunzi wa Maulidi haya ametumia tamathali za usemi ili kupamba Maulidi yake. Kutokana na utafiti huu tumepata msingi wa kuhakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud* kwa kurejelea vipengele kama vile: muundo, mtindo, tamathali za usemi, na taswira. Katika utafiti huu nadharia ya umuundo imetumika ilhali katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo. Pili, Chaniro amehakiki matumizi ya lugha katika *Maulidi ya Jambeni* ilhali katika utafiti wetu tumehakiki mtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

Kulingana na Ngugi (2018) katika uhakiki wake wa maudhui na mtindo katika ushairi wa watoto akirejelea *Utenzi wa haki za watoto na Mashairi Bulbul,* amebainisha kuwa watunzi wa mashairi hayo wametumia vipengele vya kimtindo kama vile: matumizi ya lugha, muundo, toni na michoro ya rangi wakitilia maanani kiwango cha ukomavu wa watoto. Pili, ametambua kuwa watunzi husika walitumia miundo rahisi ya mashairi. Utafiti huu umekuwa wa msaada kwa kutupa mwongozo wa kuhakiki vipengele vya kimtindo kama vile: muundo, mandhari, mtindo na tamathali za usemi, vipengele ambavyo tumevishughulikia katika utafiti wetu. Katika utafiti huu nadharia ya uhalisia na umtindo zimetumika kuhakiki kazi husika ilhali katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo kuhakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud*.

Nyamari (2016) amezamia mtindo katika *Utenzi wa Katirifu* ambapo amehakiki wahusika na uhusika wao, uhuru wa mshairi, dayolojia, taswira, mandhari, tamathali za usemi kama vile: maswali ya balagha, tashihisi, chuku na sitiari. Mtafiti huyu ameshughulikia karibu vipengele vyote tunavyohakiki katika utafiti wetu. Katika utafiti wake amegundua kuwa tamathali za usemi humsaidia msanii katika kuwasawiri wahusika wake, usimulizi nao humsaidia msomaji kuelewa yatendekayo katika kazi ya fasihi. Utafiti huu umetufaa kwa sababu kutokana nao tumepata mwongozo wa kuhakiki vipengele kama vile: usimulizi, mandhari, wahusika na tamathali za usemi kwani vipengele hivi ndivyo tunavyohakiki katika utafiti wetu. Utafiti wetu na wa Nyamari ni sawa kwa msingi wa nadharia kwani nadharia ya umtindo ndiyo imetumika. Ingawa hivyo, utafiti huu ni tofauti na wetu kwani Nyamari ametafiti *Utenzi wa Katirifu* nasi tumezamia *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

Kwa maoni ya Soud (2016) katika uhakiki wake wa kipengele cha fani katika *Maulidi ya Nuni*, amebainisha wazi kuwa kuna wahusika wa aina mbalimbali katika maulidi haya wakiwemo wahusika wa kawaida, wahusika wasiokuwa wa kawaida, wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wadogo. Vile vile, amegundua uwepo wa matumizi murua ya tamathali za usemi mbalimbali kama vile: takriri, tashbihi, tashhisi, istiari, uhaishaji pamoja na chuku. Pia, amegundua kuwa muundo umezingatiwa kwa kuangalia umbo la utungo. Utafiti huu umekuwa wa msaada katika kazi yetu kwa sababu tumepata maelezo kuhusu vipengele kama vile: muundo, mandhari, na tamathali za usemi kwani ni baadhi ya vipengele tunavyohakiki katika utafiti wetu. Pili, katika utafiti huu mtafiti ametumia nadharia ya umtindo sawia na wetu. Tofauti ni kuwa katika utafiti wetu tumehakiki vipengele vya kimtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* kinyume na utafiti huu ambapo mtafiti amehakiki fani katika *Maulidi ya Nuni*.

Kemunto (2015) katika uhakiki wake linganishi wa sifa za mashujaa akiangazia Sakawa na Fumo Liyongo kama majagina katika jamii zao, amegundua kuwa sifa za mashujaa hawa zinalingana zaidi ukilinganisha na tofauti zao. Utafiti huu umefanana na wetu kwa vile umerejelea kipengele cha wahusika ambacho ni mojawapo ya vipengele tunavyorejelea katika utafiti wetu. Kazi hii imetufaa sana kwani kutokana nayo tumeelewa namna mashujaa hawa wamejengwa katika jamii zao na kuwafananisha na wahusika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Katika kazi yake anaeleza kuwa shujaa kwa kawaida huwa na maadui au wapinzani na hivyo kumlazimu kuonyesha ushujaa wake; kauli ambayo tunaitathimini kwa kumrejelea Mtume Muhammad kama mhusika mkuu

katika utenzi wetu. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwani mtafiti huyu amelinganisha wahusika wawili nasi tunaangazia vipengele vya kimtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

Naye Mohochi (2000) akihakiki *Usimulizi wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini* amebaini kuwa mtunzi wa riwaya hii ametumia mbinu ya usimulizi vizuri. Vile vile, ametumia ubunilizi wake mwenyewe kuepuka ukinai kutokana na usimulizi wa nafsi ya kwanza. Kulingana na Mohochi (khj) mtunzi wa riwaya hii amewapa wahusika wengine kando na Juma ambaye ni msimulizi mkuu, nafasi ya kuendeleza hadithi yake. Kutokana na utafiti huu tumepata mwongozo wa kuhakiki kipengele cha usimulizi kwa kurejelea dhana usimulizi, aina za usimulizi pamoja na wahusika na uhusika wao kwani ndivyo vipengele tunavyoshughulikia katika utafiti wetu. Tofauti ni kwamba mtafiti huyu amehakiki riwaya ilhali katika utafiti wetu tumehakiki utenzi.

Kwa maoni ya Muthoni (2014) katika uhakiki wake wa *Maudhui na Mtindo katika Tikitimaji,* mtunzi ametumia tamathali za usemi kama vile: tashbihi, tashhishi, nidaa, takriri na sitiari kwa ustadi wa hali ya juu kwa lengo la kupamba kazi yake. Utafiti huu umetufaa kwani tumepata msingi wa kuhakiki tamathali za usemi kama kipengele kimojawapo cha kimtindo tunachohakiki katika utafiti wetu. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa misingi kuwa mtafiti huyu ametumia nadharia mbili kuhakiki kazi yake ambazo ni: nadharia ya uhalisia na umtindo ilhali katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya umtindo. Pili, Muthoni amehakiki maudhui na mtindo ilhali katika utafiti wetu tumehakiki mtindo.

### 1.8.0 Mbinu za utafiti

Kwa sababu utafiti wetu ni wa kiusomi, tulisoma na kuuchanganua utenzi wenyewe ili kubainisha namna ambavyo msanii ametumia mtindo. Vile vile, tulipitia makala mbalimbali katika mtandao ili kubaini historia halisi ya utenzi wenyewe. Katika sehemu hii, tumejadili mikakati yote ya utafiti huu na ufaafu wake katika utafiti wetu. Tumeelezea mbinu za kukusanya data, jinsi ya kuzichanganua na kisha namna ya kuziwasilisha. Sehemu hii tumeigawa katika vijisehemu vitatu kama ifuatavyo:

### 1.8.1 Mbinu za ukusanyaji data

Abdalla (2016) anaeleza kuwa hatua ya ukusanyaji data katika utafiti wowote ni muhimu iwapo mtafiti atalenga kufaulu. Hatua hii ni sharti imsaidie mtafiti kupata data ambazo zitamfaa na kuafikia malengo ya utafiti wake. Ili uchambuzi na uwasilishaji wa data ufaulu, sharti ukusanyaji wa data kufaulu. Iwapo ukusanyaji data utafeli, basi bila shaka utafiti wote utafeli, yaani hautatoa

picha halisi. Maoni ya Abdalla tunayaunga mkono kwa sababu, kimsingi, lengo la kufanya utafiti wowote ule ni kutambua shida au changamoto iliyoko katika jamii na kutafuta namna ya kupata suluhu ya kudumu. Ni dhahiri shairi kwamba, data ambazo haziwezi kutegemewa katika utafiti haziwezi kumpatia mtafiti picha halisi kuhusu hali ilivyo mashinani au maktabani na kwa hivyo mwisho utafiti huo huishia kutosuluhisha changamoto iliyokusudiwa. Hivyo, ni muhimu sana kwa mtafiti kuhakikisha kuwa amepata data ambazo zitamfaa zaidi katika utafiti wake.

Katika utafiti wetu tulichagua *Utenzi wa Vita vya Uhud* kimakusudi ili kuuhakiki kimtindo. Kama tulivyotaja hapo awali, data muhimu zaidi katika utafiti wetu zilitokana na kusoma na kuchambua *Utenzi wa Vita vya Uhud* ili kuhakiki namna wahusika na uhusika wao, taswira, muundo, usimulizi, tamathali za usemi na mandhari vimetumika kama vipengele vya kimtindo ili kufanikisha utenzi huu. Baadaye tulipitia kazi mbalimbali ambazo ni pamoja na tafiti za awali, makala, majarida, vitabu, tasnifu ambazo zilikuwa za manufaa katika uboreshaji wa utafiti wetu. Data mbalimbali mtandaoni na hata katika maktaba mbalimbali vile vile zilitufaa katika utafiti wetu. Wakati mwingine ililazimu kusoma tenzi nyingine za kale, ambazo zinahusiana na utafiti wetu kwani ndizo zimeweka msingi wa utenzi wa Kiswahili kwa jumla. Ni muhimu pia kutaja kuwa katika utafiti wetu tulirejelea makamusi mbalimbali ambayo yalitupa ufafanuzi wa dhana mbalimbali ambazo zinahusiana na utafiti wetu.

Njia nyingine ya kukusanya data ilikuwa ni kutafuta maoni kutoka kwa wasomi wa lugha ya Kiswahili, haswa utenzi kama vile wahadhiri wetu na wa vyuo vingine tuliowapata. Pia, tuliomba usaidizi kutoka kwa wataalamu wa fasihi kwa sababu vipengele tulivyorejelea katika utafiti wetu vimejikita katika fasihi.

### 1.8.2 Mbinu za uchambuzi wa data.

Uchambuzi ni kule kufafanua data ama maoni aliyopata mtafiti alipokuwa maktabani au nyanjani. Uchambuzi huu hulenga kupanga na kufasiri data zilizopatikana ili kutambua iwapo zimeafiki mada inayotafitiwa. Ili data iliyokusanywa kuwa na maana, ni sharti ichambuliwe ndipo iweze kuwasilishwa kwa umma kusudiwa. Katika hatua hii tulijikita katika *Utenzi wa* V*ita vya Uhud*. Tuliusoma utenzi huu kwa makini na kuchunguza namna vipengele vya kimtindo vimetumika ili kufanikisha uwasilishaji wa dhamira na maudhui ya utenzi wenyewe. Maelezo ya wazi kuhusu namna vipengele vya kimtindo vimetumika katika utenzi huu yametolewa kwa namna inayoeleweka. Katika uchambuzi na uhakiki wa kazi za kifasihi lengo huwa ni kumsaidia msomaji

kuzielewa au kupata uelewa fulani juu ya kazi zenyewe. Katika utafiti wetu pia tumelenga kurahisisha uelewa wa *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

### 1.8.3 Mbinu za uwasilishaji wa data.

Matokeo ya data hizo yamewasilishwa kimaandishi na kiufafanuzi, huku tukizingatia nadharia ya umtindo kuwasilisha vipengele vyote vinavyoshughulikiwa katika utafiti huu. Wakati mwingine katika uwasilishaji wetu ilipolazimu tulidondoa beti mbalimbali kwa lengo la kutoa ithibati ya jinsi vipengele mbalimbali vya kimtindo vimejitokeza katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura hii tumetoa utangulizi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* na historia yake kwa kifupi. Tumedokeza tatizo letu la utafiti ambalo limefuatwa na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka ya utafiti wetu, tumeeleza msingi wa nadharia ya umtindo na mihimili yake ambayo imeongoza utafiti wetu, yaliyoandikwa kuhusu mtindo na yaliyoandikwa kuhusu uhakiki wa kimtindo pia yameshughulikiwa, kisha mbinu za utafiti na za uwasilishaji wa data za utafiti huu. Katika sura inayofuata tumechambua na kueleza dhana muhimu ambazo zimekuwa za manufaa katika utafiti wetu.

## SURA YA PILI

## UFAFANUZI WA DHANA MBALIMBALI KATIKA UTAFITI WETU.

### 2.0 Utanguzlizi

Katika sura hii tumejadili dhana mbalimbali ambazo tumetumia katika utafiti wetu. Dhana hizo ni kama vile: ushairi, utenzi, mtindo, muundo, tamathali za usemi, wahusika, mandhari na usimulizi. Dhana hizi tumezitumia kwa lengo la kufanikisha utafiti wetu. Maelezo ya dhana hizi yametumika hapa na pale katika utafiti wetu kadri ya vile tumeyaeleza katika sura hii. Dhana hizo na maelezo ni kama zifuatavyo:

### 2.1 Ushairi

Ushairi ni mojawapo ya vipera vya fasihi ambacho kimekuwa muhimu katika jamii za Waswahili tangu jadi. Ushairi umekuwa njia muhimu ya mawasiliano tangu jadi hata leo. Ingawa mashairi ya kitambo yanaaminika kuwa katika mfano wa nyimbo ambapo uteuzi wa maneno ulizingatiwa ili kuleta mahadhi kwa lengo la kuvutia sikio, hili si hoja kwa wasikilizaji kwani haja yao kubwa ni kupata ujumbe. Ni muhimu kutaja kuwa kuelezea maana ya dhana ushairi wakati mwingine hukanganya. Sababu kuu ikiwa tofauti baina ya wasanii kuhusu namna ya kupanga mawazo yenyewe katika shairi. Kuna kundi linaloshikilia kuwa shairi lazima lizingatie vina na mizani na kundi lingine linapinga kwa madai kuwa arudhi huwanyima washairi chipukizi nafasi ya kujitosa katika ulingo wa utunzi. Hata hivyo, katika sura hii tumejadili maoni ya wasomi mbalimbali kuhusu dhana ushairi kama ifuatavyo:

Kulingana na wasomi wanaounga mkono ushairi wa kimapokeo akiwemo Robert (1958), Abdalla (1973) na Massamba (1983) wanauona ushairi kama utungo wenye umbo maalumu lenye mpangilio wa beti, vina na mizani na ambao sharti utumie lugha ya mkato na yenye mnato. Kwa upande mwingine wataalamu wa ushairi huru akiwemo Topan (1973) na Mulokozi na Kahigi (1979) nao wanauona ushairi kama utungo wa kisanii ambao si lazima ufuate arudhi bali ni sharti utumie lugha ya mkato na yenye mnato. Bila shaka maoni hayo yanadokeza mzozo mzima baina ya pande mbili ambazo ni wanamapokeo na wanausasa. Hata hivyo kuna ule uelewano kwamba shairi sharti liwe na mpangilio wa maneno yenye mkato. Inadhihirika wazi kuwa namna ya uwasilishaji wa ujumbe katika shairi ni sharti iwe ya kuvutia. Katika utafiti huu hatutazingatia mgogoro huo kwani si mojawapo ya malengo yetu.

Wanyama na wengine (2006) akimnukuu Mnyampala (1965) ameeleza kuwa ushairi ni utungo wenye maneno ya busara. Anazidi kufafanua kuwa utungo huu hutumia lugha ya mnato kuwasilisha ujumbe wake kwa lengo la kutoa mwongozo kwa jamii lengwa. Mpangilio wa vina na mizani ni sharti uwe kwa urari unaovutia sikio. Maoni haya tunayaunga mkono kwamba mbali na kuburudisha, ushairi pia ulilenga kutoa nasaha na kuimulika jamii kwa kuikosoa kama ilivyo katika fasihi yoyote ile. Ingawa hivyo, katika uelewa wetu, shairi ni namna ambavyo msanii hutoa mawazo yake kwa wasikilizaji kwa njia anayoipenda kimaandishi ama kimapokezi mradi tu ujumbe uliofumbatwa uwe mfupi na wenye mnato. Kulingana nasi mashairi yote yawe ya jadi au ya kisasa yana nafasi sawa katika jamii kwa sababu yote hutoa mausio muhimu katika jamii. Hata hivyo katika utafiti wetu tumejikita katika shairi la *Utenzi wa Vita vya Uhud* ambalo linazingatia arudhi.

Naye Wellek (1933) anaeleza shairi kama utungo unaotumia maneno kwa mpangilio maalum na kwa ufundi wa hali ya juu kwa lengo la kuwasilisha habari nzito kwa jamii husika. Naye Pribady (2017) mbali na maelezo kuwa ushairi ni taaluma, anasisitiza kuwa ushairi ni utungo wa mwanzo kabisa kuliko tungo nyingine za fasihi simulizi. Kanema (2015) naye anaeleza kuwa ushairi ndio umekuwa chombo muhimu cha kuhifadhia falsafa, tamaduni na historia ya jamii. Historia na tamaduni hizi zilifaa kupitishwa kutoka kizazi hadi kizazi kimapokezi. Ndiyo maana zilikaririwa watoto ili wazielewe na kuzihifadhi bongoni mwao ndipo nao wazipitishie kizazi kitakachowafuata. Hali hii ilitokana na kutokuwepo na mbinu ya kimaandishi ya kuzihifadhi.

Kwa mtazamo wa Omari (2014) akimnukuu Harries (1962) anaeleza kuwa ushairi ni kama taaluma iliyokamilika katika kuelezea ukweli wa maisha katika jamii lengwa. Maoni ya Omari (khj) yanalingana na ya Raffel (1984) anayesema kwamba, ushairi tangu jadi umekuwa chombo muhimu cha kuhifadhia historia, falsafa na hata tamaduni za Waswahili. Maoni ambayo ni kweli kwa vile ukitathimini matumizi ya mashairi katika jamii utatambua kuwa yanatumika katika mawasiliano hasa kutoa nasaha na mwongozo katika jamii. Zaidi ya hayo, miktadha ya matumizi ya mashairi ambayo ni katika sherehe mbalimbali kama vile: sherehe za mazishi, ndoa, jando, mavuno na kadhalika ni dhihirisho kwamba mashairi ni utamaduni wa watu. Omari (khj) akimnukuu Olson (1975) anaeleza kuwa ushairi wa Kiswahili ni chombo cha kuhamisha matarajio na matamanio ya jamii ya uswahilini kwa jumla kwa lengo la kujiendeleza. Anasisitiza kwamba ushairi wa Kiswahili umechukua nafasi kubwa kama chombo cha mawasiliano baina yao tangu

jadi. Ingawa hivyo, katika uelewa wetu, ushairi ni namna ambavyo msanii hutoa mawazo yake kwa wasikilizaji kwa njia anayoipenda mradi tu ujumbe uliofumbatwa uwe mfupi na wenye mnato. Kulingana nasi mashairi yote yawe ya jadi au ya kisasa yana nafasi ijapokuwa katika utafiti wetu tumejikita katika shairi la utenzi ambalo ni la kiarudhi.

Kuna aina mbalimbali za mashairi yakiwemo mashairi ya kiarudhi na yale ya kisasa. Mashairi ya arudhi pia yameainishwa katika aina mbalimbali kwa kuzingatia idadi ya mistari na mpangilio wa mizani na uwepo wa mkarara kama vile: ngonjera, kikwamba, utenzi, pindu, takhimisa, tasdisa na kadhalika. Katika utafiti wetu tumeangazia shairi la utenzi ambapo tumeeleza maana hapo chini.

## 2.2 Utenzi

Kulingana na maoni yetu, utenzi au utendi ni utungo wenye maudhui yasimuliwayo kwa kirefu kuhusu tukio fulani la kihistoria au mhusika fulani ambaye aghalabu huwa ni shujaa katika jamii fulani. Kwa kawaida utenzi huwa na beti nyingi zaidi ya ishirini na huwa na mizani nane au sita lakini si zaidi ya kumi na mbili katika kila mshororo. Mishororo yake huwa haigawiki kwani haina vina vya kati bali vya nje peke yake. Utenzi huwa na urari wa vina ijapokuwa kina cha mwisho katika mshororo wa nne wa kila ubeti kinachoitwa kina cha bahari huwa hakibadiliki katika utenzi mzima.

Kulingana na Abedi (1954) utenzi ni shairi ambalo huwa na mizani chache kuliko kumi na mbili ambalo aghalabu huwa halina vina vya kati kwenye mishororo yake, ila katika kila ubeti huwa na vina vinavyofanana kwenye mishororo isipokuwa katika mshororo wa mwisho wa kila ubeti, ambao huwa na kina cha bahari kinachofanana katika utenzi mzima.

Kwa maoni ya Wanyama (2006) anaeleza utenzi kama shairi refu la masimulizi linalozungumzia kwa kirefu na kwa mtindo wa upeo, matendo ya majagina au jagina mmoja. Kwa maoni yake utenzi huwa na sifa chungu nzima kwani unaweza ukaleta pamoja hadithi za kishujaa, visasili na mighani. Maoni haya ni kweli ijapokuwa tenzi nyingine vile vile zinahifadhi masuala ya kihistoria ambayo ni muhimu katika jamii ya Waswahili pamoja na tamaduni zao mbalimbali.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa huenda utungo wa utenzi wa kwanza kutungwa ni ule wa *Utendi wa Mwnamanga*. Kauli hii hata hivyo haina uthibitisho wowote kwa kukosa rekodi ya tarehe ya uchapishaji wa utendi huo. Kwa kifupi, ni vigumu kutambua utenzi wa mwanzo kabisa kuandikwa kwa sababu ya kizingiti cha tarehe ya uchapishaji. Vile vile, ni muhimu kutambua kuwa huenda

kulikuwa na tenzi nyingi ambazo zilitungwa zamani na kukosa kuchapishwa. Hata hivyo *Utenzi wa Fumo Liyongo* unapigiwa upatu kuwa wa awali ulioandikiwa zaidi ijapokuwa suala la terehe pia huzua utata. Katika utafiti wetu hata hivyo hatutajihusisha na mjadala huu kwani utafiti wetu hauna uhusiano wowote nao.

### 2.3 Mukhutasari wa Utenzi wa Vita vya Uhud

*Utenzi wa Vita vya Uhud* ni utenzi ambao unasimulia vita baina ya Waislamu na Makureshi. Ni mojawapo ya vita maarufu Mtume Muhammad aliwahi kushiriki. Ni vita vilivyotokea nje ya mji wa Madina karibu na mlima Uhud. Katika vita hivi imedhihirika wazi kuwa Waislamu walishindwa na Makureshi. Kabla ya masimulizi ya vita vya Uhud msanii anatusimulia vita vya Badri vilivyotangulia vita vya Uhud ambapo inadhihirika wazi kuwa Mtume Muhammad alipata ushindi mkubwa dhidi ya Makureshi. Baada ya kushindwa, Makureshi wakala kiapo kulipiza kisasi. Waliporejea makwao walianza maandalizi ya kivita. Walipanga zana mbalimbali za kivita pamoja na kuandaa jeshi kubwa ili kuwakabili Waislamu kikamilifu. Baada ya miezi tisa ya maandalizi kukamilika, wakatuma ujumbe kwa Mtume Muhammad kuwa tayari kwa pambano la Uhud.

Baada ya Mtume Muhammad kupata habari kutoka kwa Makureshi kuwa walikuwa tayari kupigana vita vya Uhud, bila kupoteza muda akaita jeshi lake ili kuwaandaa. Kabla ya pambano kung'oa nanga, wanajeshi mia tatu wa Mtume Muhammad walimsaliti kwani walihepa kabla ya Mtume Muhammad kumaliza sala ya alfajiri. Hata hivyo, Mtume Muhammad hakusitisha pambano. Alipanga wanajeshi hamsini kuchunga njia za milimani ilhali wengine wakapewa majukumu mengine. Baada ya mashujaa wa Mtume Muhammad waliowekwa kuchunga njia za milimani kutotii, mashambulizi ya Makureshi yalizidi na kupelekea kushindwa kwa jeshi la Mtume Muhammad. Pambano lenyewe lilipokamilika, visa kadha vya mauaji kutoka pande zote mbili vilidhihirika ijapokuwa maafa mengi yaliwapata wanajeshi wa Mtume Muhammad kuliko jeshi la Makureshi. Ni muhimu pia kuelewa kuwa katika vita hivi, Mtume Muhammad alipata majeraha makubwa kichwani pamoja na kinywani.

### 2.4 Mtindo

Mtindo ni dhana inayoeleza njia au namna ya kutekeleza jambo au kitu. Mtindo hubainika kutokana na jinsi binadamu huvaa, hujenga, huchora na jinsi anavyotumia lugha. Katika utafiti

wetu dhana umtindo inahusishwa na fasihi. Mtindo katika fasihi hutumiwa kama nembo na kila msanii.

Kulingana na Hamad (2017) mtindo ni namna ya kuwasilisha jambo. Njia hizo huweza kjitokeza katika hali ya kawaida ya maisha katika jamii. Hata hivyo, katika utafiti wetu dhana mtindo tumeihusisha na lugha. Kwa kifupi, mtindo ni mbinu, stadi au ubingwa anaotumia msanii ili kujieleza katika ujumbe wake kwa wasomaji wa kazi yake ya kisanii. Ubingwa wenyewe huhusisha vipengele vyote vya lugha kwa jumla. Kulingana na matumizi maalum ya vipengele hivi kwa kila msanii, msomaji huwa na uwezo wa kumtambua msanii kutokana na kazi zake hata kabla ya kumwona kimachomacho. Kwa kweli, lugha ni kipengele muhimu katika fasihi kwa sababu mawasiliano hutokea tu pakiwa na lugha. Lugha ni malighafi ya msanii yeyote kwani ni sharti aichukue na kuifinyanga kwa mtindo wake maalum kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake.

Kulingana na Leech na Short (2007) mtindo ni jinsi lugha inavyotumika na wanajamii. Maelezo haya yanashabihiana na dhana ya utendaji *(parole)* iliyoelezwa na Saussure. Aidha, wanaeleza kuwa mtindo ni jinsi lugha inavyotumiwa na msanii kwa njia ya kipekee ambayo huwatofautisha waandishi wa kifasihi. Kwa maoni yetu, mtindo ni namna au jinsi maalum msanii hutumia lugha kisanii ili kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake. Lugha hii ya kisanii inatofautiana na ile ya kawaida kwa sababu ina misururu ya mbinu na tamathali mbalimbali zinazofinyangwa na msanii kwa jinsi yake maalum.

**2.5 Muundo**

Kwa maoni yetu muundo ni dhana katika fasihi inayorejelea namna ambavyo kazi za kisanaa huwasilishwa kimaandishi au kimapokezi. Muundo ni mwonekano wa kazi yenyewe kimaandishi. Aghalabu muundo huhusu vipengele mbalimbali vinavyojenga kazi husika kama vile: mishororo, beti, msuko, na kadhalika. Katika utafiti wetu tumechunguza namna ambavyo mtindo unavyodhihirika katika utenzi wetu. Wasanii mbalimbali nao wametoa maoni mbalimbali kuhusu dhana muundo tunavyoeleza hapa chini.

Kwa maoni ya Hamad (2017) muundo ni mfumo wa lugha au mpangilio maalum wa lugha katika vitengo mbalimbali vya sarufi. Mpangilio huu ndio tu utakaowasilisha maudhui ya msanii kwa njia aliyokusudia. Naye Wanyama (2016) vile vile anaelezea muundo kama uhusiano wa vipengele

vya kazi ya kifasihi katika mpangilio unaoleta mshikamano unaokubalika. Anazidi kusisitiza kuwa ili msomaji aweze kuelewa kazi ya kisanii kikamilifu ni sharti aisome kazi yenyewe kikamilifu ili aweze kuuelewa muundo wake.

Wataalamu mbalimbali kama Crystal (1971), Lyons na John (1995) na Katamba (1978) wameeleza kuwa muundo ni mpangilio wa lugha katika vitengo mbalimbali vya kisarufi. Starobinski (1979) naye anaeleza muundo kama mfumo wa lugha ambao una sehemu nyingi ndanimwe zinazojitokeza katika viwango vyote kuanzia cha chini hadi cha juu. Kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Vipengele hivi vina uhusiano usiopingika. Mpangilio huu kulingana naye ni wa kijumla yaani unadhihirika katika lugha zote za ulimwengu ijapokuwa kila lugha huwa na sarufi yake.

Katika utafiti wetu, kipengele cha muundo tumekishughulikia kwa kutathimini mipangilio ya silabi, vina, mistari pamoja na beti ili kufanikisha maudhui katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Katika utafiti wetu pia tumetathimini umuhimu wa uhusiano wa vipengele hivyo katika utenzi huu.

**2.6 Tamathali za usemi**

Kulingana na Omari (2014) tamathali za usemi ni semi fupi fupi, maoni ambayo yanalingana na ya Njogu na Chimerah (1998) wanaoeleza kuwa tamathali za usemi ni semi fupifupi ambazo hudokezwa kimafumbo ili kuwasilisha dhamira kusudiwa kwa njia yenye mnato na inayochochea fikra ili kuelewa maana halisi. Tamathali za usemi ni nyingi ila tumeshughulikia zile ambazo zinahusu utafiti wetu ambazo ni pamoja na tashbihi, takriri, chuku, kinaya na kadhalika. Matumizi ya tamathali hizi kwa kweli humwezesha msanii kuchagua mtindo au muundo wa shairi analolitunga.

Muthoni (2014) akiwanukuu Senkoro (1982), Mbatiah (2001) na Wamitila (2003) anafafanua kuwa tamathali za usemi ni nahau, semi au kauli ambazo hutumiwa na waandishi wa fasihi kwa lengo la kukweza ubora au ujumi wa kazi zao. Pia, anaziita ukiushi wa kimakusudi wa jinsi lugha hutumiwa kwa kuzingatia maana pamoja na mpangilio wa maneno kwa lengo la kuwasilisha ujumbe hitajika. Utafiti wetu umetilia maanani maoni hayo kwani tumetathimini namna mipangilio ya sentensi imepangwa katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

### 2.6.1 Taswira

Kwa maoni yetu, taswira au jazanda ni picha ambazo hujengwa akilini mwa msomaji wa kazi za kifasihi kwa mfano: utenzi, riwaya, tamthilia, novela, hadithi fupi na nyinginezo. Picha hizo hujengeka kwa kutumia mpangilio maalum wa maneno au sentensi kwa lengo maalum.

Kulingana na Hamad (2017) akiwanukuu Mulokozi na Kahigi (1979), Mohamed (1995) anafafanua taswira kama jinsi ya kuwasilisha picha bongoni mwa msomaji au msikilizaji kwa kutumia maneno hasa ya kitamathali ili kuathiri fikra za msomaji au msikilizaji wa kazi yake. Picha hizi aghalabu humfanya msomaji ama msikilizaji kunusa, kuonja, kuona, kushika hata kuhisi akihisi hali isiyo mbali na hali halisi. Katika utafiti wetu picha za kuona, kuhisi zimedhihirika wazi wazi tangu mwanzo wa utenzi wenyewe hadi tamati. Lengo letu kuu limekuwa kuzibaini na kueleza umuhimu wake katika utenzi wetu.

Kwa mtazamo wa Salem (2019) taswira ni picha ya jambo ambalo humjia mtu akilini baada ya kusoma kazi ya kisanaa. Maoni haya ya Salem yanapiga mwau maelezo ya Hamad (khj) nasi tunayaunga mkono ijapokuwa picha tunazorejelea katika fasihi ni zile zinazoirejelea jamii husika na kuisawiri ilivyo. Katika hali hii basi, fasihi hutekeleza wajibu wake wa kuirudi na kuirekebisha jamii. Katika utafiti wetu hata hivyo, tumechunguza picha mbalimbali kwa lengo la kudhihirisha namna vita vya Uhud vilitokea.

Kulingana na Massoud (2013) taswira ni namna ya kutumia maneno yaliyoteuliwa kwa njia ya upekee kwa lengo la kuwasilisha ujumbe wake mzito kwa hadhira yake. Kulingana naye, taswira ni jina jingine la jazanda. Jazanda huwa ni muhimu sana katika uwasilishaji wa ujumbe kwa njia fiche inayomlazimu msomaji kumakinika anaposoma kazi ya kifasihi. Kulingana na Massoud (khj) kuna aina mbalimbali za taswira nazo ni kama vile: Taswira za kimaelezo ambazo ni picha zile zilizo na maana rahisi kueleweka kwani hazina maana ziada. Pili, kuna Taswira za kiishara ambazo Massoud (khj) amezipanga katika makundi matatu. Makundi hayo ni kama vile:

Taswira zile zilizo na mtazamo wa macho. Mara nyingi hizi ni zile zinazotokana na kutizama umbile la kitu na kubashiri picha yake halisi.

Taswira zile ambazo zina mnuso. Taswira hizi hujengeka katika akili ya msomaji hadi msomaji kudhania kuwa amenusa harufu ya kitu chenyewe.

Taswira zile zinajenga fikra ya mguso. Hapa msomaji hupata picha ya kukigusa kitu na kuelewa hali halisi ya kitu kinavyohisika kama aliyekigusa.

### 2.6.2 Tashbihi

Kwa mtazamo wa Kithuku (2017) tashbihi ni kule kulinganisha vitu kwa kutumia vifananishi kama vile: ja, tamthili, bimithili, falau, kama, mfano wa, falau ya, lau na kadhalika. Tashbihi ni mojawapo ya mbinu za kifasihi ambazo msanii yeyote hutumia kuboresha kazi yake. Maoni haya yanaungwa mkono na Senkoro (1982) na Wamitila (2003). King'ie na Kemoli (2001) nao wanaeleza kuwa tashbihi ni ufananisho wa vitu halisi kwa kuonyesha mshabaha fulani katika sura au tabia. Kulingana nasi, mbinu hii hufananisha vitu viwili visivyo na uhusiano wowote kwa kubandika kitu kimoja sifa ya kitu kingine. Ni mbinu ambayo hutoa msisitizo wa jambo zaidi katika kazi za kisanaa.

### 2.6.2 Takriri

Kulingana na Massoud (2013) takriri ni kule kuradidi hoja, sauti, maneno au hata sentensi kwa lengo la kusisitiza jambo au suala linalozungumziwa. Muthoni (2014) naye anaeleza takriri kama urudiaji wa sauti, maneno au sentensi katika kazi ya kifasihi. Takriri aghalabu hutumika kwa lengo la kusisitiza ujumbe fulani. Maoni hayo tunayaunga mkono lakini pia ili mahadhi ya ushairi kudumishwa ni sharti msanii apange silabi zake kwa mtindo unaoleta kiimbo anachokipendelea. Katika utenzi wetu kuna takriri za aina mbalimbali ambazo tumezifafanua kwa kirefu katika utafiti wetu. Lengo kuu la takriri ni kudumisha mahadhi katika ushairi.

Kulingana na Ntarangwi (2004) na Wamitila (2003) takriri ni tamathali ambapo mtunzi hurudiarudia maneno, sauti, wazo au vifungu katika utunzi wake. Kuna aina mbalimbali za takriri kwa mfano: takriri konsonanti, irabu, msitari, neno na kadhalika. Mbinu hii hutumiwa kwa lengo la kusisitiza ili msomaji aelewe ujumbe ambao mtunzi hukusudia kusema. Neno takriri ni neno litokanalo na kitenzi kariri. Ni mbinu ambapo mofimu, neno au sentensi hurudiwarudiwa kwa lengo la kusisitiza.

## 2.7 Wahusika

Dhana wahusika inamaanisha viumbe, vitu au vifaa ambavyo msanii hutumia katika kazi yake ya kisanaa kwa lengo la kuwasilisha dhamira na maudhui yake. Wahusika ni kipengele muhimu cha

kimtindo kwani humsaidia msanii kuzungumza na hadhira yake. Hivyo, wahusika husawiriwa na msanii kwa lengo la kuafikia malengo yake.

Kithuku (2017) akimnukuu Foster (1972) ameainisha wahusika katika makundi mawili makuu. Kundi la kwanza ni lile la wahusika duara na la pili ni la wale wahusika bapa. Anazidi kufafanua kuwa wahusika bapa huwa hawabadiliki kuanzia mwanzo wa hadithi hadi mwisho ilhali duara ni wahusika katika kisa ambao hubadilikabadilika kadri hali inavyozidi kubadilika. Kulingana naye, wahusika duara hupigiwa upatu kuwa ndio wanaokaribiana na binadamu halisi. Aina zote hizi za wahusika zimedhihirika katika utenzi wetu ambapo Mtume Muhammad akiwa ndiye mhusika bapa ilhali baadhi ya majemedari wa Makureshi waliobadili nia na kusilimu na kumfuata Muhammad waliyempinga awali wakiwa ndio wahusika duara.

Kulingana na Njogu na Chimerah (1998) wahusika huwa ni sehemu ya fani ya msanii na aghalabu msanii huwabuni kutokana na mandhari yake. Msanii sharti awajenge wahusika wake katika mandhari yatakayomsaidia kuafikia matamanio yake ya kiutunzi. Maoni haya tunayaunga mkono kwani msanii yeyote sharti atumie wahusika kutokana na mazingira yake kuwasilisha maoni yake kisanii. Vile vile, katika utenzi huu msanii amefanikiwa sana kuwabuni wahusika wake kwa mandhari kusudiwa.

Wahusika ni watu, wanyama au vitu anavyotumia mtunzi kupitishia ujumbe wake katika hadhira yake. Wahusika katika kazi yoyote ya fasihi, ndio hubeba dhamira ya mtunzi haya ni kulingana na Wamitila (2002) na Senkoro (1983).

Kwa maoni ya TUKI (1998) wahusika katika fasihi ni kama watu, miti au viumbe viwakilishavyo watu katika kazi ya kifasihi. Wanapotumiwa katika fasihi, hulenga kuwakilisha hali inayokaribiana na uhalisia wa maisha ya adinasi katika jamii. Yaani, hulenga kumulika jamii ilivyo. Rono (2013) anasisitiza kuwa wahusika wa kisanaa hubuniwa kwa lengo la kuwakilisha dhana mbalimbali katika jamii. Wahusika hao husawiriwa kwa kuzingatia sifa walizo nazo, namna walivyo na misimamo yao kuhusu masuala mbalimbali.

### 2.8 Mandhari

Mandhari ni hali inayozunguka jambo fulani. Mandhari yanaweza yakawa ya kiuhalisia au ya kisaikolojia. Lyimo (2014) akimnukuu Wamitila (2008) anaeleza kuwa hii ni hali inayozunguka utokeaji wa jambo fulani ambayo ndio msingi katika uandishi wa fasihi. Kulingana naye, kuna

mandhari ya kijiografia (mandhari ya kihalisia), kihistoria (mandhari yanayohusiana na masuala ya kihistoria), kidhanifu au kinjozi (mandhari yanayokiuka uhalisia), kidokezi (mandhari yanayoishia kudokeza), kiishara (mandhari yanayotokana na ishara) na kiajinabi (mandhari yanayoishia na sifa za kawaida). Anazidi kueleza mandhari kama zile elementi ambazo hutueleza mahala ambapo matukio fulani yalitendeka. Mandhari kulingana naye, huathiri mno mfululizo wa mawazo na huelekeza jinsi dhamira ya kazi hujengwa. Hata hivyo mandhari makuu katika uainishaji wake ni pamoja na yale ya kijiografia na ya kisaikolojia au hata yote. Katika utafiti wetu tumezingatia mandhari aina tatu ambazo ni pamoja na: mandhari ya kihistoria, kijiografia na kivita. Vile vile, ni muhimu kutaja kuwa mandhari huwa na sehemu kubwa katika utunzi wa fasihi ikiwemo usawiri wa wahusika katika kazi ya kifasihi, kubaini dhamira na maudhui muafaka, maleba yanayofaa na kadhalika.

Tumeeleza mandhari kama elementi ambazo hutueleza mahala ambapo matukio fulani yalitendeka. Mandhari kwa kawaida huathiri mno mfululizo wa mawazo na huelekeza jinsi dhamira ya kazi hujengwa. Kwa uelewa wetu mandhari ni mahali halisi au bunilizi mnamotokea matukio na visa vya fasihi husika. Mandhari huchangia pakubwa sana uwezo wa msanii kuafikia lengo lake la kiutunzi kama vile kubuni wahusika, kubuni dhamira, maudhui na kadhalika. Mandhari sharti yaafiki kiwango cha uchumi wa wahusika katika kisa husika.

**2.9 Usimulizi**

Dhana ya usimulizi si ngeni katika jamii zetu za Kiafrika kwani tangu jadi ilikuwa kawaida kwa vijana kutambiwa hadithi na wazee. Hata inafahamika vyema mtindo wa kukaribisha mtambaji wa hadithi ambapo fanani alianza kwa kauli ya hadithi…hadithi…. nayo hadhira kujibu hadithi njoo...Kisha usimuliaji unaanza moja kwa moja. Hata hivyo wasomi mbalimbali pia wameweza kutoa maoni yao kuhusu dhana hii kama ifuatavyo:

Kwa maoni ya Mohochi (2000) usimulizi una nafasi kubwa katika kazi za kifasihi hata kama mtindo wa usimuliaji umebadilika tangu uvumbuzi wa maandishi kuchipuka. Anasisitiza kuwa ingawa siku hizi fasihi hazisimuliwi ilivyokuwa tangu jadi, kunayo ile sauti ya msimuliaji ambayo kila wakati husikika akilini mwetu wakati tunasoma kazi mbalimbali za masimulizi. Ni dhahiri shahiri kwamba bado usimulizi upo. Kulingana na Mohochi (khj) akimnukuu Attenbernd na Lewis (1963) anaeleza usimulizi kama mkabala unaotuwezesha kuyaona yatendekayo na kupambanua yasemwayo katika kazi za kifasihi. Katika makala yake ameweza kutufafanulia aina mbalimbali

za usimulizi na umuhimu wake katika fasihi kama tunavyoyaelezea hapo chini. Msanii ana mbinu nyingi kadri atakavyopenda kuzitumia katika usimulizi wake wowote ule. Ni muhimu pia kutambua kuwa mbinu hizi pia hutofautiana kwa njia tofauti za kuzua athari kwa wasomaji. Hivyo basi, msanii yeyote analazimika kuteua mbinu za usimulizi ambazo bila shaka zitakidhi mahitaji yake ya kiusanii.

### 2.9.1 Usimulizi maizi

Kulingana na Mohochi (khj) usimulizi huu ndio mkongwe zaidi. Akimnukuu Hawthorn (1985) anafananisha mbinu hiyo na sifa mojawapo ya Mungu kwa sababu msimulizi katika kisa chenyewe anaonekana kama anayeelewa kila kitu kinachoendelea katika hadithi tangu mwanzo hadi mwisho. Msimulizi katika hadithi hii husimulia kisa ambacho hakimhusu yeye na hivyo hashiriki. Katika usimulizi huu msimulizi huwa na uhuru mwingi ambapo hata anaweza kutoa maoni yake ndani ya kisa akilenga kutoruhusu wasomaji kujiamulia wenyewe kuhusu matendo ya wahusika katika kisa chenyewe.

### 2.9.2 Usimulizi wa nafsi ya tatu

Katika usimulizi huu msimulizi hutumia viwakilishi vya nafsi ya tatu a/wa kuelezea yanayotokea katika kisa. Akimnukuu Mohammed (1995), Mohochi (khj) anasisitiza kuwa aina hii ya usimulizi humpa fursa mhusika mmoja kusimulia hadithi badala ya msimulizi binafsi. Hapa kumedhihirika wazi kuwa wakati mwingine mbinu zaidi ya moja za masimulizi huweza kutumika katika masimulizi ya kisa kimoja. Inamaanisha kuwa katika usimulizi wa aina hii usimulizi wa kwanza huenda sambamba na huu wa tatu.

### 2.9.3 Usimulizi wa nafsi ya kwanza

Katika mbinu hii ya usimulizi, msimulizi humwachia jukumu lote mhusika mmoja katika kisa chake kufanya masimulizi yote. Ni mbinu ambayo haijatamba sana katika kazi za kisanii za Kiswahili. Katika usimulizi huu, itambidi msimulizi kuchunga mipaka yake ili asije akapotoka na kuanza kuelezea yale ambayo hayamhusu katika kisa chenyewe. Wakati mwingi kiwakilishi cha nafsi ya kwanza “ni” hutumika. Mara nyingi wasanii hutumia mbinu hii kuelekeza wasomaji wa kazi zake kuelewa mwonoulimwengu wake kupitia kwa mhusika yule wake mkuu ambaye amempa fursa kusimulia kisa chake.

## 2.10 Hitimisho

Katika sura hii, tumefafanua kwa kifupi dhana mbalimbali ambazo zimekuwa muhimu katika utafiti wetu. Vile vile, tumetoa mifano pamoja na kuifafanua inavyofaa. Katika sura inayofuata tunashughulikia kipengele cha wahusika na uhusika wao pamoja na kipengele cha muundo na tumebaini namna vimetumika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*.

## SURA YA TATU

## WAHUSIKA NA UHUSIKA WAO NA MUUNDO KATIKA UTENZI WA UHUD.

### 3.0 Utangulizi

Tumejadili kipengele cha wahusika na uhusika wao katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*.Wahusika ni viumbe anavyotumia msanii kupitisha ujumbe wake kwa wasomaji wake. Viumbe hivi vinaweza kuwa binadamu, wanyama, vitu na hata vifaa.  Wahusika hawa mara nyingi huwakilisha maisha halisi katika jamii anamoishi msanii fulani huku msanii akiwa na lengo la kuirudi au kuionya jamii kuhusu madhila yanayotendeka katika jamii. Katika hali hii, tunajua kuwa kuna aina nyingi za fasihi ambazo lengo si tu kuonya jamii bali kuburudisha, kusifia matendo mazuri na kumulika masuala mbalimbali yanayoikumba jamii. Ili hayo yatimike, ni sharti msanii atambue atahitaji wahusika wapi ili kufanikisha malengo yake ya kiutunzi.

Katika sura hii, tumejadili dhana ya wahusika na aina mbalimbali za wahusika katika utenzi huu. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* tumeainisha wahusika katika makundi mawili makuu ambapo kuna wale wa kimakundi na wale wa kibinafsi. Makundi hayo ni kama vile: kundi la jeshi la Makureshi, kundi la jeshi la Mtume Muhammad, Masahaba wa Mtume Muhammad, wanawake wa Kiislamu, na wanawake wa Makureshi. Pili, kuna kikundi cha wahusika binafsi katika utenzi huu ambao ni pamoja na Mungu Muumba, Mtume Muhammad, Munsabu Omar, Ubayyi bin Khalafu, Utuba na Abdillahi bin Shihabi, Abu Sufyan, Hinda Binti Ustadh na kadhalika. Zaidi ya hapo, katika utafiti wetu, wahusika hawa binafsi tumewagawanya katika makundi kama vile: wahusika wakuu, wahusika duara, wahusika bapa sugu, wahusika wasaidizi na wahusika wadogo. Vile vile katika sura hii tumehakiki kipengele cha muundo kama kinavyojitokeza katika utenzi huu. Katika kuangazia muundo tumeangazia mpangilio wa beti, idadi ya mistari, idadi ya beti, na bahari ya ushairi huu na muwala vinavyojitokeza katika utenzi wetu.

### 3.1.0 Wahusika binafsi

Hawa ni wale wahusika ambao katika utafiti wetu tumewarejelea kwa kutathimini vile ambavyo mtunzi wa utenzi wetu amewasawiri kibinafsi kupitia kwa maelezo yake mwenyewe, vitendo vyao na maelezo ya wahusika wengine kuwahusu. Katika mkondo huu tumetathimini sifa za kibinafsi za mhusika mmoja mmoja kama mtunzi wetu anavyowasawiri katika utenzi huu. Wahusika hao ni pamoja na:

### 3.1.1 Mungu Muumba

Katika utenzi huu, msanii amemchora Mungu kama mhusika bapa sugu. Msimulizi amefanikiwa kwa hili kwani amemchora kuwa aliye zaidi ya binadamu kwa kila jambo. Matendo yake yanazidi ya binadamu ndiyo maana hawezi kufananishwa na kiumbe yeyote. Tujuavyo, Mungu ndiye Muumbaji wa vyote tuonavyo na tusivyoona, ulimwenguni na mbinguni. Msanii huyu amemtumia Mungu kama mhusika bapa sugu kwa lengo la kutusisitizia kuwa Mungu ni Mungu ambaye huwa habadiliki kama binadamu. Kwa hivyo, binadamu sote tuelewe na kukubali kuwa bila Mungu hamna chochote kingeumbwa ulimwenguni. Kulingana na msimulizi wa utenzi huu, Mungu ni mhusika **mtenda haki** siku zote inavyodhihirika katika ubeti wa 7. Pia, katika maelezo ya mtunzi wa utenzi huu katika utangulizi amemwangazia Mungu Muumba kama **mwenye uwezo mkuu** kwani ndiye pekee anayewapa wanadamu nguvu. Kwa mfano: Mungu ndiye alimpa msanii nguvu ya kutunga utenzi huu inavyodhihirika katika ubeti wa 5. Vile vile, amemsawiri Mungu kuwa **mkuu wa yote**, aliyekuwepo tangu mwanzo na atazidi kuwepo hadi mwisho wa ulimwengu inavyodhihirika katika ubeti wa 3. Pia, amemsawiri Mungu Muumba kama **asiyefananishwa** na kiumbe chochote kwani yeye ndiye tu kwa tabia yake **ya huruma** hamna anayefanana naye thibitisho likiwa katika ubeti wa 4. Msimulizi wa utenzi wetu amemwelezea Mungu Muumba kuwa **mwenye kujitosheleza** na aliye mbali ukilinganisha na binadamu inavyodhihirika katika ubeti wa 5. Vile vile, msanii amemchora Mungu kama **mtenda haki** kinyume na viumbe vyake vyote inavyodhihirika katika ubeti wa 7. Katika beti za 8 na 9 msimulizi amemsawiri Mungu kuwa **mwenye kujibu maombi** dhihirisho kwamba kila binadamu aendaye kwake kwa imani hupata anachohitaji kulingana na Mungu mwenyewe anavyotaka. **Ukamilifu wake Mungu** ni wazi katika ubeti wa 13 ambapo msanii anaeleza kuwa hamna mungu yeyote kuliko yeye ndiyo maana ukuu wote ni wake pamoja na mamlaka juu ya yote. Kwa sababu hii, sisi kama binadamu twapaswa kwenda kwake kila wakati ili kupata mahitaji yetu yote kwani yeye ndiye tu anayeweza kutukamilishia yote. Mtunzi wa utenzi huu anakiri kuwa Mungu ndiye wa kuabudiwa na inalazimu kila binadamu kumwendea kwa maombi na unyenyekevu. Katika ubeti wa 15 msanii anakiri kuwa **huruma zake ni za milele**. Sifa ambayo kwa binadamu hukosekana dhihirisho tosha kuwa binadamu ni dhaifu sana akilinganishwa na Mungu. Sifa hizo mtunzi anazommiminia Mungu Muumba ni dhihirisho tosha kuwa hawezi kufananishwa na binadamu kwa lolote. Kwa sababu hiyo binadamu hulazimika kuwa chini yake milele kwa sababu kudura zake ndizo kila binadamu hutegemea.

Vile vile, katika ubeti wa 15 Mungu amesawiriwa kuwa **mwenye rehema** kwa vile huwajaalia binadamu wote neema siku zote bila ubaguzi. Hili hutusisitizia kumwomba na kumtanguliza kwa kila tunalotenda ili atujaalie neema zake. Sifa hizo alizonazo Mungu ni dhihirisho tosha kuwa mtunzi amemtumia kama mhusika bapa sugu kwani yeye habadiliki wala sifa zake hazifananishwi na za binadamu.

### 3.1.2 Mtume Muhammad.

Katika utenzi huu Mtume Muhammad ametumika kama mhusika mkuu. Ni mhusika mkuu kwa vile ameonekana kuanzia mwanzo wa utenzi wetu hadi mwisho. Pili, amehusika katika usimulizi wa utenzi huu tangu mwanzo hadi mwisho. Vile vile, ni mhusika mkuu kwa sababu wahusika wasaidizi wote wametumiwa kumjenga ili kufanikisha dhamira na maudhui katika utenzi huu. Katika utangulizi, mtunzi wa utenzi huu amemmiminia sifa kochokocho kwa kumwita majina ya sifa si haba kama vile: 'kipamba' kumaanisha kuwa alikuwa na sura ya kuvutia inavyojitokeza katika ubeti wa 19. Vile vile, amemwita 'saburi' kuonyesha sifa yake ya **uvumilivu** inavyodhihirika katika ubeti wa 20**.**

Vile vile, msanii amemsawiri Mtume Muhammad kama mhusika **amwaminiye Mungu,** yaani ni Mtume wa Mungu na ndiye bora zaidi katika uumbaji wote. Imani yake inadhihirika pale ambapo anakubali kutumika na Mungu Muumba kupeleka ukweli kwa wanadamu wengine. Kulingana na msanii wa utenzi huu, hakuna kiumbe ambaye ana nafasi kubwa mbele ya Mungu kama Mtume Muhammad inavyodhihirika katika beti za 19-22. Sifa hizi zinadhihirisha thamani ya Mtume Muhammad mbele za Mungu pamoja na ulimwengu mzima. Amethaminiwa na Muumba ndiyo maana akamfanya Mtume wake ambaye humwakilisha ulimwenguni. Katika ubeti wa 188 na 189 Mtume Muhammad amesawiriwa kuwa **mwenye subira,** sifa ambayo imedhihirika pale ambapo alipowajua mashujaa wa uwongo mia tatu waliojipendekeza kwake kwa muda mrefu hakuwakaripia hadi siku ile walipong'atuka kutoka kikundi chake wakiwa katika maombi ya alfajiri ya tarehe ya vita vya Uhud. Pili, alisubiri siku ya kumwua adui yake Ubayyi bin Khalafu hadi alipojileta mwenyewe mbele yake. Kitendo cha kumwangamiza Ubayyi bin Khalafu vile vile kinadhihirisha **ushujaa** wake vitani. Mtume Muhammad amesawiriwa kama **mtiifu** kwa Mungu madai ambayo ni wazi katika ubeti wa 23, mtunzi anaposema kwamba Mtume Muhammad hawezi kutenda kinyume na sheria ya Mungu wala kufanya kitendo chochote kisichofaa.

Mtume Muhammad pia amechorwa na msanii wa utenzi huu kama mhusika **mwenye hekima na tabasuri**. Kwa kweli, jinsi alivyopanga jeshi lake na kuwapa mawaidha siku ile ya vita ni dhihirisho kuwa ana hekima. Aliteua wanajeshi hamsini kuwa walinzi wa njia za milimani, akateua kiongozi wao vile vile akawapa wanajeshi waliobaki majukumu mengine katika pambano hili inavyodhihirika katika ubeti wa 24. Msanii pia amemsawiri Mtume Muhammad kama mhusika **mwenye ulimi mwepesi** katika utoaji nasaha kauli inayodhihirika katika ubeti wa 24. Mtume Muhammad amesawiriwa pia kama mhusika mwenye **kutimiza ahadi zake**; sifa hii imedhihirika baada ya vitisho vya shujaa wa Makureshi Ubayyi bin Khalafu kuwa angemwua Mtume Muhammad. Hali hii ndiyo iliyomlazimu Rasuli kuweka ahadi kuwa angemuangamiza Ubayyi bin Khalafu. Ahadi hiyo ilitimia pale ambapo alimwua kwa kumsukumia kijambia kilichomkata kwenye shingo yake inavyodhihirika kwenye beti za 479 na 499.

Katika utenzi huu, msanii amemdhihirisha Mtume Muhammad kama kiongozi **wa mfano mwema** inavyojitokeza katika ubeti wa 25 ambapo msanii ametumia jazanda kufafanua nafasi yake katika jamii ambapo ametumia ishara ya taji kuleta maana ya uongozi wa Mtume Muhammad, ishara ya mwangaza kuashiria uongozi wake wakati wa mema au mazuri, ishara ya mwezi kuashiria uongozi wa Mtume Muhammad wakati wa shida au matatizo. Ishara hizo bila shaka zinaashiria kuwa Mtume Muhammad ni kiongozi mwema wakati wote. Vile vile, katika beti 188 na 189 tunapata kuelewa kuwa kuhama kwa wale wanajeshi wake mia tatu wakati walikuwa katika maombi ya alfajiri haikuwa siri kwa Mtume Muhammad lakini alijua na kuamua kuiweka moyoni siri hiyo.

Msanii amemchora Mtume Muhammad kama **mwenye uhusiano mzuri na jeshi lake** kwani alipopata siri kwamba mahasidi wake hawakuwa mbali, aliwaelezea masahaba wake aliowaamini kwa ujasiri wao inavyodhihirika wazi katika ubeti wa 149. Katika beti za 150 na 151 mtunzi amemsawiri Mtume Muhammad kama **asiyepoteza muda wake** hivi kwamba alipopata habari ya kwamba maadui wake walikuwa njiani, hakupoteza wakati bali alianza mara moja kuandaa jeshi lake na kuweka mikakati ikiwa ni pamoja na kuwateua wanajeshi wale hamsini wa kuchunga njia za milimani pamoja na mbeba bendera ya jeshi lake. Mtume Muhammad pia amesawiriwa kama **mwenye hekima** kwani ingawa alitambua mipango ya mahasidi wake mia tatu waliomtoroka aliamua kujifanya asiyeelewa hadi pale walipodhani hakutambua kilichoendelea kwenye jeshi lake ithibati ikiwa ni baina ya beti za 189-192.

Katika ubeti wa 198 msimulizi amemsawiri Mtume Muhammad kuwa mhusika **mwenye mpangilio thabiti** hivi kwamba aliwachagua wanajeshi hamsini na kuwapa jukumu la kulinda njia za milimani. Wanajeshi aliowapanga hapa walikuwa jasiri kupindukia. Lengo kuu la kuwapanga hapa ni kuhakikisha maadui hawawezi kupenya hadi upande wa jeshi lao kuwashambulia. Mtume Muhammad pia amechorwa kama mhusika ambaye ni **imara katika kutoa maagizo** kwa jeshi lake. Baina ya beti za 207-211 inadhihirika anavyowaamuru walinda njia za milimani kutoacha wajibu wao katu liwalo na liwe hadi pale atakapotuma mjumbe kuwaamuru kivingine. Mtume Muhammad amesawiriwa kuwa **mwenye ujasiri** dhihirisho ni pale ambapo adui yake mkuu Ubayyi bin Khalafu alimjia kwa vitisho vya kumwangamiza mbele ya masahaba wake. Mtume Muhammad kwa upole akawaomba masahaba wake kujitenga naye ndipo atekeleze ahadi aliyompa adui yake wa jadi. Ahadi ilikuwa kwamba angemwua akiwa juu ya farasi wake. Masahaba wake wakampa kijambia na kujitenga naye kisha Mtume Muhammad akamsukumia kijambia chenyewe shingoni na kumpa jeraha lisilojua kupona. Mtume Muhammad hakumwogopa adui yake eti kavaa nguo za kivita ambazo zilitengenezwa kwa vyuma bali alimkabili **kwa ujasiri.** Imedhihirika wazi kuwa Mtume Muhammad **ndiye amiri mkuu** wa jeshi la Waislamu kulingana na beti za 154-156. Ametambuliwa pia kuwa **shujaa** akiwa vitani kama mashujaa wengine.

Mtume Muhammad ameelezewa kuwa ni **mwenye kusamehe** kwani baada ya vita vya Uhud, aliwasamehe maadui zake ambao walimshambulia kwa mawe na kumjeruhi. Vile vile, **aliwasamehe** wale maadui waliomwua ami yake na kumkatakata vibaya hali iliyomfanya Mtume Muhammad kutaka kulipiza kisasi kama inavyodhihirika katika beti za 551-555 na 557-559. Mtume Muhammad pia amechorwa kuwa **mwenye ujasiri kupindukia** kwani hata ingawa alikuwa na jeshi dogo kuliko la Makureshi alikubali kwenda vitani na maelfu ya jeshi hilo. Pili, vitisho alivyotishiwa na Ubayyi bin Khalafu eti angemwua, hakuviogopa katu badala yake aliwatuliza masahaba wake na kuwaomba kijambia ambacho alimchoma shingoni na kumpa jeraha la mauti inavyoshuhudiwa katika ubeti wa 429. Mtume Muhammad pia amesawiriwa kama mwenye tamaduni kwani ana jinsi ya kuvaa nyakati tofauti tofauti ilivyo wazi katika beti za 432-434 ambapo msanii anaeleza kuwa Mtume Muhammad alivaa vazi lake maridadi la kitamaduni na kujipamba namna ambavyo huwa hajiviki ila wakati wa kivita. Baada ya kukamilisha mavazi yake kwa kuvaa nguo nzito akawaomba masahaba wake kuondoka na kumwacha peke yake. Maagizo hayo ni dhahiri shahiri kuwa Mtume Muhammad alilenga kuwadhihirishia masahaba wake kuwa Mungu hahitaji msaada kutoka kwa binadamu aliye kiumbe chake.

### 3.1.3 Munsabu bin Omari

Mhusika huyu ni sahaba wa Mtume Muhammad wa karibu. Yeye ndiye aliyeshabihiana kwa sura na Rasuli hadi alipouawa Makureshi wakadhani walikuwa wamemwua Rasuli. Omari ndiye alibeba bendera ya jeshi la Mtume Muhammad. Pia, ndiye alipewa jukumu la kuelekeza kundi jingine la wapiganaji mbali na lile la wanajeshi hamsini waliowajibishwa kuchunga njia za milimani. Alipouawa, Makureshi walishangilia wakidhani walikuwa wamemuua Mtume Muhammad inavyodhihirika katika beti za 338-342. Katika utenzi huu, mhusika huyu ametumika kama mhusika mdogo kwani kwa matendo yake amechangia ukuzaji wa maudhui ya kivita. Msanii wa utenzi huu amemsawiri kuwa **mhusika jasiri na mwenye bidii** inavyodhihirika katika ubeti wa 338. Kufia vitani kwake ni ithibati tosha kuwa alikuwa mtu jasiri na aliyekuwa na bidii vitani. Tulivyotangulia kusema, mhusika huyu ametumiwa na msanii kujenga maudhui ya kivita katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*.

### 3.1.4 Bwana Khalid mwana wa Walid

Mhusika huyu alikuwa ni shujaa wa Makureshi. Vile vile ametumika kama mhusika mdogo kwa kuchangia ukuzaji wa maudhui na mandhari ya kivita. Katika utenzi huu amechorwa kuwa mtu **hodari na jasiri kupindukia** ambaye alitambulika kote kote kama shujaa imara. Ithibati tosha ni katika ubeti ufuatao:

Ali shujaa shadidi,
Jinale Bwana Khalid,
Ndie mwana wa Walid,
Ndo mkubwa wa awali.

(ub. 127)

### 3.1.5 Ukirima bin Abii Jahl

Huyu ni shujaa wa Makureshi. Katika utenzi huu, msanii amemtumia mhusika huyu kama mhusika mdogo kwa sababu anachangia katika kukuza mandhari na maudhui ya kivita. Dhihirisho ni katika beti za 305-311 ambapo msanii anaeleza kuwa alikuwa jemedari ambaye aliongoza jeshi la Makureshi kushambulia Waislamu baada ya kugundua kuwa walinda njia za milimani wa Kiislamu walikuwa wametoweka. Msanii amemsawiri kama **mwenye ujasiri** kwa vile alikuwa jemedari aliyeongoza jeshi la Makureshi vitani inavyodhihirika katika beti za 305-316.

### 3.1.6 Amir Ibn Alyas

Huyu ni shujaa wa Makureshi. Vile vile, ametumika kama mhusika mdogo anayechangia katika ukuzaji wa mandhari na maudhui ya kivita katika utenzi huu. Msanii anamtambua kama jemedari wa pili baada ya Ukirima bin Abii Jahl ambaye walishirikiana katika vita vya Badri. Msanii amemsawiri kama mhusika **mwenye ujasiri** kwa vile mtunzi anaeleza kuwa mhusika huyu alikuwa **mwenye ujasiri na hasira pia**. Amesawiriwa vile vile kama **asiye na huruma** kwani alikuwa mtu asiyeweza kuonea adui huruma hata kidogo maoni yanayothibitishwa katika ubeti ufuatao:

Akisimama mtesi
wala nae si mwepesi
Amiri bin Alyasi
ndie mkubwa wa pili.
(ub. 128).

### 3.1.7 Sufian Ibn Banu Umayya

Huyu ni shujaa wa Makureshi. Katika utenzi huu ametumika kama mhusika duara kwa sababu hata baada ya kuamua kujiunga na kikundi cha Mtume Muhammad, baadaye anaghairi na kusaliti uamuzi huo na kushirikiana na Makureshi. Msanii amemchora kama mhusika mmojawapo wa wale waliokuwa na **pingamizi** kwa lolote lililowaathiri katika hisia zao. Yeye na wenzake walikuwa **maarufu** mbele ya Mtume Muhammad hadi akawateua kama maamiri katika jeshi lake ijapokuwa baadaye walimgeuka. Vile vile, mtunzi amemsawiri kuwa **kigeugeu na mwongo** kwani baada ya kujipendekeza kwa Mtume Muhammad kuwa mfuasi wake, mwishowe yeye na wenzake walimtoroka na kujiunga na jeshi pinzani kwa sababu njama yao ilikuwa kumpiga vita na kummaliza Rasuli.

### 3.1.8 Hindu Binti Ustadh

Huyu ni bibiye Abu Sufiani ambaye alikuwa shujaa wa Makureshi. Msanii amemtumia kama mhusika mdogo kwani anachangia katika ukuzaji wa mandhari ya kivita pamoja na maudhui ya vita. Mhusika huyu amesawiriwa kama mmojawapo wa wale wanawake **jasiri** kwani alimfuata mumewe kwenda vitani pamoja na kundi jingine la wanawake wa Makureshi kwa lengo la kumchochea na kumpa moyo katika vita. Amesawiriwa pia kama **mwimbaji hodari**. Aliimba

wimbo kwa maringo baada ya vita vya Uhud. Kuimba kwake kwa majitapo ni dhahiri shahiri kuwa ni mweye maringo na madaha inavyothibitishwa katika beti za 684 na 686.

Kema huyo mwanamke
Hindi ndiye jina yake
akaimba nyimbo zake
ali juu ya jabali
(ub. 684).

Baada hapo kuimba
mwanamke kujigamba
na mumewe akawamba
Abu Sufyani kakuli.
(ub. 686)

Vile vile mwanamke huyu amechorwa kuwa **mshairi hodari** kwani alighani mashairi baada ya vita vya Uhud akiwa na mumewe inavyodhihirika katika ubeti wa 685. Hinda pia ni **mwenye kiburi** dhihirisho likiwa majigambo yake katika nyimbo na mashairi kuhusu ushindi wa mumewe kwani ndiye alikuwa amiri mkuu wa jeshi la Makureshi inavyojitokeza katika ubeti wa 686. Aliimba nyimbo na mashairi ya pongezi kwa ushindi wa Makureshi katika pambano la Uhud. Mhusika huyu bila shaka hukuza mandhari na maudhui ya kivita katika utenzi huu.

### 3.1.9 Abdillahi bin Shihabi Kabihi

Mhusika huyu ni shujaa wa Makureshi ambaye msanii amemtumia kama mhusika mdogo katika utenzi huu kwa sababu amechangia maudhui na mandhari ya kivita. Kulingana na mtunzi wa utenzi huu, mhusika huyu amechangia sana kumjeruhi Mtume Muhammad kwa mawe baada ya Utuba Al Ukasi kufungua mkondo. Msanii huyu amemtambua kama **adui kweli wa Mungu**. Ametambuliwa kuwa adui wa Mungu kwa vile alikuwa akimpinga Mtume Muhammad. Uadui huu unaonekana wazi katika beti za 536-538 ambapo msanii anaelezea wazi namna alimrushia Mtume Muhammad mawe vitani kwa fujo bila kukoma. Hivyo basi akahesabiwa mmojawapo wa maadui wa Mungu. Mhusika huyu amechorwa kama **asiyekata tamaa** kwa vile yeye pamoja na wenzake hata baada ya kukimbizwa mbali na jeshi la Mtume Muhammad, bado walirejea kutazama hali ilivyokuwa na walipoona mwanya ulioachwa na jeshi la Rasuli katika njia za milimani,

waliwashambulia Waislamu vikali na kuwaua na kujeruhi watu wengi katika jeshi la Mtume Muhammad. Msanii amemsawiri kuwa **mwenye chuki kwa Mtume Muhammad** dhihirisho ni kwamba alimvurumishia Mtume Muhammad mawe hadi moja likamwangukia katika utosi wake na kumpasua inavyoelezwa katika ubeti wa 539.

### 3.1.10 Abdalla bin Ubayya bin Sululi

Msanii amemtumia mhusika huyu kama mhusika mdogo kwani amechangia ukuzaji wa maudhui na mandhari ya kivita katika utenzi wetu. Mhusika huyu alikuwa ndiye kiongozi wa kundi lile la wanajeshi mia tatu waliomtoroka Mtume Muhammad wakiwa katika maombi ya alfajiri ya siku ya vita inavyodhihirika katika beti za 180-187. Msanii amemsawiri kuwa mhusika kigeugeu asiye na msimamo. Dhihirisho likiwa kule kujifanya kwake eti anashirikiana na Mtume Muhammad kumbe alificha uovu wake na baadaye akamtoroka alfajiri ile ya siku ya vita. Katika nukuu ifuatayo, msanii anaelezea namna wanajeshi wale mia tatu walimtoroka Mtume Muhammad angali akiomba:

Sala haijatimia
kiamu na rukuia
wala kukaa tahiya
sijida na itidali.
(ub. 176)

Vile vile, mhusika huyu amesawiriwa kuwa mtu **mwongo na msaliti,** kulingana na msimulizi, hana dini rohoni kwani yeye ni Isilamu laghai maelezo ambayo ni wazi katika beti za 185 na 186. Alijionyesha mbele ya Mtume Muhammad kama mtu mzuri ila ni laghai rohoni mwake kwani alimsaliti Rasuli kwa kumtoroka wakati wa maombi ya kujiandaa kwa vita. Dondoo ifuatayo inatudhihirishia tabia hiyo ya usaliti wake kwa Mtume Muhammad.

Alikuwa maalumu
mbele yake Muungamu
kuonesha Uislamu
na kwamba mwenye fiili.
(ub. 187)

Msanii pia, amemsawiri kuwa **kiongozi potovu** kwani aliongoza wanajeshi mia tatu kumsaliti Mtume Muhammad inavyojitokeza wazi katika beti za 184 na 185. Vile vile, msanii huyu amemsawiri kuwa **mwenye kujipendekeza** kwani awali alijionyesha mbele ya Mtume Muhammad kuwa mtu wa kuaminika ilhali alikuwa hasidi rohoni inavyojitokeza katika beti za 186 na 187 ambapo kuna dhihirisho la kujifanya Muislamu wa kweli kumbe alikuwa mwenye imani ya uwongo.

### 3.1.11. Abu Sufiani

Huyu alikuwa shujaa na jemedari mkuu wa jeshi la Makureshi. Msanii amemtumia kama mhusika mdogo kwani amechangia katika ukuzaji wa maudhui ya kivita. Katika utenzi wetu, msimulizi amempa sifa ya **mwenye vitisho** kwa vile alisikika akisema angependa vita vingine viandaliwe mwaka ambao ungefuata. Alisema hivyo kwa sababu ilikuwa dhahiri shahiri kwake kuwa alikuwa ameshinda vita hivyo. Vile vile, amesawiriwa kuwa **mwenye kiburi** kwani katika beti za 673-680 msanii amedhihirisha maringo yake pale anapofurahia namna majeshi yake yalivyowaangamiza wanajeshi wa Mtume Muhammad katika vita hivyo na kuwapongeza wanajeshi wake. Anadhihirisha **ukatili wake** katika ubeti wa 675 anapofurahia mauaji ya kiholela waliyofanyiwa Waislamu. Vile vile, katika ubeti wa 687 msimulizi anamtambua kama **mwenye mamlaka** dhihirisho ni kwamba, yeye ndiye aliyaamuru majeshi ya Makureshi kurejea Maka na vita kumalizika. Dhihirisho tosha kuwa ndiye alikuwa amiri mkuu wao.

### 3.1.12 Ubayyi bin Khalafu

Huyu ni shujaa wa Makureshi ambaye kulingana na msimulizi ni hodari sana vitani. Msanii amemtumia kama mhusika mdogo na mjenzi. Kama mhusika mdogo amechangia katika kukuza maudhui na mandhari ya kivita. Vile vile kama mhusika mjenzi, msanii amemtumia kumkuza Mtume Muhammad haswa sifa yake ya ushujaa. Katika beti za 416 na 417 shujaa huyu ametajwa kuwa **adui mkuu** wa Mtume Muhammad. Katika utenzi huu msanii amemsawiri mhusika huyu kama mtu **mkali** kwani katika nukuu ifuatayo inadhihirika kwamba alibeba upanga wake mkononi kwani alishindwa kujisetiri kutokana na hasira zake za kutaka kumwua Mtume Muhammad.

Ndipo kafanya ghamizi
kujiweka hajiwezi,
kaja na upanga wazi

ambao wa kweli kweli.

(ub. 418)

**Ujasiri wake** ni wazi pale ambapo amejitolea kabisa akiwa peke yake kwenda kumkabili Mtume Muhammad bila kujali lolote. Inadhihirika wazi kuwa alimdharau Mtume Muhammad rohoni mwake inavyodhihirika katika beti za 423 na 424 ambapo anajiamini kuwa ana uwezo wa kumwangamiza Mtume Muhammad bila kujua angeangamizwa yeye. Vile vile, msimulizi amemsawiri kuwa **mwenye kumbukizi** kwani baada ya kujeruhiwa na Mtume Muhammad, aliweza kukumbuka ahadi Mtume Muhammad aliyoweka dhidi yake. Alikiri binafsi kwamba Mtume Muhammad akitoa ahadi ni sharti aitimize na hivyo akatambua wazi kwamba mauko yake yalikuwa njiani alipofumwa kijambia na Rasuli. Baadaye tunajulishwa na msimulizi kuwa alifariki kabla ya kufika Maka mahali panapoitwa Sarifu. Mtunzi wa utenzi huu amemsawiri mhusika huyu kama **mwenye hasira asiye na subira** inavyodhihirika katika beti za 428 na 461 hakuwahi kukubali ushinde vitani maoni ambayo ni kutoka kwa wapiganaji wenzake aliowaendea kwa kuomba usaidizi baada ya kupata kipigo cha Mtume Muhammad katika beti 463-466. Kulingana na msanii mhusika huyu ni jasiri ambaye akienda vitani hawezi kubanduka kwa kuogopa ilivyo wazi katika beti za 464- 466.

### 3.1.13 Utuba Al Ukasi

Huyu ni shujaa wa Makureshi. Kulingana na mtunzi, shujaa huyu amezaliwa na mama mmoja na Sadi ambaye ni mmoja wa masahaba wa Rasuli. Msanii huyu amemtumia kama mhusika mdogo ambaye amechangia katika ukuzaji wa maudhui na mandhari ya kivita katika utenzi huu. Hili ni wazi kwani msimulizi katika beti za 531-535 anaelezea namna mhusika huyu alijiunga na dini batili na kulenga kumwangamiza Mtume Muhammad. Mhusika huyu ndiye alimpiga Mtume Muhammad jiwe katika mdomo wake wa chini kwa lengo la kumwua. Juhudi zake za kumwangamiza Mtume Muhammad zinajenga mandhari na maudhui ya kivita katika utenzi huu. Mtunzi amemsawiri kuwa mhusika **mwenye imani batili** kwani aliasi imani ya Kiislamu na kutoizingatia kama nduguye Sadi inavyoelezwa na mtunzi katika ubeti wa 530. Vile vile, amedhihirika kuwa mtu **asiye na huruma** kwa kurejelea namna alimsukumia Rasuli jiwe na kumwumiza vibaya sana katika mdomo wake wa chini hadi likavunja baadhi ya meno yake ilivyo dhahiri katika ubeti wa 534. Kutokana na jinsi alivyorusha jiwe lake na kumwumiza kiasi kile, ni dhahiri shahiri kuwa ni mtu **mwenye nguvu kupindukia** ukirejelea ubeti wa 532. Katika ubeti wa

530, msimulizi amemsawiri kuwa **msaliti** kwa misingi kuwa ingawa yeye na Mtume Muhammad walitoka katika ukoo mmoja, anamsaliti wakati anajiunga na kundi linalopingana naye.

### 3.1.14 Abdalla Khuberi

Ni shujaa wa Mtume Muhammad. Vile vile ametumika kama mhusika mdogo kwani amechangia maudhui na mandhari ya kivita kwenye utenzi huu. Huyu ndiye aliongoza kikosi cha Rasuli cha wale wanajeshi hamsini ambao walipaswa kuchunga adui wasipitie kwenye njia za milimani kuwashambulia Waislamu inavyodhihirika baina ya beti za 200-206. Amesawiriwa kuwa **mwenye ujasiri** wakati wa kivita. Dhihirisho linatokana na kule kutokataa kwake jukumu la kuongoza jeshi lake hata kama idadi yao ilikuwa ndogo ukilinganisha na idadi ya Makureshi. Katika beti za 296-299 inadhihirika wazi kuwa mhusika huyu ni **mwenye utiifu.** Kulingana na msimulizi wa utenzi huu, yeye pamoja na wenzake kumi na wawili waliamua kuzingatia amri ya Rasuli ya kutotoka kwenye njia za milimani hadi pale wangepata ujumbe kutoka kwa Rasuli. Msanii anaeleza kwamba hata alipojaribu kuwarai wenzake thelathini na nane walikataa katakata kutilia maanani mwongozo wake. Bila shaka maelezo hayo yote yanakuza mandhari na maudhui ya kivita katika utenzi huu.

### 3.1.15 Seyyida Fatima

Mhusika huyu ni bintiye Mtume Muhammad aliyeandamana na wanawake marafiki zake kwenda kumtazama baba yake baada ya kupata uvumi mbaya kuhusu hali yake kuwa alikuwa ameaga dunia akiwa vitani ilivyo wazi katika ubeti wa 642. Msanii wa utenzi huu amemtumia kama mhusika mdogo kwani amechangia ukuzaji wa mandhari ya kijiografia kutokana na pangoni alimomtembelea Mtume Muhammad.

Mtunzi wa utenzi huu amemsawiri kama **mwenye hekima** kwani baada ya kutazama hali ya majeraha ya babaye, alibaini njia rahisi ya kumtibu kutokana na majeraha aliyokuwa nayo. Kwa hivyo alikata vipande vya nguo za baba yake na kuvichoma na kupata jivu alilompaka baba yake kwenye majeraha yake anavyosimulia msanii katika beti za 642-645. Kitendo chenyewe ni dhihiriho tosha la mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo kwa baba yake mpendwa. Vile vile, amesawiriwa kuwa **mwerevu** kwa jinsi ya kumpaka majivu hayo katika majeraha yake bila kumwongezea uchungu zaidi.

### 3.1.16 Abu Ubeid

Abu Ubeid ni shujaa wa Mtume Muhammad ambaye tunaambiwa katika utenzi huu kuwa alimpenda Rasuli kwa penzi la ajabu. Mhusika huyu ndiye alikuwa kiongozi wa masahaba wa Mtume Muhammad. Msanii pia anatuelezea kuwa ndiye aliyemng'oa Mtume Muhammad misumari aliyodungwa mwilini wakati wa vita inavyosimuliwa katika beti za 623-627. Katika utenzi huu, msanii amemtumia kama mhusika mdogo kwa lengo la kuchangia maudhui ya kivita katika utenzi huu. Kutokana na uongozi wake shupavu kwa masahaba wa Mtume Mohammad, mauko hayakumpata Rasuli wakati wa vita. Mtunzi wa utenzi huu amemchora kama **mwenye imani thabiti** kwa Mtume Muhammad kwa sababu alionelea kuwa ni vyema kumng'oa misumari hiyo kutoka mwilini ili angalau Mtume Muhammad apate nafuu haraka.

Msanii huyu pia amemsawiri kama **mwenye huruma** kwa kujitolea kumng'oa Mtume Muhammad misumari kutoka kwenye mwili wake ili kupunguza maumivu yake. Hakupenda kumwona Mtume Muhammad akiumia kwa majeraha hayo. Vile vile, amesawiriwa kama mtu **jasiri** kwani kibarua cha kung'oa rafiki misumari kutoka mwilini bila shaka huhitaji mtu jasiri kwa sababu aumiaye hutoa kilio cha ajbu hali ambayo mtu asiye jasiri hawezi akastahimili asilani. Katika utenzi huu msanii huyu pia amemchora kama mhusika **mwenye upendo** inavyodhihiri katika ubeti wa 623 ambapo tunagundua kuwa walipendana sana na Mtume Muhammad mbali na kuwa sahaba wake wa karibu.

### 3.1.17 Talha

Talha amesawiriwa kama mmojawapo wa masahaba wa Mtume Muhammad. Katika utenzi huu ametumika kama mhusika mdogo anayechangia maudhui ya kivita na mandhari ya kijiografia. Kule kimficha Mtume Muhammad asiuawe kulifanya Makureshi kutoafikia lengo la kumwangamiza Mtume Muhammad na hivyo ushindi wao katika vita hivyo haukuwa kamili. Chini ya pango lenye jabali alipokuwa amemficha Mtume Muhammad hudhihirisha mandhari ya kijiografia. Msanii amemsawiri kama mhusika **mwenye nguvu**. Dhihirisho hapa ni kutokana na kile kitendo cha kuingia shimoni na kumtoa nje Mtume Muhammad baada ya kupigwa jiwe na mahasimu wake Makureshi inavyodhihirika katika beti za 383-386.

### 3.1.18 Ali

Ali ni mume wa binti ya Mtume Muhammad. Katika historia ya vita hivi, ametambuliwa kuwa kiungo muhimu zaidi akishirikiana na Hamza na Abu Dujana. Baada ya kifo cha Hamza aliendelea

katika vita bila woga. Katika utenzi huu Ali ametumika kama mhusika bapa sugu kwani tabia yake ya ujasiri inadhihirika hadi mwisho wa utenzi huu. Vile vile, anakuza maudhui ya kivita, kidini na mandhari ya kijiografia. Kule kupatikana kwake akiwa na Talha sahaba wa Mtume Muhammad Mtume Muhammad walipokuwa wakimtoa shimoni ni dhihirisho la mchango katika mandhari ya kijiografia. Msanii huyu amemsawiri kuwa **jasiri kupindukia** alitumia ujasiri wake wote kumficha Mtume Muhammad kutokana na kuumizwa au kuuawa na Makureshi. Kwa vile Mtume Muhammad alikuwa Mtume wa kueneza dini na imani ya Kiislamu ndiyo maana tumeeleza kuwa mhusika huyu amekuza maudhui ya kidini katika utenzi huu. Vile vile, amesawiriwa kuwa **mwenye huruma** kwani alikuwa tayari kumsaidia Mtume Muhammad inavyosimuliwa katika beti za 386 na 390. Pia amechorwa kama **mwenye nguvu** kutokana na kitendo chake cha kumshika Mtume Muhammad alipokuwa amejeruhiwa na Makureshi dhihirisho likiwa katika beti za 388 na 389.

### 3.1.19 Bwana Sadi

Msanii amemtumia mhusika huyu kama mhusika mdogo anayechangia maudhui ya vita. Mhusika huyu ni mmojawapo wa masahaba wa Mtume Muhammad. Katika ubeti wa 526 msanii amemtaja kuwa **mwenye ujasiri na nguvu.** Sifa hii imetokana na ukakamavu wake alioonyesha kila wakati akiwa vitani. Vile vile, ametambuliwa kuwa **shujaa kweli kweli** kwa sababu alibaki kuwa imara vitani kila wakati inavyodhihirika katika ubeti wa 526. Sifa yake ya **kuaminika** vile vile imedhihirika kwa sababu ya ujasiri wake. Mtume Muhammad **alimwamini sana** kwani akiwa mbele vitani mambo huenda shwari.

### 3.1.20 Bwana Hamza

Mhusika huyu alikuwa ami ya Mtume Muhammad. Mhusika huyu ametumiwa kama mhusika mdogo katika utenzi wetu. Kifo chake kinatupa picha ya udhalimu wa Makureshi dhidi ya Waislamu. Picha hiyo inakuza maudhui ya kivita katika utenzi wetu. Kifo chake kilimhuzunisha sana Mtume Muhammad hadi akaonyesha nia ya kulipiza kisasi kwa sababu yake. Katika utenzi huu msanii amemsawiri kuwa **mwenye nguvu** kwani alipenda sana kushiriki na kushinda mapambano ya kivita kila wakati inavyodhihirika katika ubeti wa 704. Vile vile, katika utenzi huu ametambulika kuwa **mpiganaji mahiri** kutokana na uzoevu wa kushiriki vita na kuwa stadi wa kutegemewa ilivyo wazi katika ubeti wa 704. Kwenye ubeti wa 705 vile vile, msimulizi amemchora kama **mwandani wa** Mtume Muhammad kwani walipendana na kuenziana sana na

hivyo kila wakati ungewapata pamoja. Msanii pia amemchora kuwa **shujaa wa kupigiwa mfano** kwani kila wakati kila shujaa anayetajwa alifananishwa na yeye kwa sababu alikuwa **stadi wa vita** na hakuna aliyewahi kupigana zaidi yake inavyodhihirika katika ubeti wa 708.

### 3.1.21 Sayyid Umari

Huyu ni mmojawapo ya sahaba wa Mtume Muhammad. Katika utenzi huu ametumiwa kama mhusika mdogo. Ametumika kukuza maudhui na mandhari ya kivita. Katika utenzi huu ametambuliwa kuwa mhusika **mwenye hasira** inavyodhihirika katika ubeti wa 666 ambapo, baada ya Mtume Muhammad kuamuru masahaba wote kutojibu sauti ya Abu Sufiani shujaa wa Makureshi aliyetaka kujua iwapo Mtume Muhammad na masahaba wake walikuwa hai au wamekufa, yeye alishindwa kujizuia na kujibu kwa kauli kwamba hao wote aliowaulizia walikuwa hai na tayari kwa pambano lingine. Kauli hiyo pia ni dhihirisho tosha kuwa alikuwa mhusika **jasiri.**

## 3.2.0 Wahusika wa kimakundi

### 3.2.1 Seyyidati Esha na Seyyidati Batuli

Kina dada hawa walimtembelea Mtume Muhammad kuangalia hali yake kwani minong'ono iliyokuwa imechacha kuwa kafariki iliwatia wasiwasi dhihirisho ni katika beti za 634,636 na 640. Wamesawiriwa kama **wenye ustahimilivu** kutokana na maelezo kuwa walipopata habari kuwa Rasuli kafariki, walikuwa na matumaini hadi walipomtembelea na kupata ukweli kuwa alikuwa hai ndipo mioyoni mwao wakaridhika inavyodokezwa katika ubeti wa 641.

### 3.2.2 Masahaba wa Mtume

Hawa ni wafuasi, walinzi na marafiki wa Mtume Muhammad. Ingawa Makureshi walikula kiapo cha kumwangamiza Mtume Muhammad, masahaba wake walifanya kadri ya uwezo wao kuhakikisha kuwa Mtume Muhammad alikuwa salama salimini. Dhihirisho kwamba ni **wenye bidii** ni katika beti za 517-519 ambazo msanii anaelezea namna shambulizi la Makureshi lilifanywa kwa kishindo kikubwa lakini masahaba hawa wakajizatiti kuhakikisha Mtume Muhammad alibakia kuwa hai. Msanii katika beti hizo anafafanua kuwa pigano la siku hiyo halikuwahi kushuhudiwa awali. Anazidi kusisitiza kuwa ingawa hivyo, jeshi la Mtume Muhammad lilijizatiti namna ambavyo hawajawahi kufanya awali kwa lengo la kumlinda Mtume Muhammad kutokana na mauko.

Kundi hili vile vile, limesawiriwa kama kundi la watu ambao ni **wenye upendo** kwani walijaribu njia zote kuzuia pigo lolote kwa Mtume Muhammad ijapokuwa hali ilikuwa ngumu inavyodhihirika katika beti za 371-380. Kule kula kiapo kwamba wangesema ukweli kwamba Mtume Muhammad alikuwa hajafa ni ishara ya upendo waliokuwa nao kwa Mtume Muhammad. Vile vile, ni ishara ya kuwa ni watu wenye msimamo thabiti. Walikuwa tayari kwa uzuri au kwa ubaya kumtetea Mtume Muhammad asije akaangamizwa na maadui wake.

Msanii huyu pia amewatambua kama watu **jasiri kupindukia** ijapokuwa walikuwa kumi na watano, hawakuogopa jeshi kubwa la Makureshi lililomshambulia Mtume Muhammad kwa mawe mengi kama mvua bali walijizatiti na kumzingira asipatwe na mauko inavyoelezewa katika beti za 406-408. Pia, wamedhihirika wazi kuwa **wenye nidhamu ya hali ya juu** kwa vile, licha ya Ubayyi bin Khalafu kutoa kauli kali za kuazimia kumwua Mtume Muhammad, hawakujibishana naye kwa lolote ila walingoja amri kutoka kwa Mtume Muhammad kama anavyotujuza msanii katika beti za 425-430. Katika ubeti wa 429 **utiifu** wao umedhihirika pale ambapo Mtume Muhammad aliwaomba masahaba wake kijambia nao wakamletea vingi akachague. Mtume Muhammad akachukua kilichokuwa kidogo zaidi na kumwangamizia adui yake Ubayyi bin Khalafu msanii anavyoeleza katika beti za 435-437.

Mtunzi wa utenzi huu amewasawiri wahusika hawa kuwa **wenye kujitoa mhanga** kwani pale ambapo Mtume Muhammad alizidiwa na mahasidi wake na kuweka maisha yake katika hali ya hatari walifanya kila walichoweza kumkinga kutokana na mauaji inavyodhihirika katika beti za 602-605. Walisimama na Mtume Muhammad ima fa ima dhihirisho kuwa walikuwa **wenye bidii ya mchwa** katika kutekeleza majukumu yao. Walionyesha sifa ya **utiifu** kwani kila wakati walitii kauli za Mtume Muhammad inavyoelezwa katika ubeti wa 656. Walimtii Rasuli alipowaambia kuacha kujibu kauli za shujaa wa Makureshi Abu Sufiani alipotaka kujua iwapo Mtume Muhammad alikuwa kafariki au alikuwa bado hai. Ni watu **wenye uaminifu** kwani walitegemea sana maoni ya Mtume Muhammad kila wakati. Wamechorwa kama **wenye heshima** kwa vile waliheshimu mamlaka ya Mtume Muhammad kwa kila jambo.

### 3.2.3 Wanawake Makureshi

Katika utenzi wetu hatujapata wahusika wengi wa kike bali kunao wachache ambao wametambuliwa kwa kijumla nao ni kama vile: wake za maamiri wa kijeshi waliokuwa kumi na watano ambao waliandamana na waume zao kwenda vitani na mwisho kuna mwanamke ambaye

ndiye mwanamke wa pekee ambaye alijitokeza kubeba bendera ya kivita ya Makureshi baada ya kukosa mwanajeshi yeyote kuibeba. Wahusika hawa katika utafiti wetu tumewasawiri kwa sifa za kijumla tu kama vile:

Ni **wenye ujasiri** kwa sababu waliamua kuandamana na waume zao kwenda vitani. Kwenda kwao, kulilenga kuwapa waume zao motisha ya kutia bidii katika pambano hilo. Vile vile tunaweza kuwasawiri kama **wapenzi wa taifa lao** kwa sababu walijitolea kukaa pale vitani kuhakikisha ushindi ungepatikana. Kwa kweli **ni wazalendo kindakindaki** haswa yule mwanamke aliyeamua kutoa maisha yake kwa kuibeba bendera iliyoachwa na wenzake wa kiume.

### 3.2.4 Jeshi la Makureshi

Jeshi hili lilikuwa na wanajeshi elfu tatu, ngamia elfu tatu na farasi elfu tatu inavyojitokeza katika beti za 136-139. Ni makafiri **wenye hasira na chuki** kwa Mtume Muhammad pamoja na dini yake. Lengo lao moja ni kumwangamiza Mtume Muhammad na familia yake kabisa. Kwa mfano katika ubeti wa 141 msanii anatueleza kuwa nia yao ni kumuangamiza Mtume Muhammad kabisa pamoja na masahaba wake. Walinuia kutekeleza hayo kwa sababu hawakuamini ukweli wa Mtume Muhammad.

Kikundi hiki kimeongozwa na mashujaa **jasiri kweli kweli** akiwemo Khalid bin Walid, Amir bin Alyas, Ukirimu bin Abu-Jahl na Sufiani bin Ummaya. Kulingana na msimulizi, baadhi ya wahusika hawa walisilimu na kujiunga na Mtume Muhammad aliyewapa kazi za uongozi katika jeshi lake nao wakazitekeleza kwa ufasaha anavyotuarifu msanii katika beti za 132-135. Kwa hivyo, wale wahusika waliobaki katika jeshi lao wanaonyeshwa kuwa wao ni watu **wenye umoja** kwa lengo la kumuangamiza nabii wa Mungu Mtume Muhammad. Walikusanya mali na zana za kivita kuandaa vita dhidi ya Mtume Muhammad inavyodhihirika katika ubeti wa 60. Wale ambao walighairi msimamo wao wanadhihirisha uduara wao na hivyo **kuwa wasaliti**. Wahusika hawa pia wameelezewa kama **wenye tamaa ya kulipiza kisasi** yote yakiwa ni baada ya kushindwa katika vita vya Badri. Viongozi wa Maka wakatangaza zawadi kwa mtu yeyote ambaye angeleta hata kichwa cha Rasuli bila hata kiwiliwili anavyotuarifu mtunzi wa utenzi katika beti za 61, 62, 63, 64 na 65.

Wahusika hawa pia ni **wenye uchokozi** kwa sababu wao walizidi kumkejeli Mtume Muhammad na kumvunjia heshima kila uchao anavyotujuza msanii katika beti za 66, 67. Vile vile,

wamesawiriwa kama **wapenda ugomvi** kwa misingi kuwa baadhi yao walikwenda Madina kudhihirisha kuwa walitaka kuzua ugomvi inavyoelezewa katika beti za 99-102. Viongozi wa jeshi la Makureshi wamesawiriwa kuwa wahusika **jasiri kupindukia** kwani walishindwa kubakia kwenye taifa lao Maka na kwenda Madina kwa lengo la kumpiga vita Mtume Muhammad inavyosimuliwa katika beti za 117-121. Tendo hili linadhihirisha uzalendo wao kwa nchi yao. Msanii amewachora pia kuwa watu wasio na subira na wenye hasira kupindukia baada ya kufika mahali pa vita kukielekea usiku, walitaka kupigana hata kama usiku ulikuwa umekaribia anavyothibitisha msanii katika beti za 167, 168 na 169.

Kwa mtazamo wa msimulizi, wanajeshi hawa ni **wenye fitina** kwani katika ubeti wa 66, Makureshi hawa walizidi kumtukana Mtume Muhammad baada ya juhudi zao za kumwua kugonga mwamba. Msanii amewatambua pia kuwa watu **wapenda fujo** kwani walidhani kwamba iwapo wangezidi kumvuruga Mtume Muhammad, angeanza vita nao inavyosimuliwa katika beti za 66, 67 na 102. Msanii pia amewasawiri kama watu **wenye ghadabu** kwani baada ya kushindwa katika pigano la Badri, waliweka kisasi mioyoni mwao na kuapa kwamba iliwalazimu kulipiza kisasi. Kwa upande mwingine, msimulizi wa utenzi huu amewachora kama watu **wenye jitihada** kwani hata kama walishindwa Badri, hawakufa moyo bali walijikaza kisabuni ili kutimiza kilichowasumbua katika nyoyo zao inavyodhihirika katika beti za 77-82 ambapo msanii anatusimulia namna ambavyo walianza kutayarisha silaha zao kwa vita vingine. Katika ubeti wa 117 msanii huyu amewachora kama watu **wenye ujasiri kupindukia.** Wakati wa vita vya Uhud, hata viongozi wao wakubwa serikalini hawakutaka kuwachwa nje ya vita hivyo kwa vile kila mmoja alisukumwa na uzalendo na hivyo kuamua kwenda vitani. Baadhi yao haswa wale viongozi majemedari walienda na wake zao vitani.

Wanajeshi hawa wamesawiriwa kama wahusika **weledi** kwani baada ya kupata habari kuwa Waislamu walikuwa wamewacha mipaka ya njia zao za milimani wazi, walifanya kasi na kuwashambulia nyuma yao kwa kishindo wasijue mahali pa kutorokea. Shambulizi hili kwa Waislamu ni dhihirisho tosha kuwa walikuwa **wajuzi** katika vita. Msanii amewasawiri kama **wenye fitina** kwa Mtume Muhammad kwa sababu walipotambua kuwa Mtume Muhammad alikuwa hai, walizidi kuwa na hasira zaidi iliyowatia moyo wa kuzidi kupambana zaidi dhidi ya Mtume Muhammad na masahaba wake inavyosimuliwa katika ubeti za 412.

### 3.2.5 Jeshi la Waislamu

Hawa ni wanajeshi wa Mtume Muhammad ambao idadi yao ni elfu moja. Akitumia jazanda, msimulizi anawatambua kwa jina la kimajazi la "panga kali." Msanii ametumia sifa hiyo kufananisha weledi wao na ukali wao katika vita.

Katika beti za 151 na 154 wanajeshi hawa wamesawiriwa kama **jasiri** kwani kulingana na msanii, hawakuwa na nafasi ya woga rohoni wala kutetereka kwani kwao hizo zilikuwa ni sifa ambazo hawakuzitambua maishani mwao. Walikuwa imara na thabiti vitani. Pili, wanajeshi wale hamsini waliopangwa kuchunga njia za milimani waliteuliwa katika nafasi hizo kwa minajili ya **ujasiri wao.** Kulingana na mtunzi wa utenzi huu amewatambua kuwa wanajeshi ambao **walijitolea vitani** bila kukaribisha hitilafu yoyote. Kwa kweli ni watu **wenye msimamo thabiti.** Kwenye ubeti wa 153 msanii wa utenzi huu anawatambua kama **wazalendo kindakindaki** kwani waliacha nyumba zao kwenda vitani na wakiwa vitani hupigana kwa nguvu na ujuzi wao wote. Walikuwa wanajeshi ambao ni **wenye jina zuri** kwani hata kwenye makazi yao waliheshimika wala hawakuwa na dosari hata kidogo anavyotusimulia msanii katika ubeti wa 154. Tabia yao ya **utiifu** si suala la mjadala kwani walikuwa tayari kwenda vitani wakiitwa wakati wowote mara moja bila kuchelewa anavyodhihirisha msanii katika beti za 154 na 155.

Baada ya Mtume Muhammad kupata habari kuwa Makureshi walikuwa tayari kwa vita, alilipanga jeshi lake bila tashwishi yoyote kisha wakaenda vitani. Kulingana na maelezo hayo, msanii amewachora kama wahusika **wenye ujasiri** kwani Mtume Muhammad alipanga watu hodari kweli kweli kukabiliana na maadui zake waliokuwa njiani kuwavamia. Walikuwa watu **wasiokuwa na hofu pamoja na wahaka**; hawakupenda mchezo na walipenda vita anavyotujuza mtunzi katika beti za 149, 150 na 152. Walikuwa **watiifu** kwa vile walikuwa tayari kwenda popote vitani kulingana na amri ya Rasuli kwao.

Msanii amewasawiri kuwa **wakali mno** kwani hii ndiyo sababu amewafananisha na panga kali anavyosimulia msanii katika ubeti wa 155. Ingawa hawakuwa wengi walijitayarisha na kuingia vitani bila wasiwasi wowote. Vile vile, wameelezewa kama **jasiri** kwa sababu ingawa walibakia wanajeshi mia saba dhidi ya wanajeshi wa Makureshi waliokuwa elfu tatu, hawakuogopa bali waliendelea na vita ilivyopangwa. Wamedhihirika kama watu wenye mpangilio kwa kuzingatia uongozi wa Mtume Muhammad ambapo wanajeshi hamsini aliwaamrisha kuchunga njia za

milimani anavyotudhihirishia mtunzi katika beti za 199 na 120. Hawa ndio walitambuliwa kama panga madhubuti.

Baadhi yao wamesawiriwa kama watu **wenye tamaa** kwani baadhi ya wale wanajeshi hamsini waliopaswa kuchunga njia za milimani walikaidi na kuondoka kinyume na amri ya Rasuli. Hii ikiwa ni kwa sababu walitamani mali iliyoachwa na Makureshi baada ya kuwafukuzia mbali. Tamaa hiyo iliwafanya kuadhibiwa na jeshi la Makureshi baada ya kurejea na kugundua njia za milimani zilikuwa wazi anavyotusimulia msanii katika ubeti wa 228. Baadhi yao wamesawiriwa kama **watundu** na wasiotii hii ni baada ya kukaidi amri ya Rasuli hata ingawa kiongozi wao alijaribu kuwasihi kutii waliikaidi kabisa.

### 3.2.6 Wanawake wa Kiislamu

Wanawake hawa vile vile tumewasawiri kwa sifa jumuishi. Wakiongozwa na mkewe Mtume Muhammad pamoja na bintiye Batuli walimtembelea Mtume Muhammad pangoni alimopafanya makazi ya muda akiuguza majeraha yake ya kivita. Msanii amewasawiri wanawake hawa kama watu **wenye nyoyo safi na zenye upendo** kwa kitendo chao cha kuamua kwenda kumwangalia Mtume Muhammad katika hali yake ya ugonjwa bila kujali hali tete ya kivita ambayo haikuwa imetulia kabisa. Vile vile, imedhihirika wazi kwamba ni wanawake **jasiri kupindukia** kwa vile hawakuona pingamizi yoyote ambayo ingewazuia kubatilisha kauli ya kumtembelea Mtume Muhammad wamwone ili nyoyo zao zipate faraja. Tabia yao **ya huruma** si jambo la kutiliwa shaka kwani walikuwa na wasiwasi mkubwa walipopata uvumi kwamba Mtume Muhammad kafariki ndio sababu walihitaji kujionea na kuthibitisha wao binafsi.

### 3.3.0 Muundo

Katika utafiti wetu, tumehakiki muundo ili kutathimini ulivyotumika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Muundo huelezea namna au jinsi ambavyo shairi linavyoonekana kiumbo. Katika sehemu hii tumeelezea namna muundo unavyojitokeza katika utenzi wa vita vya Uhud. Tumeangazia vipengele vya kimuundo kama vile: muwala, bahari, idadi ya mishororo, beti, mizani, vina, ukiushi wa kisarufi na tabdila.

### 3.3.1 Muwala

Katika utenzi huu, msanii amefanikiwa kufuma kazi yake kwa njia ya mshikamano tangu utangulizi wake hadi hitimisho. Msanii ametutangulizia utenzi kwa kukweza jina la Muumba,

anafuatia Mtume Muhammad ambaye ni Mtume wake. Baada ya utangulizi wake msanii anatuelezea chanzo cha pigano katika mlima Uhud. Hapa tunagundua kuwa kulikuwa na vita vya kwanza vya Badri ambapo Makureshi walishindwa na jeshi la Mtume Muhammad. Basi ikawa Makureshi wakaazimia kulipiza kisasi katika pigano la Uhud lililoandaliwa miezi tisa baada ya pigano la Badri. Katika hatima ya maelezo hayo msanii anatuelekeza kuelewa maandalizi yalivyofanywa na makundi mawili hasimu na kisha vita vyenyewe na athari ya vita hivyo. Mwisho kabisa msanii huyu anahitimisha utenzi wake kwa kumpa Mungu shukurani kwa kumwezesha kufika tamati mwa utunzi wake.

### 3.3.2 Bahari

Dhana bahari katika ushairi hutumiwa sawia na aina za mashairi. Katika fani ya ushairi kuna bahari nyingi kwa kuzingatia vigezo mbalimbali kama vile idadi ya mistari, ufupisho wa mistari, urudiaji wa maneno na kadhalika.

Ushairi wetu upo katika bahari ya utenzi. Sababu kuu ikiwa kila mshororo una mizani nane. Pili, shairi hili linatupa historia au maelezo marefu kuhusu makundi mawili hasimu ambayo ni ya Waislamu na Makureshi. Tunapata kuelewa kutoelewana baina ya Waislamu na Makureshi hadi wakapigana vita vya Badri na baadaye vita vya kihistoria vya Uhud. Vita hivi vinasimuliwa kama vita ambavyo havijawahi kupiganwa. Vile vile, katika usimulizi huu tunapatana na maelezo ya wahusika mashujaa wa makundi yote mawili na matendo yao ya kishujaa.

### 3.3.3 Ubeti

Ubeti ni mkusanyiko wa mistari inayobeba wazo moja linaloambatana na mawazo mengine kutoka katika mistari mingine inayounda beti kisha shairi zima linalojenga dhamira na maudhui hitajika. Utenzi huu una beti mia saba thelathini na tisa. Beti hizi vile vile, zimepangwa kwa urari unaovutia kwa lengo la kutuwasilishia masimulizi yenye mnato. Beti hizi zina ulinganifu wa mizani katika utenzi mzima.

### 3.3.4 Kina cha bahari

Kina ni silabi ya kati, kati na kati na mwisho katika kila mshororo wa shairi lolote. Kuna mashairi ambayo yamegawika katika vipande viwili au vitatu ilhali mengine kama vile; tenzi huwa na kina kimoja tu ambacho ni cha nje. *Utenzi wa vita vya Uhud* umetimiza kanuni ya utenzi kwani una

kina cha bahari ambacho huja mwishoni mwa mshororo wa nne katika kila ubeti. Kina hicho ni **li** na kimedumishwa katika utenzi mzima.

### 3.3.5 Mishororo

Mishororo ni idadi ya mistari katika kila ubeti wa shairi. Katika utenzi wetu kila ubeti una mishororo minne. Mistari hii hupangwa kwa mtiririko murua wa mawazo ya mtunzi ili kujenga dhamira na maudhui ya ushairi.

### 3.3.6 Vina

Hizi ni silabi zinazopatikana kati, kati na kati na mwishoni mwa mishororo ya ushairi. Vina aghalabu hutumika kuzua ulingano wa kisauti katika shairi kwa lengo la kuleta kiimbo hitajika katika ushairi husika. Katika utenzi wetu kuna kina kimoja tu ambacho huwa ni tofauti katika kila ubeti. Hata hivyo kina cha bahari katika utenzi wetu kinafanana utenzi mzima.

### 3.4.0 Uhuru wa kishairi

Hii ni idhini ambayo wasanii hupewa ambapo wana uhuru wa kufinyanga lugha kulingana na malengo yao ili kuwasilisha jumbe zao za kisanii kwa hadhira zao. Idhini hii humruhusu msanii kukiuka kaida za kisarufi za lugha husika ili kutimiza mahitaji yake ya kiutunzi. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* uhuru huu umetumika haswa kwa lengo la kutimiza utoshelevu wa mizani na vina.

### 3.4.1 Inkisari

Ni mbinu ambayo watunzi haswa wa mashairi hutumia kwa lengo la kufupisha maneno ili kuafikia idadi ya mizani hitajika katika ubeti au mishororo. Mbinu hii aghalabu hutumiwa na watunzi wa mashairi ya kiarudhi kwani haya ndiyo huzingatia kanuni ya utoshelevu wa mizani katika kila ubeti.

Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*, mtunzi ametumia mbinu hii kwa lengo hilo hilo ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wake. Kwa mfano katika ubeti wa 2 ametumia neno naandika badala ya ninaandika, katika ubeti wa 3 neno jinale limetumika badala ya jina lake, kwenye ubeti wa 4 neno mamboye limetumiwa badala ya mambo yake, ubeti wa 43 ametumia neno napatwa badala ya ninapatwa. Katika ubeti wa 49 msanii ametumia neno moyonimwa badala ya moyoni mwangu, neno nakwenda badala ya ninakwenda, neno nampanda limetumika badala ya ninampanda, ubeti wa 50 neno nenda limetumika badala ya ninaenda, neno nampanda badala ya ninampanda, ubeti wa 64 neno zikenda badala ya zikaenda, ubeti wa 66 neno yaso limetumiwa badala ya neno yasiyo,

ubeti wa 79 ametumia neno ndo badala ya ndiyo, ubeti wa 80 neno ikendelea badala ya neno ikaendelea.

Vile vile, ubeti wa 81 msanii ametumia neno zikangia badala ya zikaingia, ubeti wa 87 neno jinale limetumiwa badala ya jina lake, ubeti wa 114 neno moyonimo badala ya moyoni mwao, ubeti wa 115 neno walo badala ya walio, ubeti wa 116 neno jumulae limetumiwa badala ya jumla yake, ubeti wa 131 neno litalosaki badala ya litakalosaki, ubeti wa 148 kusikiakwe limetumika badala ya kusikia kwake, ubeti wa 175 neno jeshile limetumika badala ya jeshi lake, ubeti wa 219 neno neleze badala ya nieleze.

### 3.4.2 Mazida

Huu ni uhuru alio nao mtunzi wa kazi za kishairi ambapo anarefusha maneno yake kwa lengo la kutimiza idadi ya mizani inayohitajika katika shairi husika. Mbinu hii haswa huzingatiwa na watunzi wa mashairi ya kimapokeo. Hii ni kwa vile wao hushikilia kuwa ni sharti shairi kupangwa kwa mizani na vina kinyume na wanausasa ambao hawatilii maanani kauli hiyo. Katika utenzi wetu tumechanganua namna mbinu hii imemfaa msanii kuafikia idadi ya mizani na vina katika utenzi mzima.

Katika ubeti wa 29 msanii ametumia mazida katika neno **kuutungao** ambalo limerefushwa kutokana na neno **kuutunga** kwa kuliongezea irabu **o.** Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* msanii pia amefaulu kutumia mbinu hii katika kuwasilisha maoni yake. Katika beti wa 58 na 146 neno **kureshia** limetumiwa ambalo ni urefushaji wa neno **kureshi,** ubeti wa 94 neno **mhodari** limerefushwa kutokana na neno **hodari**, tazama beti za 104 na 194 neno **sabaa** limetumika ambalo ni urefushaji wa neno **saba**, ubeti wa 145 neno **hanayo** ni urefu wa neno **hana,** ubeti wa 223 neno **kuokotwapo** limerefushwa kutokana na neno **kuokotwa** na kadhalika.

### 3.4.3 Tabdila

Mbinu hii imejitokeza kama ifuatavyo katika utenzi wetu. Katika ubeti wa 12 neno **kino** limetumika badala ya neno **kimo**. Msanii katika ubeti wa 15 ametumia neno **dawama** badala ya neno **dawamu.** Vile vile katika ubeti wa 33 neno **ziruku** limetumika badala ya neno **zimeruka.** Katika ubeti wa 35 msanii ametumia neno **maarifu** badala ya neno **maarifa.** Kadhalika msanii ametumia neno **herufu** badala ya **herufi** ili kuapata kina katika ubeti wa 37. Neno **Nabia** badala ya **Nabii** limetumika katika ubeti wa 58. Msanii ametumia tabdila vile vile katika ubeti wa 223

anapotumia neno **nasabu** badala ya **nasaba.** Neno **kauma** vile vile limetumika katika ubeti wa 313 badala ya neno **kaumu.** Hizi ni baadhi ya ithibati ambazo mtunzi wa utenzi huu amefanikiwa kuzitumia katika ufinyanzi wa kazi yake. Mbinu hii imemfaa msanii huyu kupata vina kwa njia ya urahisi katika utunzi wa kazi yake.

### 3.4.4 Ukiushi wa kisarufi

Mbinu hii aghalabu hutumika katika mashairi kwa lengo la kutimiza urari wa vina katika vipande vya mistari. Mbinu hii, aghalabu hukiuka mpangilio wa sarufi ya lugha yenyewe kwa kukidhi mahitaji ya kisanaa. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud,* msanii amefanikiwa kuitumia mbinu hii katika usukaji wa kazi yake. Katika utafiti wetu tumeonyesha mifano mbalimbali kama ifuatavyo.

Katika ubeti wa 41 kauli …huu wimbo… imetumika badala ya …wimbo huu. Kwenye ubeti wa 30 kauli …huniondoka fahamu… imetumika badala ya …fahamu huniondoka. Katika ubeti wa 29 usemi …utenzi kuutungao… umetumika badala ya …kuutungao utenzi. Katika ubeti wa 76 kuna sentensi inayosema …kila zana kutafuta… badala ya kusema …kutafuta kila zana. Vile vile katika ubeti wa 77 kuna kauli inayosema …zivunje japo jabali… badala ya …japo zivunje jabali. Kwenye ubeti wa 100 kauli …chao kishindo… imetumika badala ya …kishindo chao. Kwenye ubeti wa 111 kauli …ili wengi hao watu… imetumika badala ya …ili watu hao wengi.

Kwenye ubeti wa 203 msanii ametumia sentensi …pa kwenda wapi mahali badala ya …wapi mahali pa kwenda. Ametumia msitari …katika pao pahali…badala ya …katika pahali pao. Msitari …ni moja yao nasabu… umetumika badala ya …yao nasabu ni moja…tazama ubeti wa 233. Katika ubeti wa 290 kauli …katika yake kauli…imetumika badala ya …katika kauli yake. Kwenye ubeti wa 368 mshororo …la kufanya alijue…umetumika badala ya …alijue la kufanya. Vile vile sentensi …ni hapo tena mahali badala ya …ni mahali hapo tena. Tazama ubeti wa 372. Msitari …niupoze wangu moyo…umetumika badala ya …niupoze moyo wangu. Tazama ubeti wa 424. Katika ubeti wa 448 sentensi …hajijui yake hali… imetumika badala ya …hajijui hali yake. Kwenye ubeti wa 520 kauli …mno walijitahidi…imetumika badala ya …walijitahidi mno. Mshororo …ni mmoja yao baba …umetumika badala ya …baba yao ni mmoja. Tazama ubeti wa 530. Katika ubeti wa 631 sentensi …limeisha letu pigano…imetumika badala ya pigano letu limeisha. Katika ubeti wa 734 msitari …hapo ndo pangu mahali… umetumika badala ya …hapo ndo mahali pangu. Mshororo …katika yangu makali… umetumika badala ya …katika makali yangu kama ilivyo katika ubeti wa 739.

### 3.5 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili kipengele cha wahusika na uhusika wao katika utenzi wetu. Tumegawa wahusika hawa katika makundi mawili makuu ambayo ni kama vile: wahusika kimakundi pamoja na wahusika wa kibinafsi. Sifa zao zimetokana na maoni ya mtunzi, maoni ya wahusika wenzao kuwahusu pamoja na vitendo vyao katika utenzi wenyewe. Vile vile tumefafanua namna muundo umejitokeza katika utenzi huu na kubainisha umuhimu wake katika utenzi huu. Katika sura inayofuata tumeangazia tamathali za usemi, mbinu rejeshi pamoja na kipengele cha taswira.

## SURA YA NNE

## TAMATHALI ZA USEMI, MBINU REJESHI NA TASWIRA KATIKA UTENZI WA VITA VYA UHUD

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii, kimsingi tumeshughulikia tamathali mbalimbali za usemi, mbinu rejeshi pamoja na kipengele cha taswira vinavyotumika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Tumetoa mifano ya takriri zinazojitokeza katika utenzi huu. Pili, tumeeleza mbinu ya chuku, tashhisi, kinaya, maswali ya balagha na tashbihi zinavyotumika katika utenzi huu. Vile vile, tumeangazia mbinu rejeshi na taswira mbalimbali na jinsi zimetumika katika utenzi huu. Kisha tumehitimisha sura hii kwa kutathimini yote ambayo tumeyashughulikia kwa jumla kimukhutasari.

### 4.1.0 Tamathali za Usemi

Kulingana na Ndumbu (2013) tamathali za usemi ni mbinu za kutumia lugha ya kisanaa na ya mkato inayomsaidia msanii kuwasilisha ujumbe wake mrefu kwa maneno haba yenye mnato na mguso. Anazidi kueleza kuwa, tamathali hizi huwa ni vipengele muhimu vinavyotumika katika uchanganuzi wa lugha ya kifasihi kwa jumla. Hata hivyo ni muhimu kutambua kuwa tamathali za usemi si eti hupatikana katika lugha ya fasihi peke yake, zipo katika mawasiliano ya kawaida ingawa aghalabu hutumika bila wanaowasiliana kutarajia.

Kwa mtazamo wetu, tamathali za usemi ni matumizi ya semi fupifupi ambazo hulenga kuwasilisha dhamira na maudhui ya kazi ya fasihi kwa hadhira lengwa. Semi hizi zikitumiwa vyema na msanii yeyote bila shaka huleta mnato fulani katika kazi yake unaomvutia msomaji wa kazi yake ya kifasihi. Hali hii inamchochea msomaji kutafakari maana halisi ambayo aghalabu hubanwa kwenye mafumbo na jazanda ambazo hutumiwa na wasanii kuwasilisha jumbe zao. Katika utafiti wetu tumejadili tamathali za usemi ambazo msanii wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* ametumia kufinyanga kazi yake. Yafuatayo ni maelezo ya tamathali za usemi zinavyotumika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

### 4.1.1 Takriri

Takriri ni urudiaji wa sauti, neno au sentensi katika kazi ya kifasihi.  Lengo mahususi la kutumia takriri katika kazi ya fasihi ni kusisitiza maudhui fulani ambayo msanii angependa yaeleweke

kikamilifu kwa hadhira yake. Kuna aina mbalimbali za takriri zinazotumika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* kama vile takriri vokali, takriri silabi, takriri neno, na takriri sentensi.

#### 4.1.1.1 Takriri silabi

Takriri silabi ni urudiaji wa silabi ambazo aghalabu huwa ni muungano wa konsonanti na vokali au vokali peke yake. Mbinu hii ya takriri silabi vile vile imetumika katika utenzi huu kwa lengo la kuleta kiimbo kinachopendeza sikio. Aghalabu kiimbo hiki hufanya shairi kuimbika katika sauti yenye mnato kwa msikilizaji. Kwa mfano katika ubeti wa 2 silabi **na** imerudiwa katika mistari ya mwanzo mitatu inavyodhihirika katika ubeti ufuatao:

**Na**anza kushika kalamu,
**na**tanguliza isimu,
**na**andika Jina Adhimu
bisimilahi awali.
(ub. 2)

Katika ubeti wa 84 vile vile, silabi **na** imeradidiwa kama tunavyoonyesha katika nukuu ifuatayo hapa chini. Katika ubeti huu, baada ya msimulizi kutuelezea namna Makureshi waliaibika baada ya kushindwa katika vita vya Badri, anarejelea nafsi ya kwanza kutuhakikishia kuwa yu tayari sasa kuanza kuandika kisa chenyewe, yaani kuhusu pambano la Uhud. Tazama:

**Na**ndike uandikike
**na** ndugu wafurahike
niwambie jina lake
**na** vita vya pigo hili
(ub. 84)

Kwa kweli takriri silabi tofauti tofauti zimetumika kwa wingi katika utenzi huu na huu ndio msururu wa beti ambapo tumethibitisha utumizi wake. Beti ni kama vile: 16, 24, 29, 30, 34, 39, 45, 50, 64, 70, 71, 77, 84, 85, 88, 89, 92, 98, 104, 107, 110, 124, 130, 132, 133, 135, 138, 141, 142, 143, 148, 153, 154, 156, 165, 171, 178, 179, 192, 196, 199, 221, 227, 235, 243, 254, 255, 259, 265, 270, 277, 287, 288, 289, 295, 296, 297, 299, 300, 305, 308, 310, 313, 315, 321, 323, 324, 329, 331, 333, 337, 346, 356, 360, 362, 376, 381, 382, 396, 399, 407, 408, 409, 410, 414,

417, 423, 426, 434, 440, 441, 443, 447, 458, 462, 476, 479, 484, 487, 491, 493, 496, 498, 503, 504, 505, 509, 510, 511, 512, 517, 520, 521, 529, 532, 535, 537, 550, 559, 560, 562, 566, 573, 581, 583, 587, 591, 597, 681, 693, 694, 697, 699, 706, 714, 720, 722, 730, 734, 737 na 738.

Ni muhimu kutaja kuwa katika utenzi huu silabi za mwisho wa mishororo pia zimeradidiwa kuleta ulingano wa vina na kiimbo sawa. Hata hivyo, tumetambua kuwa silabi hizo huwa tofauti kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Kwa kurejele beti tulizonukuu hapo juu ambazo ni ubeti wa 2 na ubeti wa 84, silabi **mu** katika ubeti wa 2 imeradidiwa kutoka mshororo wa kwanza hadi ubeti wa tatu ilhali katika ubeti wa 84 silabi **ke** imeradidiwa namna hiyo hiyo.

#### 4.1.1.2 Takriri vokali

Aghalabu, mtunzi huradidi irabu katika maneno au sentensi ili kuibua mdundo au ridhimu fulani katika utungo wake hususan ushairi. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* uradidi huu umetumika kwa wingi. Tumetambua takriri ambapo irabu imerudiwa mwanzoni mwa mishororo na zingine kuradidiwa mwishoni mwa mishororo ya baadhi ya beti kama tutakavyoonyesha hapa chini.

##### 4.1.1.2.1 Takriri vokali zinazojitokeza mwanzoni mwa mishororo

Katika ubeti wa (389) msanii ameradidi nafsi ya tatu **a** kusisitiza namna ambavyo sahaba wa Mtume Muhammad aitwaye Ali alimtoa Mtume Muhammad shimoni baada ya kujeruhiwa na Makureshi kwa kumiminiwa mawe mengi inavyodhihirika katika nukuu ifuatayo:

Kainyosha mikonoye
**a**mpate amgwie
**a**mfuate atoe
**a**toke nje Rasuli.
(ub. 389).

Katika nukuu ifuatayo pia msanii ameradidi nafsi ya tatu **a** kwa kumrejelea shujaa wa Makureshi ambaye ni Ubayyi bin Khalafu. Katika ubeti ufatao msanii anaeleza namna shujaa huyo alivyoenda mbele za Mtume Muhammad akiwa juu ya farasi wake akidai kupambana na Mtume Muhammad.

**A**ma Mkureshi huyu
**a**li adui mkuu,
**a**likuja yuko juu

katika wake haili.

(ub. 416).

Katika utenzi huu kuna beti nyingi ambazo zimedhihirisha matumizi ya takriri vokali kukiwemo: ubeti wa 13, 23, 75, 79, 128, 144, 147, 161, 172, 190, 205, 213, 309, 336, 340, 367, 370, 377, 384, 387, 389, 392, 416, 417, 427, 439, 452, 481, 577, 613, 624, 662, 684 na 729. Katika mifano hii, msanii amefanikiwa kutumia angalau takriri ya vokali katika mistari miwili katika kila ubeti. Tumegundua kuwa msanii huyu ameradidi vokali **a** na **i** kwenye takriban mifano yote tuliyoitambua katika beti hizo. Vile vile, ni muhimu kutambua kuwa mifano ya takriri ambayo tumebainisha hapa ni takriri vokali ambazo huja mwanzoni mwa mishororo katika kila ubeti.

#### 4.1.1.2.2 Takriri vokali zinazojitokeza mwishoni mwa mishororo

Takriri hizi aghalabu hutokea wakati vokali inafuatwa na vokali. Msanii huyu amefanikiwa kudhihirisha takriri hizi kikamilifu kwa kushirikisha wakati mwingine maneno tata kuafikia malengo yake. Tumegundua kuwa msanii huyu ametumia vokali **a, i** na **o** ijapokuwa ametumia mifano haba ya uradidi wa vokali **u** katika baadhi ya beti zake.

Tazama:

Yeye alitanguli**a**

kabla ya mawali**a**

na jamii Anbi**a**

pamwe nayo Murisali

(ub. 21).

Na mimi niupenda**o**

utenzi kuutunga**o**

na tena kwa lugha ya**o**

iitwayo Kiswahili.

(ub. 29).

Jeshi hili lilikuwa

farasi limechuk**u**a

ambao wasio t**u**a

idadiye mia mbili

(ub. 136)

Mifano ya mingine ya takriri hizi katika utenzi huu ni katika beti: 21, 58, 80, 104, 112, 124, 126, 132, 136, 138, 152, 159, 165, 167, 176, 177, 184, 194, 199, 200, 209, 221, 225, 229, 269, 264, 272, 287, 289, 291, 293, 295, 296, 304, 314, 335, 342, 350, 356, 372, 377, 386, 389, 390, 394, 396, 402, 412, 429, 446, 483, 499, 508, 517, 518, 519, 529, 539, 541, 552, 555, 559, 560, 562, 565, 567, 581, 582, 588, 593, 594, 601, 613, 625, 636, 647, 668, 675, 693, 699, 701, 715, 720, 727 na 734.

#### 4.1.1.3 Takriri neno

Hapa ni pale ambapo maneno hurudiwa katika ushairi. Urudiaji huu pia hulenga kusisitiza jambo fulani. Ifuatayo ni mifano ya takriri neno inavyodhihirika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*.

Neno **Lillahi** linaloleta maana ya Mungu limerudiwarudiwa inavyodhihirika katika beti za 3, 5, 6 na 7. Vile vile, neno **Rahmani** ambalo ni mojawapo la majina ya Mwenyezi Mungu na lililo na maana ya mwenye huruma pia limerudiwa katika beti za 8, 9, 10 na 12. Takriri hizi zimetumika kusisitizia msomaji kuelewa Mungu pamoja na tabia yake ya kuwa na huruma kila wakati kwa binadamu aliowaumba.

Katika ubeti wa 91 neno **jangwa** limerudiwa katika mstari wa 1 na 2. Msimulizi hapa anatusisitizia kuelewa mandhari anakosafiri juu ya nyumbu wake. Mandhari ni jangwani ambako kulingana naye, huwa na changamoto si haba. Neno **watu** pia limerudiwa katika beti za 103, 104, 106, 108, 110, 111 na 116 ambapo limetumika kurejelea vijana wapiganaji wa Makureshi ambao walitoka Maka na kuingia Madina. Vijana hao wanajulikana kama wapenda ugomvi na vurugu.

Kirejeshi **ndiye** pia kimerudiwarudiwa katika ubeti wa 203. Hapa mtunzi anasisitiza ufaafu wa Mansabu bin Omari kubeba bendera ya jeshi la Mtume Muhammad kwa sababu ya ushujaa wake. Katika ubeti wa 332 neno **ajili** limerudiwa katika mstari wa mwisho kutilia mkazo hali ya wasiwasi wakati Makureshi waliwavamia Waislamu. Katika ubeti wa 333 neno **kweli** limerudiwarudiwa kuonyesha hali ya kisasi walichoonyesha Makureshi kwa Waislamu. Vile vile katika ubeti wa 342 neno hilo hilo limerudiwa kuonyesha shujaa Mansabu wa Omari alivyofananishwa na Mtume Muhammad hadi pale alipojeruhiwa na Makureshi wakadhani kwamba walikuwa wamemwangamiza Rasuli.

Kiunganishi **na** katika ubeti wa 411 pia kimerudiwa katika mstari wa 2 na 3, kimetumika kama kiunganishi kwa kurejelea jitihada za Makureshi kumuangamiza Rasuli walipogundua alikuwa hajafa. Katika ubeti wa 454 neno **kaniua** limerudiwa na Ubayyi bin Khalafu alipokuwa akilia kwa kupata kipigo kutoka kwa Rasuli alipomrushia kijambia kikaingia shingoni pake asipate wokovu. Alikuwa akiwaarifu rafikize kuwa alikuwa kachungulia kaburi bila wao kuamini na mwishowe alifariki njiani kabla ya kufika Maka.

Neno **tangu** limerudiwa katika ubeti wa 558 kusisitiza umilele wa Mungu Muumba. Hapa ni pale ambapo Rasuli alifanya sala ya kumwomba Mungu nafasi ya kumdhuru adui yake Ubayyi bin Khalafu aliyejidai kuwa ndiye hodari zaidi ya Rasuli na kudhani angemdhuru. Katika beti wa 672 na 673 neno **siku** limerudiwa kuleta dhana kwamba vita ni mpokezano, ambapo vita vya Badri Waislamu walishinda ilhali vya Uhud wakalemewa. Waislamu walifanya ajizi kwa kukaidi kufuata mawaidha ya Mtume Muhammad hasa baadhi ya wale wanajeshi hamsini walipowacha jukumu la kulinda njia za milimani.

Vile vile, neno **wala** limerudiwa katika ubeti wa 677 ambapo Sayyid Umari alijitokeza na kushukuru juhudi za jeshi lake vitani ijapokuwa hakuwaelekeza kwa yote waliyofanya bali ni Mungu wao anayeitwa Hubali. Kwenye ubeti wa 706 **ni** pia imerudiwa kurejelea ushujaa wa Bwana Hamza.

### 4.1.2 Tashbihi

Huu ni ulinganishi wa vitu viwili kwa kutumia vilinganishi mbalimbali kama vile: mithili ya, ja, kama, mfano wa, shabiku ya, tamthili ya na kadhalika. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* mbinu hii imetumika kwa lengo la kuifanya kazi hii kuwa yenye mnato na mvuto kwa msomaji.

Kulingana na King'ei na Kemoli (2001), tashbihi vile vile huitwa tashbiha au mshabaha. Huu ni ufananisho wa vitu viwili au zaidi ambavyo huwa na ufanano kisura au kitabia. Naye Wamitila (2003) anafafanua tashbihi kama tamathali ambapo vitu viwili hufananishwa waziwazi kwa kutumia vifananishi kama vile: mfano wa, mithili ya, ja, falau na kadhalika. Ufafanuzi zaidi kwa tashbihi unatolewa na Mohammed (1995) anapoeleza kuwa tashbihi katika kazi ya sanaa ni ufananisho ule unaolenga kuweka wazi ujumbe, dhana, picha au hali fulani ya mambo kwa kuilinganisha kupitia picha.

Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud,* msanii ametumia tashbihi kulinganisha vitu au hali katika harakati ya kuwasilisha dhamira yake na maudhui katika utenzi huu. Kwa mfano katika ubeti wa 70 msanii anaelezea hali ya **kukonda kama ng'onda** kwa Makureshi baada ya kupigwa katika vita vya Badri. Kauli hii bila shaka inaashiria hali ya kujidharau kwa Makureshi kwa kupata kichapo cha ajabu na wanajeshi wa Muhammad ambao walikuwa haba ukilinganisha na jeshi lao la watu elfu tatu. Walirejea makwao kwa aibu kubwa. Hili liliwafanya kujiandaa kulipiza kisasi dhidi ya jeshi la Waislamu baada ya miezi tisa.

Katika ubeti wa 138 tashbihi kuwa **Makureshi wakaikabili njia kama matari mithali.** Wingi wa ngamia hao ulifunga barabara hadi waliopanda juu wakaonekana kama wale ambao wanaruka. Hali hii inaashiria jinsi jeshi la Makureshi lilivyojiandaa kwa kishindo kuingia vitani. Walikuwa wamejiandaa kweli kweli. Katika ubeti wa 157 jeshi la Mtume Muhammad lilikuwa tayari **kuandamana na Mtume kama moshi** kufukuzia mbali Makureshi. Kauli hii ya tashbiha imetumika kusisitiza namna ambavyo jeshi la Mtume Muhammad lilivyokuwa tayari kumfuata Mtume Muhammad kwa hali yoyote.

Vile vile katika ubeti wa 196 msanii ametumia tashbihi kwamba **Makureshi walikuwa watu kathiri wazagaa ja ramli** kwa lengo la kusisitiza wingi wa wanajeshi hao ambao walisambaa kila mahali. Katika ubeti wa 199 Mtume Muhammad alipowateua wanajeshi wake hamsini **akawaweka ili ngao** kusisitiza nafasi kuu waliyopaswa kutekeleza askari hao wa Rasuli waliochunga njia zile za milimani wakati wa vita vya Uhud kuzuia Makureshi kuingia na kuwashambulia Waislamu wakati wa vita. Katika ubeti wa 245 mbeba bendera mmoja wa Makureshi **aliuawa akaanguka kama gogo** kauli inayosisitiza namna ambavyo shujaa huyo alivyouawa.

Katika ubeti wa 276 msanii ametumia tashbihi kutuonyesha namna ambavyo Makureshi walipolemewa vitani **walivyokwenda mbio ja kuku aliyeona mwewe**. Kauli hii inaashiria jinsi jeshi la Makureshi liliamua kutoroka kuokoa maisha yao baada ya vita baina yao na Waislamu kuchacha. Katika ubeti wa 284 tashbihi kuwa jeshi la Makureshi **lilizingira jeshi la Mtume Muhammad ja moshi** ni kuonyesha jinsi jeshi la Makureshi lilizingira jeshi la Rasuli kwa wingi. Katika ubeti wa 330 kuna tashbihi kuwa **Makureshi kujaa juu kama moto na kifuu kingurumo na ukali,** hili linaashiria hasira na kisasi walichokuwa nacho Makureshi kwa Waislamu. Waislamu wengi sana waliuawa pamoja na wengine wengi kupata majeraha makubwa.

Katika ubeti wa 350 habari za uwongo kuhusu kifo cha Mtume Muhammad **zikazagaa pasi mahali kusaza kama maji.** Hili ni thibitisho kuwa habari kuwa Rasuli kafariki vitani ilipenya pembe zote na kila mtu kuipata kwa wasiwasi mkubwa. Katika ubeti wa 364 kuna tashbihi kwamba **watu katika vita hivi walikatana kama wembe.** Tashbihi hii inaonyesha namna ambavyo vita vilichacha katika pande zote mbili na kusababisha madhara makubwa. Katika ubeti wa 543 kuna tashbihi kuwa ukamiminika damu uso wa Muungamu ja maji na mziramu yachimbukapo mahali kauli ambayo ni dhihirisho kuwa Rasuli alikuwa amepata pigo kubwa kutoka kwa mahasimu wake na kutokwa na damu nyingi. Pigo lenyewe lilitokana na kumiminiwa mawe kadhaa ambayo yalimpa majeraha makubwa.

### 4.1.3 Maswali ya balagha

Katika mbinu hii, msanii huuliza maswali yanayomfanya msomaji kumakinika zaidi katika usomaji wa kazi yake ijapokuwa maswali hayo huwa hayahitaji majibu kwani aghalabu msomaji huwa ana jibu lenyewe au linalorejelewa huwa ni la kawaida na hivyo hujulikana na kila mmoja. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*, msanii ametumia mbinu hii kwa lengo la kuchochea fikra za ndani za msomaji au kusisitiza wazo fulani.

Katika ubeti wa 61 kuna swali ambalo limeuliza **"ni nani ataempata Muhammad kumleta japokuwa chake kitwa pasina kiwiliwili?"** Swali hili linalenga kuwachochea wazalendo wa kikureshi kutia bidii zaidi kuhakikisha wamemuangamiza Rasuli. Pia kwenye ubeti wa 124 msanii anauliza swali, **"kwa kuiogopa haya nani muweza kimbia na hapo watabakia zaujati na baai?"** Hapa msimulizi analenga kutuhakikishia kuwa wanaume hawawezi kukubali aibu ya kushindwa mbele ya wake zao. Hivyo basi, wanawake wa kikureshi kuja vitani, walilenga kuhakikisha wanaume wametia juhudi mara dufu bila kulegea vitani. Kulingana na mtunzi huyu, wanaume hawapendi aibu mbele ya wake zao. Kwa hivyo ujaji wao katika vita hivi kulikuwa ni kuwachochea kabisa ili wapate ushindi katika vita hivyo.

Swala la balagha lingine ni katika ubeti wa 203 ambapo msanii anauliza, **"kureshi wataposaki kwa jeshi na kuhamaki katikati haijiki pa kwenda wapi mahali?"** Swali hili linasisitiza kuwa iwapo jeshi la Rasuli lingezingira pembe zao zote Makureshi wasingepata nafasi ya kuingia ndani kuwashambulia.  Sababu hii ndiyo ilimfanya Rasuli akaweka majeshi yake kuchunga njia za milimani zote. Kwenye ubeti wa 354 msanii alitaka kutuonyesha kuwa baada ya habari ya kifo cha Mtume Muhammad Waislamu walibakia wasijue la kushika yaani hali ya kubabaika na kuuliza,

**"ni lipi la kufanyika jambo lilo afadhali?"** Hapa swali hili linatuonyesha jinsi Waislamu walianza kubabaika baada ya kupokea ujumbe kuwa Rasuli alikuwa ameangamizwa vitani. Walijawa na wasi wasi na woga dhihirisho tosha kuwa walikuwa wamemwamini Mtume Muhammad zaidi na hivyo wasingependa mauko kumpata katika vita hivyo.

Tazama ubeti wa 362 ambapo msanii anahoji kujua, **"madharuba kumetoka, ni nani muweza toka?"** Hapa ni dhahiri kwamba vita vilichacha na watu wakauawa yeyote asitumainie kupona. Hata hivyo watu walijitolea kutoka pande zote kuzidi katika vita bila kukoma. Kwenye ubeti wa 459 swali la balagha wapiganaji wenzake wanamwuliza Ubayyi bin Khalafu kuwa, **"tambo waliivuruga ngapi siku tumekuwa hatujakuona mwoga?"** Hapa msimulizi anatuelezea mshangao wa Makureshi eti Mtume Muhammad alimjeruhi Ubayyi bin Khalafu jeraha la kufa. Wanamcheka eti amekuwa mwoga na mjinga siku gani bila wao kutambua. Hii ilikuwa ni kwa vile awali alikuwa amestahimili majeraha makubwa makubwa bila yeye kulalamika.

### 4.1.4 Istiari

Kulingana na Kuvuna na wengine (1992) sitiari ni mbinu ambapo msanii hulinganisha vitu viwili ambavyo ni tofauti kabisa kwa kufuatisha sifa moja vilivyo nayo bila kuitaja sifa hiyo. Maelezo haya yanashabihiana na ya Wamitila (2008), anayesema kuwa hii ni tamathali inayolinganisha vitu viwili bila kutumia vifananisho vyovyote kama vile; kama, mithili ya, kwa mfano katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* mwandishi ametumia istiari kutoa ulinganisho wa aina tofauti tofauti ili kuleta msisitizo au shada katika kazi yake.

Katika ubeti wa 25 msanii ametumia istiari akilenga kumsifu Mtume kama vile: **Muhammadi ndiyo taji, ndiyo nuru-i-siraji, ni badiru-i-kamali.** Ishara ya taji inaashiria kuwa Mtume Muhammad ni kiongozi wa dini ya Kiislamu duniani, ishara ya jua inaashiria kuwa yeye atabaki kuwa kiongozi wakati wa furaha na faradhi kisha ishara ya mwezi ikiashiria uongozi wake kwa waumini wa Kiislamu wakati wa shida na majonzi. Ishara hizi hutusisitizia kuwa Mtume Muhammad ni kiumbe cha Mungu ambacho ni cha thamani kubwa kwake. Ni kiumbe ambacho ni bora zaidi ya viumbe vyote alivyoumba Muumba.

**Wanajeshi wale hamsini wa Mtume Muhammad wanaitwa panga madhubuti** kwa lengo la kusisitiza kuwa walikuwa wakali katika vita. Istiari hii pia inaashiria kwamba wanajeshi hawa walikuwa watu wasioweza kubembeleza wala kuonea yeyote huruma kama zilivyo panga kali

zinazokata kulingana na inavyohitajika. Vile vile inaashiria sifa ya utiifu wao kwa sheria na maagizo ya Mtume Muhammad. Tujuavyo panga huwa hazina uwezo juu ya anayezitumia bali hutumika kwa njia yoyote. Huenda hii ikawa ndiyo maana msimulizi anawaita wale wanajeshi hamsini wa Mtume Muhammad panga madhubuti inavyodhihirika katika beti za 200-202.

Msimulizi anatupa taswira ya mauaji ya wabeba bendera wa Makureshi kutoka uzao wa Banu Abdi-Dari ambao waliangamizwa asibakie yeyote wa kuibeba tena. Ghafla bin vuu akatokea mwanamke na kuibeba bendera hiyo kisha pambano likaendelea kwa muda mfupi. Katika **maelezo yake msimulizi alipomwona mwanamke huyo alisema kwamba alikuwa ameingia kichinjioni.** Ishara hii inadhihirisha kuwa vita vilikuwa vimewalemea Makureshi wasijue la kufanya kama ng'ombe aliyefikishwa kichinjioni. Vita viligeuka kichinjio cha Makureshi kumaanisha kila mtu aliyeenda mbele kubeba bendera hakuwa na ambacho angekifanya kuzuia kifo. Istiari hii inaashiria uhasama ulioshuhudiwa katika pigano hili la Uhud.

Katika ubeti wa 704 msanii ametumia istiara anapoelezea kuwa **Hamza aliyeuawa alikuwa ni simba wa jalali.** Maelezo katika kauli hii yanatoa msisitizo kuwa Hamza alikuwa ni hodari na shujaa kweli kweli. Hii ilikuwa ni kutokana na ujasiri wake vitani bila woga abadan. Ijapokuwa Hamza aliuawa kwa kuumizwa vibaya sana alikuwa shujaa kweli kweli. Mbinu hii ya ufananisho hutumiwa katika kazi za kifasihi kusifu au wakati mwingine kukejeli anayerejelewa au kinachorejelewa.

### 4.1.5 Chuku

Katika mbinu hii ya lugha msanii hutia chumvi ujumbe kwa lengo la kuufanya ujumbe huo kupendeza na hivyo kuvutia hadhira. Kutia chumvi ina maana kuwa maana ambayo haikuwepo katika mawasiliano lengwa huongezwa kwa lengo la kutia ladha ujumbe wenyewe. Aghalabu ujumbe uliotiwa chumvi hujitokeza kwa njia ya msisitizo na mvuto kwa msomaji au msikilizaji.

Katika ubeti wa 102 msanii anatufafanulia tabia ya wanajeshi wa Makureshi kuwa wanafananishwa na silaha inayoweza kumwua adui kwa mbali. Hapa msanii ameitumia kusisitiza ukali wa jeshi hilo katika vita. Madai ya Ubayyi bin Khalafu kwamba uchungu aliohisi baada ya kurushiwa kijambia na Mtume Muhammad kuwa kila binadamu angepata fungu lake na ubakie, ni chumvi tupu. Msanii ametumia mbinu hii hapa kutueleza kwamba uchungu huo ulikuwa mbaya zaidi ambao hauwezi kufananishwa inavyodhihirika katika beti za 473-478. Vile vile, katika ubeti

wa 352, anafafanua kuwa uvumi wa kifo cha Mtume Muhammad ulipowafikia Waislamu, uliwashangaza na kuwafanya kuwa na wasiwasi hadi wakashindwa kuelewa kilichotokea. Msanii huyu ametumia chuku anaposema kuwa ujumbe wenyewe uliwafanya kurukwa na akili. Msanii analenga kusisitiza kuwa ujumbe huo uliwaathiri Waisilamu zaidi. Hali hii inadhihirisha kuwa Waislamu wanamuenzi sana Mtume Muhammad. Ujumbe katika ubeti huu umetiliwa chumvi pale ambapo mtunzi anatuambia kuwa Waislamu walirukwa na akili punde tu walipopata habari kuwa Mtume Muhammad alikuwa amefariki baada ya uvamizi wa Makureshi katika vita vya Uhud. Mtunzi hapa ametumia chuku kusisitiza jinsi Waislamu walijawa na wasi wasi baada ya ujumbe huo kuwafikia.

### 4.1.6 Kinaya

Katika sanaa ya uandishi, msanii husema jambo ilhali anamaanisha kinyume cha anachosema. Ni pale ambapo usemi usemwao hulenga kutoa maana kinyume. Wakati mwingine ni kinaya wakati jambo hutokea kinyume na matarajio. Mbinu hii ndiyo huitwa kinaya. Kulingana na Murungi (2013) akiwanukuu Chimerah na Njogu (1999), anaeleza kuwa mbinu hii inahusu ukinzani kati ya hali ilivyo na isemekanavyo. Ni maana iliyo kinyume na matarajio. Tamathali hii katika kazi za kisanii huwa na lengo la kuzua ujumbe ambao si wa moja kwa moja kwa kutia chumvi au kukejeli yote kwa lengo la kusisitiza ujumbe husika. Wakati wa kusoma kazi za kisanaa, msomaji sharti ajue kuwa kauli zinazodokeza kinaya humlazimu kuzitilia maanani zaidi na kuzidadisi ili kutambua maana fiche. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud,* mbinu hii pia imetumika kwa lengo la kurutubisha utenzi huu yaani kuufanya uwe wa kuvutia.

Mfano; Katika beti za 420 na 421 tunapata picha ya namna ambavyo shujaa wa Makureshi aitwaye Ubayyi bin Khalafu alivyojivika nguo za kivita akitaka kukabiliana na Mtume Muhammad. Kinaya ni kwamba, ingawa hivyo, aliuawa kwa njia rahisi sana. Mtume Muhammad alimsukumia kijambia kikamwingia katika shingo yake na kumpa jeraha lililomsafirisha kaburini kabla ya kufika kwao Maka. Kinaya hiki kinatudhihirishia kuwa kweli Mtume Muhammad ni mwenye nguvu na ujuzi zaidi ya binadamu anavyosimuliwa mwanzoni mwa utenzi huu na msimulizi. Maelezo hayo ni kinaya kwa sababu, ingawa shujaa huyu alikuwa amejivika kadri tunavyoelezwa, mavazi hayo hayakumkinga na jeraha la Mtume Muhammad. Alipata pigo ambalo mwishowe lilimsafirisha kifoni bila huruma yoyote.

### 4.1.7 Uhaishaji

Katika mbinu hii, msanii hukipa kitu kisichokuwa na uhai sifa za kitu chenye uhai ambapo chaweza kujisimamia katika mandhari yake. Maelezo haya ni sawa na ya Murungi (2013) anayefafanua uhaishaji kama mbinu ambapo vitu visivyo hai hupewa sifa ya ubinadamu. Kulingana naye, tamathali ya uhuishi hulenga kusisitiza wazo fulani. Mbinu hii ni mojawapo ya ubunilizi katika lugha ya kisanii. Kwa namna mbalimbali mbinu hii imetumika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* kumsaidia msanii kuwasilisha ujumbe wake kama tunavyodokeza hapa chini:

Wakati vita vilichacha na kuwalemea Makureshi, washika bendera waliuawa na pasibakie aliyekuwa jasiri kwenda mbele kutekeleza wajibu. Msimulizi ametumia uhaishaji anapoeleza kuwa '…bendera imejitenga ili juu ya mchanga.,' hapa ameipatia bendera sifa ya binadamu kwani bendera haiwezi kujitenga bali itatengwa. Msimulizi ametumia mbinu hii kusisitiza kuwa mashujaa wa Makureshi walihofia maisha yao ndio maana waliisaliti bendera inavyosimuliwa katika beti za 266 na 267 ambapo msimulizi ameipa bendera sifa ya kutafuta anaposema '…bendera inatafuta nani wa kuiokota?' Kitendo cha kutafuta hutendwa na viumbe hai. Matumizi yake katika muktadha huu ni kudhihirisha kwamba watu waliogopa na kuamua kuhifadhi maisha yao badala ya kuibeba bendera yenyewe na kupoteza maisha yao.

Uhaishaji vile vile umejitokeza katika ubeti wa 320 ambapo msanii amepatia panga za kivita sifa ya kibinadamu ya kuwa na tamaa ya damu. Sifa hii ni ya kibinadamu kwani ni binadamu pekee ambaye huwa na sifa ya tamaa. Sifa hii ameitumia kusisitiza namna ambavyo hasira iliwapanda wanajeshi wa pande zote na kujitoma vitani. Hapa mtunzi analenga kusisitiza kuwa panga hizo zilikuwa zimenolewa zikanoleka tayari kwa mapambano.  Vile vile, katika ubeti wa 77 kuna uhaishaji ambapo panga zimepewa sifa za binadamu. Msanii ameeleza kuwa Makureshi waliandaa panga kali kabisa zipigazo zisihofu. Sifa ya hofu huwa ni ya kibinadamu bali si kwa vifaa visivyokuwa na uhai kama panga. Msanii huyu ametumia sifa hii hapa ili kuleta maana kuwa panga hizo zilikuwa zimenolewa zikanoleka kutumika vitani.

## 4.2 Mbinu rejeshi

Mbinu hii imetumika katika utenzi huu mara si moja. Katika beti za 58-68 msimulizi ametueleza kwa kirefu sababu iliyozua suitafahamu baina ya Mtume Muhammad na Makureshi. Kwenye ubeti wa 58 tunapata kuelewa kuwa Makureshi walikuwa wameanza kumchokoza Mtume Muhammad kwa lengo la kumpiga vita na kumwua. Uchokozi huu ndio uliomfanya Mtume Muhammad

kuhama Maka hadi Madina ilivyo kwenye ubeti wa 59. Baada ya kuhamia huko, Makureshi waliobakia Maka wakaanza mipango ya kumwangamiza Mtume Muhammad popote apatikanapo. Kwenye ubeti wa 61 ahadi ikatangazwa kwa yeyote ambaye angeweza kumwua Mtume Muhammad. Baada ya Matamanio ya Makureshi yaliyolenga kumwua Mtume Muhammad kuambulia patupu, walizidi kumkejeli tu kila uchao. Kejeli hizo na stihizai alizoelekezewa Mtume Muhammad zikaishia kutokea kwa pigano la Badri ambapo Makureshi walishindwa kabisa.

Katika ubeti wa 220 msimulizi wa utenzi huu ameturejesha katika historia na tamaduni za Makureshi kwamba ubebaji wa bendera wakati wa vita ni lazima. Anatuelezea kwamba anayeteuliwa kuibeba ni sharti aipeperushe juu kwani ikianguka chini pambano husimama. Hivyo, iwapo abebaye kauawa, ni sharti msaidizi wake aibebe mara moja ili kuhakikisha pambano halisimami. Iwapo haitabebwa bila shaka ina maana kwamba pambano limekwisha inavyodhihirika katika ubeti wa 223. Hivyo, kulingana na desturi yao, uzao wa Banu Abdi- Dari ndio uliotunukiwa jukumu la kubeba bendera ya kivita.

Mbinu rejeshi pia imejitokeza pale ambapo msimulizi ametumia majemedari wa akina Ubayyi bin Khalafu kutujulisha kuwa hapo awali, Ubayyi bin Khalafu alikuwa shujaa kweli kweli ambaye alistahamili majeraha makubwa vitani kuliko alilokuwa akisema alipata kutoka kwa Mtume Muhammad. Kulingana na wenzake, hakuna siku ambayo alitoroka vitani eti kwa sababu ya jeraha kinyume na wakati huo ambapo alimgeuza farasi wake kurejea nyumbani kwa kilio inavyoelezwa katika ubeti wa 461.

Msimulizi ametumia mbinu rejeshi anaposimulia ugomvi baina ya Mtume Muhammad na shujaa wa Makureshi Ubayyi bin Khalafu ulipoanzia. Katika beti za 491-501 msimulizi ameeleza kuwa Mtume Muhammad akiwa Maka njiani wakapatana na Ubayyi bin Khalafu akimlisha farasi wake. Kichokozi, Ubayyi akamwambia Mtume Muhammad kwamba wasikutane pabaya nje ya Maka kwani angemwangamiza akiwa juu ya farasi wake huyo aliyekuwa akimlisha. Hapo hapo Mtume Muhammad akamwomba Mungu kumpa kibali cha kumwangamiza adui huyo mchokozi na ombi lake likakubaliwa na Mungu. Baada ya ombi hilo kukubaliwa, Mtume Muhammad akampa ahadi kwamba kwa jina lake Mungu angemwua akiwa juu ya farasi wake yuyo huyo. Mwishowe Mtume Muhammad alitimiza ahadi hiyo kwa kumwua kwa kijambia kilichomwingia shingoni na kumpa jeraha la mauti baada ya siku chache.

## 4.3 Taswira

Taswira ni picha ambazo msanii hukusudia kuzijenga katika fikra za wasomaji wa kazi yake. Picha hizi aghalabu hudokeza hali ya uhalisia fulani wa kinachozungumziwa. Kulingana na Murungi (2013) taswira ni sawa na jazanda ambapo lugha hutumiwa kuchora picha fulani katika mawazo ya msomaji kwa kutumia ufafanuzi wa maneno mbalimbali. Taswira hizi kulingana na Mbatiah (2001) humfanya msomaji kuona, kuhisi na kunusa kile kinachofafanuliwa katika maelezo. Itambulike kuwa, taswira kama mbinu ya kisanii hulenga kumsaidia msanii kuwasilisha dhamira na maudhui yake kwa namna anavyopenda.

Taswira huibuliwa na msanii kwa kuhakikisha ameteua msamiati unaofaa zaidi, kisha kuyapanga maneno yake kwa njia yenye mvuto ili kuzua athari fulani katika mawazo ya msomaji. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* taswira mbalimbali zimejitokeza kwa jinsi ambavyo tumeelezea katika sura hii. Kuanzia ubeti wa 1-16, msanii huyu ametupa taswira ya Mungu Muumba kama aliye na uwezo zaidi ya binadamu yeyote. Amemchora kama ambaye hana wa kufanana naye kwa lolote. Yeye alikuwa, yuko na atakuwepo milele. Anajitosheleza kwa mambo yote. Yeye ni mwenye nguvu za ajabu.

Taswira nyingine inatuangazia kuhusu Mtume Muhammad ambaye ameelezewa kama kiumbe cha Mungu mashuhuri. Kulingana na mtunzi wa utenzi huu katika beti za 21 na 22 Mtume Muhammad ndiye kiumbe bora zaidi kwa vyote alivyoumba Muumba mbingu na dunia. Picha hii inadhihirishia binadamu kuwa nafasi ya Mtume Muhammad ni ya kipekee mbele za Muumba wa dunia na hivyo basi kila mwanadamu yuapaswa kutii mafunzo na mwongozo wa Mtume Muhammad haswa waumini wa Kiislamu.

Msimulizi wa utenzi huu ametupa picha ya vita kikamilifu haswa mpokezano wa bendera katika jeshi la Mkureshi kuanzia Mansabu wa Omari hadi mbebaji wa mwisho kuangamia tunavyoelezwa katika beti za 241-255 ambapo waliotunukiwa wajibu waliisha halafu katika beti za 256-259 tumepewa picha kwamba wakuu wa jeshi la Makureshi walishika usukani baada ya kuona aibu kwa kukosa mtu ambaye angebeba bendera yao. Vita vilichacha na kuwalemea Makureshi hadi pakakosa yeyote ambaye angebeba bendera iliyokuwa chini. Mwanamke mmoja alibeba bendera baada ya muda mfupi naye akaangamizwa. Katika beti za 275-279 msanii ametueleza kuwa wakati jeshi la Mtume Muhammad lilifanikiwa kufukuzia mbali jeshi la Makureshi, baadaye walianza kuokota rasilimali za Makureshi walizowacha nyuma baada ya kukimbilia usalama wao.

Wanajeshi wa milimani kwa tamaa zao, pia walikimbilia kuokota mali hizo za Makureshi na kuasi wajibu muhimu waliopewa. Makureshi walipogundua kuwa njia za milimani ziliwachwa wazi, wakarejea kwa kishindo na kuwashambulia Waislamu vibaya sana. Vita vilichacha ilivyo wazi katika beti za 317- 334 na 338 ambapo tumeelezwa kuwa baina ya makundi haya mawili hasimu, hakukuwa na aliyembembeleza mwenzake kwani kila mmoja alijawa na hamaki. Waislamu waliuawa na kujeruhiwa na jeshi la Makuresi kwa sababu walikuwa wengi inavyoelezwa katika ubeti wa 329.

Taswira nyingine inatokana na maelezo ya msanii kuhusu jinsi shujaa wa Makureshi aitwaye Ubayyi bin Khalafu alivyovaa kijeshi. Mavazi yake ya kivita kulingana na msimulizi wa utenzi huu yalifunika kila sehemu ya mwili wake na yalikuwa yametengenezwa kwa chuma. Hata hivyo, mavazi hayo hayakumkinga na jeraha la Rasuli kwani alimwua kwa njia rahisi mno. Mtume Muhammad alimtupia kijambia kilichomwingia katika shingo yake na kumwua. Mavazi ya vyuma na ya kivita aliyojifunikia mwili wake wote hayakuwa ya msaada kwake kabisa. Tendo hili la kishujaa ni dhihirisho tosha kuwa Mungu Muumba amempa Mtume Muhammad mamlaka na nguvu ya kutenda miujiza ya ajabu. Kitendo hiki vile vile kina maana kuwa, Mungu Muumba hamna ambalo linamshinda hata pale ambapo tunaona ugumu, yeye anaweza inavyoelezwa katika beti za 420-422. Katika beti za 449-457 msimulizi ametupa picha madhubuti ya jinsi Ubayyi bin Khalafu alihisi baada ya kusukumiwa kijambia na Mtume Muhammad, alihisi uchungu usio mfano. Akawa akilia kwa sauti kuwa Mtume Muhammad kamwua.

Tunapata picha ya namna ambavyo Makureshi walimshambulia Mtume Muhammad kwa mawe walipopata kuwa hawakuwa na uwezo wa kumfikia karibu ili wamwue kwa upanga. Hii ni kwa sababu Mtume Muhammad alizingirwa na Masahaba wake pande zote ilivyowazi katika beti za 583-601. Walimmiminia mawe bila kuyapunguza, mara wakamvunja meno na kumpasua utosi. Walizidi kumwangushia mawe kama mvua kwa lengo la kumwangamiza kabisa. Namna ambavyo kofia ya chuma ilivyovunjika na vyuma kujitoma mwilini mwake ni taswira inayolenga kuashiria hasira na kisasi cha Makureshi kwa Mtume Muhammad, pili inaashiria namna vita vilivyochacha bila kundi lolote kurudi nyuma. Vile vile, kuna taswira ya namna Mtume Muhammad alivyoumizwa baada ya kuangushiwa mawe mengi yaliyompa majeraha mengi asiwe na uwezo hata wa kujinyanyua peke yake. Ilimlazimu sahaba wake kumnyanyua na kumweka ndani ya pango ili apate kupumzika inavyoelezewa katika beti za 614-618.

Taswira nyingine ni ile inayoonyesha namna mashahidi wa Kiislamu walivyouawa anavyoeleza msanii katika beti za 700-702 anasimulia namna walivyokatwakatwa na vipande vya miili yao kutapakaa kila mahali. Bwana Hamza ambaye alikuwa ami ya Mtume Muhammad alikatwakatwa vibaya sana hadi msimulizi anashindwa kufafanua. Picha hii ni dhihirisho tosha la ukatili na uroho wa Makureshi dhidi ya Waislamu. Kuna taswira ya jinsi vita vya Uhud vilivyoathiri ami ya Mtume Muhammad hadi kumfanya Rasuli kuwa na hasira hadi kukiri kulipiza kisasi. Jinsi mwili wake ulivyoharibiwa wakati wa kifo chake ni picha iliyomkasirisha Rasuli. Picha hii inadhihirisha unyama wa Makureshi dhidi ya Waislamu. Vile vile, inadhihirisha shauku ya Makureshi ya kulipiza kisasi dhidi ya Waislamu baada ya kupigwa vibaya na Waislamu katika pigano la Badri. Katika beti (19, 20 na 25) msimulizi ametujengea picha ya thamani kubwa ya Mtume Muhammad mbele za Mungu Muumba.

Baina ya beti 58-67 tunapata picha ya ukatili wa Makureshi dhidi ya Waislamu. Katika ubeti wa 58, tumegundua kuwa Makureshi ndio walianza kumchokoza Mtume kwa lengo la kumwangamiza. Fitina na uchokozi wao huo ukamfanya Mtume Muhammad kuhamia Madina. Ubeti wa 60 tumegundua kuwa Makureshi waliamua kufanya kila juhudi kumwangamiza Mtume Muhammad bila kusaza hata kutumia rasilimali zao. Waliweka ahadi kwa yeyote ambaye angefanikiwa kumwua Mtume Muhammad inavyosimuliwa katika beti za 62-64.

Vile vile, baina ya beti 66-68 tunagundua kuwa baada ya juhudi za Makureshi kumwua Mtume Muhammad kufeli walizidi dhihaka na kejeli kwake hadi pakatokea pigano la Badri ambapo Makureshi walishindwa. Katika beti za 75-82 tunapata taswira ya jinsi Makureshi walianza kujiandaa kushiriki kwenye vita baada ya kupata kichapo katika pigano la Badri. Kwenye ubeti wa 75 tunaelezwa kuwa Makureshi waliazimia kutekeleza uharibifu mkubwa dhidi ya Waislamu ili waweze kujiondolea aibu ya kushindwa katika pigano la Badri. Kwa sababu hiyo, waliunda panga za kivita inavyoelezwa katika ubeti wa 77, wakatafuta farasi ubeti wa 78, wakatafuta ngao ubeti wa 82. Kwa kifupi, walichanga silaha za kivita ili kuwafanikisha katika vita vya Uhud kwa lengo la kukuza jina lao lililodunishwa baada ya kushindwa katika pigano la Badri.

### 4.4 Hitimisho

Katika sura hii tumeelezea kipengele cha tamathali za usemi, mbinu rejeshi na taswira kama vipengele vya kimtindo vinavyotumika katika ufinyanzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Tumeeleza tamathali za usemi kama vile: maswali ya balagha, kinaya, chuku, takriri, tashhisi na tashbihi.

Tumetoa ithibati mbalimbali kutokana na utenzi wetu pamoja na dhima ya vipengele hivi katika utenzi huu. Vipengele hivi vimemfaa msanii mno kuwasilisha dhamira na maudhui yake katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Katika sura inayofuata tumeshughulikia kipengele cha mandhari pamoja na usimulizi. Tumefafanua jinsi vipengele hivi vimetumika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* kufanikisha malengo ya msanii.

## SURA YA TANO

## MANDHARI NA USIMULIZI

### 5.0 Utangulizi

Mandhari ni kipengele muhimu katika fasihi. Kulingana na Wamitila (2002), mandhari hudhihirisha wazi ni wapi matukio fulani yalifanyika na ni wakati gani haswa. Mandhari vile vile yanaweza kuathiri tabia na mienendo ya mhusika katika fasihi. Katika utafiti wetu tumeangazia aina mbalimbali za mandhari kama yanavyojitokeza katika *Utenzi wa* V*ita vya Uhud.* Kama vile: mandhari ya kivita, kidini na ya kijiografia. Vile vile, tumejadili aina mbalimbali za usimulizi zinavyojitokeza katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Usimulizi uliojitokeza pakubwa katika utenzi huu ni usimulizi wa nafsi ya kwanza, nafsi ya tatu na usimulizi penyezi ambao ni wa hapa na pale.

### 5.0 Mandhari

Kulingana na Wamitila (2008) mandhari ni wakati na mazingira ambayo huwa ni chanzo cha kazi ya kifasihi. Ni wazi kwamba msanii anapoanza kuandika kazi yake, huwa anajipata katika mandhari maalum ambayo kwa njia moja au nyingine ni sharti yaathiri kazi yake kwa njia chanya au hasi. Vile vile, mandhari hayo humpa sura ya jamii na maisha yao ambapo kazi hiyo hufinyangwa.

Ntarangwi (2004) anaelezea mandhari kama jinsi mahali fulani panavyoonekana kiuhalisia. Katika hali ya kuelezea mandhari, msanii huonyesha mazingira halisi, vifaa na vitu halisi vinavyopatikana mahali panaporejelewa kama vile: milima, maziwa, mito, soko, majumba, mabomba ya maji, maduka, shule, misikiti, makanisa, vijiji na kadhalika.

Kwa kutathimini maoni ya wataalamu hao, tunakubaliana kuwa mandhari ni mahali ambapo msanii huibunia kazi yake. Msomaji wa fasihi anapaswa kuelewa mandhari kazi husika ilifinyangwa ili kumsaidia kuelewa hisia, mienendo, imani na mwelekeo wa mtunzi wa kazi hiyo. Kwa kifupi, ili msomaji wa kazi ya kifasihi aweze kuihakiki kazi ya kifasihi kikamilifu, ni sharti atambue mandhari yanavyojitokeza katika kazi yenyewe.

Katika *Utenzi wa* V*ita vya Uhud* mandhari mbalimbali yamedhihirika waziwazi. Kwa mfano: kuna mandhari ya kidini, kivita na ya kijiografia. Mandhari ya kidini na kivita ndiyo yametamalaki utenzi wote tangu mwanzo hadi mwisho kwa sababu utenzi wote unahusu vita. Kuna mandhari ya

kijiografia ambayo yanatueleza haswa mazingira ya kulikopiganwa vita vya Uhud ambapo ni katika bonde la mlima Uhud. Msimulizi wa utenzi wetu kwa kifupi, anatuelezea safari ya wapiganaji wa pande zote mbili iliyokuwa na changamoto kwa sababu ilikuwa jangwani ambako aghalabu huwa na shida nyingi ikiwemo ukosefu wa maji, jua kali, ukosefu wa vyakula, ukosefu wa barabara nzuri, vumbi tele na kadhalika.

### 5.1.1 Mandhari ya kidini

Matumizi ya majina kama vile Mungu, Mtume Muhammad katika utangulizi wa utenzi huu ni dhihirisho kuwa utenzi huu ulitungwa katika mandhari ya dini. Sababu kuu ni kwamba, wahusika hawa ndio wanaopewa sifa zaidi katika imani ya Kiislamu inavyodhihirika katika beti za 1-26. Katika beti hizo, mtunzi anaanza utenzi wake kwa kumhimidi Mungu. Mtunzi anammiminia sifa Mungu Muumba hadi ubeti wa 16. Baadaye, katika beti za 17- 25 msanii amemrejelea Mtume Muhammad kwa kumtunuku sifa sufufu pia. Maelezo hayo bila wasiwasi kama wasomaji tunaelewa kuwa utenzi wenyewe umetungwa kwa misingi ya dini ya Kiislamu. Katika beti za 173-175 tunaelezwa kuwa Mtume Muhammad na jeshi lake walikusanyika kwa maombi kwa Mungu kabla ya kuingia vitani alfajiri siku ile ya vita. Kitendo hiki hutuelekeza kusema kuwa utenzi huu umefumbatwa katika mandhari ya kidini hususan dini ya kiislamu.

Kuna dhihirisho la mandhari ya kidini pale ambapo tunagundua kuwa Mansabu wa Omari shujaa wa Makureshi alikuwa wa kwanza kwenda Madina kusomea somo la dini linalohusu ibada za aina mbalimbali inavyojitokeza katika ubeti wa 234. Vile vile, katika beti za 553-564 mandhari ya kidini yanajitokeza pale ambapo Mtume Muhammad anaangushiwa mawe na maadui zake Makureshi, hakuridhia maombi ya masahaba wake ya kuwaapiza. Badala yake aliwaelezea kuwa hakutumwa ulimwenguni kuharibu bali kujenga na kuhifadhi. Halafu baadaye katika ubeti wa 556 Mtume Muhammad anafanya maombi ya kuwatakia fanaka katika uzao wao. Aliwaombea ulinzi kwa Mwenyezi wasije wakatenda uhasama dhidi ya wenzao. Maombi hayo ni dhihirisho la mandhari ya kidini katika utenzi huu kwa sababu Mtume Muhammad anashikilia imani ya kidini inayosisitiza msamaha pamoja na upendo kwa adui. Lengo kuu la dini katika utenzi huu ni kuhubiri msamaha na maadili katika maisha ya binadamu. Vile vile, kulingana na imani za kidini, maombi huelekezwa kwa aliye juu zaidi ya binadamu naye ni Mungu Muumba. Katika utenzi huu Mtume Muhammad ametekeleza hayo kwani amemwomba Mungu asamehe na kuwabariki mahasidi wake

waliomhangaisha sana. Kulingana na imani za kidini, maombi ya imani hujibiwa inavyojitokeza katika beti za 562-565.

Katika utenzi huu, wahusika wakuu ambao ni Mungu na Mtume wake Muhammad wanadhihirisha kwamba utenzi huu ni wa kidini. Katika utenzi huu na katika imani ya Kiislamu, Mtume Muhammad ana nafasi kubwa sana kuhakikisha waumini wa Kiislamu wamepata mfano mwema wa maadili. Pili, katika utenzi huu, tunashuhudia pande mbili pinzani ambapo Mtume Muhammad na jeshi lake wanapigana na jeshi la Makureshi ambao ni adui wa Mungu ambalo ni dhihirisho tosha kuwa utenzi huu ni wa kidini kwani upinzani wenyewe una mashiko kwamba vita vya Uhud ni baina ya upande wa shetani na wa Mungu. Kulingana na maoni hayo tunapata kuelewa kuwa wamfuatao Mtume Muhammad ni wa Mungu ilhali wampingao ni wa Ibilisi. Upinzani huo baina ya Mungu na Ibilisi hukuza mandhari ya kidini.

### 5.1.2 Mandhari ya kivita

*Utenzi wa Vita vya Uhud* ulipokuwa ukiandikwa na mtunzi, makundi lengwa yaani Waislamu na Makureshi walikuwa wametangulia kupigana vita vya Badri. Vita hivi kulingana na mtunzi wa utenzi huu vilitokana na uchokozi wa Makureshi kwa Mtume Muhammad. Ingawa hivyo, Makureshi walishindwa vibaya sana na kurejea makwao kwa aibu kubwa. Ili kuondoa aibu yao wakaazimia kupigana vita vya Uhud kama namna ya kulipiza kisasi inavyodhihirika katika ubeti wa 68. Kushindwa huku, kuliwalazimu Makureshi wafanye maandalizi kabambe ili kulipiza kisasi inavyodokezwa katika ubeti wa 98. Maandalizi yenyewe yaliwachukua takriban miezi tisa baada ya pambano la Badri.

Mandhari ya kivita yamejitokeza pale ambapo wazalendo wa Kikureshi walianza safari kwenda Madina kwa farasi pamoja na ngamia. Walikuwa wametanguliwa na kikundi cha vijana wao shupavu inavyosimuliwa katika beti za 99, 100 na 101. Lengo lao kubwa ni kwenda kutalii Madina kabla ya vita kutangazwa. Msimulizi wa utenzi huu anaelezea zaidi namna kundi hilo lilikuwa limejivika mavazi ya kivita pamoja na walivyo stadi wa vita, maelezo ambayo yanatuandalia mandhari ya kivita tukirejelea beti za 103 -105.

Kuna dhihirisho la mandhari ya kivita unapotazama jinsi jeshi la Makureshi lilivyojivika mavazi ya kivita yaliyoziba miili yao yote. Mavazi yenyewe yalikuwa yametengenezwa kwa vyuma inavyosimuliwa katika beti za 104 na 105. Vile vile, ukichunguza beti za 203-209 utapata

mandhari ya kivita pale ambapo tunapewa picha ya maandalizi ya jeshi la Waislamu. Mtume Muhammad aliteua wanajeshi hamsini na kuwapa jukumu la kuchunga njia za milimani chini ya uongozi wa Abdulla Khuberi tunavyoelezwa katika beti za 206 na 212. Pili, alimchagua Mansabu bin Omari kutoka uzao wa Banu- Dari kama mbeba bendera ya Waislamu vitani. Katika ubeti wa 216 tunaelezwa kuwa baada ya maandalizi wanajeshi wa pande zote wakajipanga tayari kuanza pambano. Maelezo hayo yote yanadhihirisha mandhari ya kivita.

Suitafahamu baina ya waumini wa Maka na Madina inadhihirisha mandhari ya kivita. Msimulizi anaeleza kuwa walikamatana na kupigana kwa panga kila mmoja asitake kupoteza katika upande wake inavyojitokeza katika beti za 235-236. Mapigano hayo yaliishia mauaji ya Mansabu wa Omari shujaa wa Waislamu. Kulingana na msimulizi, mauaji hayo yalikuwa pigo kubwa katika jeshi la Makureshi kwa vile huyo shujaa ndiye alikuwa mbeba bendera wao naye kufa wa kwanza vitani ilikuwa tatizo kubwa kwao. Uwepo wa mishale kwa waliochunga njia za milimani ni dhihirisho wazi la mandhari ya kivita katika utenzi huu.

Katika ubeti wa 317 mandhari ya kivita yamejitokeza pale ambapo kulikuwa na uvamizi wa Makureshi baada ya walinda njia za milimani wa jeshi la Waislamu kuondoka. Waislamu wakapata kipigo kikubwa. Vile vile, katika ubeti wa 339 shujaa wa Mtume Muhammad waliyeshahabiana mno akauawa na maadui kudhani walikuwa wamemwangamiza Rasuli kumbe ilikuwa ni sahaba wake Mansabu wa Omari.

Mandhari ya kivita pia yamejitokeza katika beti za 236-257 ambapo shujaa wa Makureshi aliyepewa jukumu la kubeba bendera aliangamizwa vitani. Kwenye ubeti wa 380 tunapata tukio la kujeruhiwa kwa Mtume Muhammad ambalo linadhihirisha mandhari ya kivita. Mtume Muhammad alimiminiwa mawe kadhaa yaliyompa majeraha kadhaa usoni pake na kwenye kidevu chake. Ni wazi kwamba vita vilikuwa vimechacha sana baina ya pande hizi mbili pinzani. Majeraha haya yote yanadhihirisha wazi mandhari ya kivita.

Maelezo hayo yote kwa kweli yanatuandalia mandhari ya vuta nikuvute ya kivita baina ya pande mbili husika yaani Makureshi na Waislamu. Vita hivi viliishia kuwalemea Waislamu kwa makosa yao wenyewe. Kitendo cha wanajeshi wa Mtume Muhammad aliowateua kuwa walinzi wa njia za milimani kukosa kuwajibika na kutii amri ya Rasuli ya kutoondoka mahali pao kiliwatia matatani

pakubwa. Vita vyenyewe vinajulikana kama vita vitakatifu na kulingana na historia, hamna vita vyovyote vimewahi kutokea kama hivi ambapo Mtume Muhammad hakushinda.

Mandhari ya kivita vile vile yamejitokeza waziwazi pale ambapo msanii wa utenzi huu anasimulia namna ambavyo Ubayyi bin Khalafu alijivika na kubeba upanga wake, jinsi anavyotishia kumwangamiza Mtume Muhammad kwa kishindo ilivyo wazi katika beti za 419-453. Vile vile, namna maelezo kuhusu jinsi Mtume Muhammad alivyojivika na kumpiga hasidi huyo kwa kijambia shingoni ni dhihirisho la mandhari ya kivita katika utenzi huu.

Mandhari ya kivita yamedhihirika vile vile katika beti za 530-547 ambapo baada ya Makureshi kushindwa kumfikia Mtume Muhammad karibu, waliamua kumwangushia mawe kwa fujo bila kukoma. Mawe hayo yalimpa Mtume Muhammad majeraha katika utosi na mdomo wake wa chini. Jeraha lake la utosini kulingana na msimulizi, halikuwahi kupona hadi alipofariki dunia. Maelezo hayo yanatudhihirishia mandhari ya kivita katika utenzi huu.

### 5.1.3 Mandhari ya kijiografia

Msimulizi katika utenzi huu anadhihirisha wazi kuwa mandhari ya kijiografia hapa ni jangwa anaposafiri akiwa amepanda juu ya nyumbu wake. Anatuelezea kuwa anasafiri katika jangwa ambapo kuna changamoto si haba. Katika ubeti wa 62 tunapata maelezo kuwa viongozi wa Makureshi walikuwa wametoa ahadi kwa yeyote ambaye angefanikiwa kuwapelekea kichwa cha Mtume Muhammad. Ahadi yenyewe ni ngamia mia moja. Ni jambo la wazi kuwa mifugo hawa hufugwa mahali pakavu hivyo kutuandalia mandhari ya kijiografia. Bila shaka hili ni dhihirisho kuwa utenzi huu ulifinyangwa katika mandhari ya jangwani.

Katika ubeti wa 88 mtunzi ametutajia mahali halisi ambapo vita hivi visimuliwavyo kwenye utenzi huu vilifanyika. Anatueleza kuwa vilitokea mahali panapoitwa Uhud. Uhud ni mahali ambapo pamepewa jina kutokana na mlima ulioko sehemu hiyo. Vita hivi vinaitwa vya Uhud kwa sababu vilipiganwa katika mlima unaoitwa Uhud. Anafafanua zaidi umbali wake kuwa ni maili tatu kutoka Madina na uko upande wake kusini na kaskazini katika dira. Mandhari haya ni ya kijiografia kwa sababu yanaonekana. Mandhari haya yamejitokeza katika beti za 302 na 303 ambapo msimulizi wa utenzi huu ametufafanulia kuwa safari yake ni katika jangwa kubwa zaidi katika nchi hiyo. Katika ubeti wa 303 msanii anaeleza kuwa hana haja ya kukazana mwendo wake kwani ni wazi kwamba safari hiyo haiwezi kukamilika siku hiyo. Kwenye beti za 381- 384 vile

vile, msimulizi anadhihirisha mandhari haya pale ambapo anaelezea namna ambavyo Mtume Muhammad alivyoanguka ndani ya shimo wakati vita vilikuwa vimepamba moto. Juhudi zake za kujinusuru zikagonga mwamba hadi pale ambapo sahaba wake Talha aliyekuwa mwenye nguvu alijitoma shimoni na kumwokoa.

Dhihirisho jingine ni katika beti za 571-573 ambapo msimulizi wa utenzi huu anadokeza mahali ambapo vita vilitokea. Katika ubeti wa 571 baada ya masimulizi kuhusu yaliyomfika Mtume Muhammad, msimulizi anaamua kuanza kutuelezea yaliyojiri katikati ya jangwa anakosafiri. Anatuelezea kuwa atafafanua kikamilifu atakayoshuhudia bila woga wala kuficha siri yoyote. Anadai kwamba jangwani hakuna raha kwa sababu hakuna chakula wala maji. Maelezo hayo yanadhihirisha mandhari ya kijiografia katika utenzi wetu.

Kumetokea mandhari ya kijiografia pale ambapo Talha anambeba Mtume Muhammad na kumweka katika pango chini ya jabali ili apate kutuliza makali ya mapigo ya Makureshi inavyodhihirika katika ubeti wa 618. Kwenye beti za 633-646 vile vile, kuna dhihirisho la mandhari ya kijiografia ambapo tunafafanuliwa kuhusu maisha ya Mtume Muhammad na masahaba wake pangoni baada ya Mtume Muhammad kujeruhiwa kwa mawe katika pambano la Uhud, maelezo ambayo ni dhihirisho kubwa la mandhari ya kijiografia. Vile vile, ujaji wa wanawake wa Kiislamu wakiongozwa na Seyyidati Esha, Seyyidati Batuli katika mkumbo wa wanawake wengine ambapo waliingia pangoni kumjulia Mtume Muhammad hali, kwani walikuwa wamepata habari kwamba alikuwa amefariki vitani, habari ambazo zilikuwa za uwongo kwani aliyeuawa alikuwa mmoja wa masahaba wake aitwaye Mansabu. Makureshi walikuwa wamedhania alikuwa ni Mtume Muhammad kwa sababu sahaba huyo wa Mtume Muhammad alishabihiana kabisa na Mtume Muhammad. Kwa sababu ya uvumi huo, kina dada hawa wakaamua kwenda kumjulia hali Mtume Muhammad hali ya kivita ilipotulia.

### 5.2 Usimulizi

Kipengele cha usimulizi kimefanyiwa utafiti na watafiti si haba. Usimulizi ni jinsi ambavyo waandishi wa hotuba ama habari na watunzi wa kibunilizi huwasilisha mawazo yao kwa hadhira zao. Kuna masharti mbalimbali ambayo huzingatiwa wakati wa usimulizi. Kwa mfano: sharti fanani atambue hadhira yake, matukio, wakati pamoja na motisha ya usimuliaji wake.

Kulingana na Attenbernd na Lewis (1963) usimulizi ni mkabala unaomwezesha msimulizi kuafikia yanayotendeka na kusikiliza yanayowasilishwa na kazi ya kifasihi. Naye Mlacha (1991) anaona usimulizi kama uhusiano baina ya msimuliaji na anayesimuliwa hadithi. Katika *Utenzi wa* V*ita vya Uhud* aina mbalimbali za usimulizi zimetumika kwa lengo la kuufanikisha utenzi huu. Aina hizo ni pamoja na usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya tatu pamoja na usimulizi penyezi ndizo aina za usimulizi ambazo zimedhihirika zaidi katika utenzi huu.

**5.2.1 Usimulizi nafsi ya tatu**

Katika ubeti wa 1 mtunzi anaanza kwa kumrejelea Mungu kama Mkuu na aliye pekee. Picha hii ni dhihirisho tosha kuwa Mungu ni Muweza na ana nguvu zaidi ya binadamu yeyote. Katika ubeti huo huo, anachukua fursa ya kumshukuru Mungu kwa kumtunuku nafasi ya kuandika utenzi huu. Katika nafsi hiyo hiyo, ananyenyekea kwa kusema kuwa anamwamini Mungu huyo muweza peke yake kwa kumpa mwongozo katika utunzi wake. Mtunzi anaendelea katika nafsi hiyo katika beti za 3, 4-16 ambapo anamsifu Mungu na kumtunuku sifa chekwachekwa. Thibitisho li wazi katika ubeti wa 15 ambapo anamtambua Mungu kama mwenye rehema ambaye ni wa milele na ambaye yu kila mahali.

Katika beti za 17, 18-25 msanii huyu ametumia nafsi ya tatu kumrejelea Mtume Muhammad ambapo naye vile vile amemtunuku sifa nyingi. Sifa hizi zinalenga kutusisitizia kuwa Mtume Muhammad ni kiumbe maalum si kama viumbe vingine alivyoumba Mungu Muumbaji. Katika beti hizi, msanii akitumia nafsi ya tatu, amemsawiri Mtume Muhammad kama kiumbe ambaye ni bora zaidi machoni pa Muumbaji. Kwenye ubeti wa 65 msimulizi ametumia nafsi ya tatu kutueleza walivyofanya Makureshi baada ya juhudi zao za kumwua Mtume Muhammad kufeli. Msimulizi anatuelezea kwamba Makureshi walizidi kumdhihaki Mtume Muhammad.

Vile vile nafsi ya tatu imejitokeza pale ambapo msimulizi anatufafanulia kwa kirefu namna ambavyo Makureshi walianza kujiandaa kwa vita dhidi ya Mtume Muhammad na jeshi lake punde tu waliposhindwa katika vita vya Badri. Walikusanya silaha mbalimbali na kuandaa jeshi lao vikali kulipiza kisasi dhidi ya Waislamu kama inavyojitokeza katika beti za 65-82. Baada ya kuwa tayari, katika ubeti wa 98 Makureshi waliamua kutuma ujumbe kwa Mtume Muhammad kutaka tarehe ya kushiriki vita. Vile vile, msimulizi ametumia nafsi hii kusimulia kisa cha vijana wa Maka kufanya safari ya ghafla kwenda Madina.

Usimulizi wa nafsi ya tatu umedhihirika pale ambapo msimulizi anatueleza kuwa baada ya Makureshi kukamilisha maandalizi yao ya kivita dhidi ya Waislamu, walianza safari yao kwenda Madina. Njiani wasaliti wa Mtume Muhammad walijiunga nao chini ya uongozi wa maamiri wanne ambao ni: Khalid bin Walidi, Amiri bin Alyasi, Ukirimu bin Abu-Jahili na Sufiani Ibni Umayya. Nia kuu ya jeshi hili ni kumwangamiza Mtume Muhammad inavyojitokeza katika beti za 98-142.

Katika beti za 142-157 msimulizi akitumia nafsi ya tatu anatuelezea upande wa Mtume Muhammad na maandalizi yake kabla ya pambano la Uhud. Msimulizi anafafanua kuwa Mtume Muhammad hakuwa na habari kuhusu ujaji wa mahasidi hao. Katika nafsi ya tatu, msimulizi anatuelekeza jinsi Mtume na jeshi lake walivyojiandaa kushiriki vita hivyo inavyodhihirika katika beti za 146, 147. Katika nafsi hiyo hiyo, tunaelezwa kwamba Makureshi na Waislamu walifanya makubaliano ya siku na saa ya pambano lenyewe. Maelezo kuhusu usaliti wa majeshi mia tatu ya Mtume Muhammad walipokuwa katika maombi ya alfajiri vile vile yanahadithiwa kupitia nafsi ya tatu. Katika ubeti wa 117 msimulizi akiwa katika nafsi ya tatu anatuelezea kuwa maamiri wa majeshi ya Makureshi walienda kushiriki vita pamoja na wake zao kwa nia ya kuchochea ari yao katika vita dhidi ya Waislamu.

### 5.2.2 Usimulizi nafsi ya kwanza

Msimulizi anatumia nafsi ya kwanza kutueleza kuwa ameanza safari yake ya kutusimulia utenzi huu. Anatwambia kuwa imebidi kuanza kwa kumshukuru Mungu kwa ukuu wake kwani ndiye pekee wa kutoa uwezo kwa binadamu ujumbe ulioko katika ubeti wa 2. Baada ya kutuelezea sifa za Mtume Muhammad akiwa katika nafsi ya tatu, mtunzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* anarejelea usimulizi wa nafsi ya kwanza kama inavyodhihirika katika beti za 26, 27-55 ambapo anatuelezea hali yake binafsi. Anajishusha hadhi kwamba yeye hana thamani ili afae kuandika utenzi huu. Msimulizi katika nafsi ya kwanza ametuchorea picha ya maumbile yake pamoja na hali yake ya kibinadamu. Amefanya hivyo maksudi kuwaelimisha wasomaji wake kuwa hakuna binadamu kamilifu hivyo basi, ni muhimu kuishi na wenzetu na upungufu wao. Anazidi kutujuza kwamba ikiwa tutaona dosari kwa kazi yake tusichelee kuirekebisha. Maoni haya vile vile ni ya kutuelimisha na kutusisitizia kwamba tuwe tayari kukubali makosa yetu na tuwe tayari kutoa nafasi ya kurekebishwa na yeyote. Katika ubeti wa 29 msimulizi anafafanua ari yake ya kupenda kutunga utenzi huo kwa lugha ya wasomaji wake. Vile vile, katika beti za 30-34 msanii ameweka

wazi hali yake ya huzuni kwani anajiona fukara wa kila hali ijapokuwa amepata fursa ya kusimulia utenzi huu hana amani wala utulivu utakaomwezesha kufanya utunzi huu.

Kwenye beti za 49-57 mtunzi akiwa katika nafsi ya kwanza, anatuandaa kusikiliza kisa hasa kwani ametamani sana kutusimulia kisa chenyewe kuanzia jangwani hadi mwishoni mwake. Baada ya kutueleza mahali vita vilipiganwa, mtunzi anaendelea katika nafsi ya kwanza kutuelezea kuwa amemaliza kutwambia ya Maka. Anasema kuwa yu jangwani na imembidi kung'oa nanga katika safari yake juu ya nyumbu wake. Kulingana naye, mwendo wa safari yake ni mrefu hadi anahofia atahitimisha safari yake saa ngapi. Kutokana na maelezo hayo, msimulizi katika nafsi ya kwanza amedhihirisha wasiwasi wake wa kufika hatima ya safari yake katika jangwa lenye shida chungu nzima. Kulingana naye, sababu ya kuchelewa kwake ni kwa vile nyumbu wake ana mwendo usio wa kasi na hatua zake ni ndogo.

### 5.2.3 Usimulizi penyezi

Usimulizi huu umejitokeza hapa na pale katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Kwa mfano: katika ubeti wa sita, mtunzi ametupa mwongozo ambao amefuata baada ya kutusimulia kuhusu Mtume Muhammad. Anatueleza kuwa punde si punde ataanza kusimulia kisa chenyewe. Mwongozo huu si sehemu ya utenzi huu ijapokuwa unatuelekeza kuelewa mkondo wa kisa katika masimulizi ya utenzi huu. Katika ubeti wa 26 msanii anapenyeza maneno yake ambayo yametoka nje ya kisa chake anapotudokezea usimulizi wake ulikuwa haulingani na maelezo yake. Ndiyo maana katika ubeti huo anatujulisha kuwa atarejelea usimulizi wake baada ya maelezo yake penyezi.

Vile vile, katika ubeti wa 48 nafsi penyezi imejitokeza pale ambapo baada ya mtunzi wa utenzi huu kuelezea hali yake kwetu, amefika katika ubeti huu na kuamua kubadili mkondo kwa kusema kuwa ataanza masimulizi yake moja kwa moja. Kauli hizi ni penyezi katika utenzi wenyewe kwa sababu si sehemu ya kisa chenyewe katika utenzi. Katika ubeti wa 57 msanii anatuandaa kuwa amekaribia katika mkondo wa kutusimulia sehemu ya kisa ambayo ni ya mkasa. Hapa msanii analenga kuwaandaa wasomaji wake kwamba punde si punde atawahadithia madhila aliyopitia Mtume Muhammad mikononi mwa maadui wake Makureshi.

Katika beti za 27-47 msimulizi wa kisa cha utenzi huu amekuwa akisimulia hali yake binafsi nje ya kisa cha utenzi. Masimulizi yake yanapenyeza nje ya kisa chetu cha vita vya Uhud. Katika ubeti wa 48 anatuarifu kuwa amerejelea kisa chenyewe. Dhihirisho tosha kuwa alikuwa amepenyeza

usimulizi wake nje ya kisa chenyewe kwa kuleta melezo yake binafsi. Usimulizi huu pia umejitokeza katika beti za 83-94 ambapo msimulizi anapenyeza usimulizi wake nje ya kisa cha maandalizi ya Makureshi kushiriki vita vya Badri anapoanza kueleza kuwa hamna haja ya kuharakisha usimulizi wake kwani asingependa kufanya dosari, vita hivyo ni vikubwa kuliko vya Badri na vinaitwa vitakatifu inavyodhihirika katika beti za 86-87. Tukitazama beti za 88-90 tuligundua kuwa msimulizi ametumia usimulizi penyezi pale ambapo anatujulisha kuwa vita hivyo vilifanyika hadi kutuonyesha kwa kutumia ramani. Maelezo haya yote ni nje ya msuko wa utenzi wetu ndio maana tunayatambua kama penyezi.

Vile vile, usimulizi penyezi umejitokeza katika utenzi wetu pale ambapo baada ya msimulizi kufika mahali ambapo majeshi ya Waislamu yaliyokuwa yakichunga njia za milimani kuondoka, kwa tamaa ya kujiokotea mali ya Makureshi walipofanikiwa kuwafukuzia mbali, anaachia kisa hapo na kupenyeza maelezo yake kuhusu athari ya kitendo hicho katili. Amepenyeza nje anapotukanya tusing’ang’anie minong’ono ya kubashiri yaliyotokea baada ya walinzi wa milimani wa Kiisamu kuamua kuvunja sheria ya Rasuli, bali tutulie atwambie wazi yaliyowapata baadaye. Maelezo haya ni nje ya kisa cha utenzi lakini msimulizi ameyapenyeza kusisitiza kwamba Wanajeshi wa Waislamu walifanya makosa makubwa yaliyowafanya kushindwa katika vita hivyo ambavyo awali walikuwa wamevitamalaki kabisa inavyoelezwa katika beti za 300-303.

Usimulizi penyezi mwingine unajitokeza katika beti za 488- 489 ambapo baada ya msimulizi kutusimulia mkasa uliompata shujaa wa Makureshi Ubayyi bin Khalafu baada wa kupewa jeraha la kufa na Mtume Muhammad, anapenyeza na kuanza kutoa maelezo ambayo yako nje ya kisa cha utenzi ambayo yanahusu maadili na mfano mwema ambao Mtume Muhammad huwa nao. Msimulizi anaeleza kuwa Mtume Muhammad huwa hamwagi damu ya mtu kwa mikono yake ila adui yule ambaye atalazimika kumwua. Katika beti za 502- 507 msimulizi huyu baada ya kutuelezea namna ugomvi baina ya Mtume Muhammad na Ubayyi bin Khalafu ulivyoanza, anapenyeza maelezo yake kwa lengo la kutuandaa kwa mkondo mwingine wa matukio ya usimulizi wake. Katika ubeti wa 503 mtunzi wa utenzi huu anatusihi kuwa na utaratibu ili mambo yasituwie mchanganyiko usioeleweka kwani kulingana naye, mpangilio huu ndio tu utahakikisha msomaji wa masimulizi yenyewe atafarijika akiyasoma. Vile vile, katika beti za 565-570 baada ya msimulizi kutuelezea jinsi masahaba wa Mtume Muhammad walivyomwomba Mtume Muhammad kuwaapiza maadui zake na Mtume Muhammad kukataa na badala yake kuwaombea

baraka, msimulizi anapenyeza usimulizi wake tena na kutuelezea kisa kwamba, maombi aliyoyafanya Mtume Muhammad kwa maadui zake yalijibiwa kwani wahusika walipata baraka tele wao pamoja na vizazi vyao wakafanya makuu kukuza dini ya Kiislamu.

### 5.3 Hitimisho

Katika sura hii tumeelezea dhana mandhari na aina mbalimbali za mandhari katika *Utenzi wa* V*ita vya Uhud.* Tumebaini kuwa katika utenzi huu mandhari ambayo yamefanikisha utenzi wenyewe ni pamoja na yale ya kivita, kidini na kijiografia. Vile vile, tumeelezea aina mbalimbali za usimulizi ambazo zimetumika katika utenzi huu ambazo ni pamoja na usimulizi wa nafsi ya kwanza, nafsi ya tatu na usimulizi penyezi.

Msanii huyu amefinyanga kazi yake kwa ustadi mkubwa. Amefaulu kuchanganya nafsi mbalimbali na mandhari zaidi ya moja ili kuafikia dhamira na maudhui yake katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Tumegundua kuwa ni vigumu kuwasilisha kazi nzuri pasi na kutumia mseto wa aina mbalimbali za usimulizi na mandhari. Katika sura inayofuata tumeshughulikia hitimisho la utafiti wetu ambapo tumetoa mukhutasari wa yote tuliyoyashughulikia katika utafiti wetu kisha tumetoa mapendekezo kwa watafiti watakaofuata.

## SURA YA SITA

## HITIMISHO

### 6.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia yote yaliyoangaziwa katika utafiti wetu pamoja na matokeo yake ili kudhihirisha kuwa tulizingatia malengo yetu ya utafiti. Vile vile, tumeangazia mafanikio ya utafiti wetu. Tumerejelea changamoto tulizokumbana nazo katika utafiti wetu pamoja na kutoa suluhisho. Mwisho kabisa tumetoa mapendekezo ya utafiti wa ziada kwa watafiti watakaofuata.

### 6.1 Mukhutasari wa yaliyoshughulikiwa katika utafiti wetu

Lengo kuu la utafiti wetu lilikuwa kuchunguza jinsi mtunzi ametumia vipengele vya kimtindo kusuka *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Katika sehemu ya utangulizi wa sura ya kwanza tumeelezea kwa kifupi historia ya *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Pia, tumeangazia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada yetu ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti wetu, msingi wa nadharia ya utafiti wetu ambayo ni nadharia ya umtindo. Tumeshughulikia yale yaliyoandikwa kuhusu mada hii. Tulisoma vitabu, tukapitia majarida, tasnifu za awali, makala mbalimbali katika tovuti na machapisho mbalimbali kwa lengo la kupata data tulizonuia. Tuliangazia mbinu za utafiti wetu na kuelezea jinsi tulizichambua data hizo kisha kuziwasilisha kwa hadhira. Mwisho tumefanya hitimisho la sura yetu.

Katika sura ya pili tumeshughulikia dhana mbalimbali ambazo zimekuwa za manufaa katika utafiti wetu. Dhana tulizofafanua katika sura hii ni kama vile: ushairi, utenzi, mtindo, muundo, mukhutasari wa *Utenzi wa Vita vya Uhud,* tamathali za usemi, taswira, wahusika, mandhari na aina mbalimbali za usimulizi. Katika sura ya tatu vile vile tumeangazia kipengele cha wahusika na uhusika wao pamoja na kipengele cha muundo. Katika sura hii, wahusika mbalimbali wameangaziwa kwa kueleza sifa zao. Vile vile, muundo uliotumiwa kufumbata utenzi wenyewe tumeushughulikia kwa kuangazia vipengele vyake kwa kirefu. Tamathali za usemi, mbinu rejeshi na taswira mbalimbali tumezishughulikia katika sura ya nne. Katika tamathali za usemi tumeshughulikia mbinu kama vile: takriri, tashbihi, chuku, kinaya, maswali ya balagha na istiara. Sura ya tano tumefafanua mandhari mbalimbali ambayo yametumika katika ufinyanzi wa utenzi huu kama vile: mandhari ya kidini, kivita na kijiografia. Vile vile, katika sura hii tumeangazia

namna usimulizi umetumika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Ni muhimu kutaja kuwa kila kipengele cha kimtindo ambacho tumekishughulikia tumeelezea umuhimu na matumizi yake katika ufinyanzi wa utenzi wetu. Kwa jumla, vipengele hivi vyote vimetumika kumsaidia mtunzi kukuza dhamira na maudhui yake katika utenzi huu.

## 6.2 Matokeo ya utafiti wetu.

Katika utafiti wetu tumeweza kujibu maswali yetu ya utafiti kikamilifu. Katika swali la kwanza tuligundua kwamba *Utenzi wa Vita vya Uhud* una vipengele vya kimtindo kama vile: wahusika, muundo, tamathali za usemi, taswira, mandhari, mbinu rejeshi na usimulizi. Vipengele hivi vimetumika kwa pamoja ili kumwezesha msanii wa utenzi huu kuwasilisha dhamira na maudhui yake. Tuligundua kuwa vijenzi hivi vinategemeana na kukamilishana, hili lina maana kuwa hakuna kipengele hata kimoja ambacho hakitahitaji chenzake. Vile vile, tuligundua kuwa kila kipengele cha mtindo ambacho tumeshughulikia kina nafasi yake katika utenzi huu. Katika utafiti wetu tuligundua kwamba msanii wa utenzi wetu ametumia muundo kikamilifu katika ufinyanzi wa kazi yake. Muundo unashughulikia namna maneno yamepangwa pamoja na mawazo yanavyotiririka katika utenzi wetu.

## 6.3 Changamoto zilizotukumba kipindi cha utafiti wetu na suluhisho.

Changamoto ya kifedha ndiyo ilikuwa kubwa wakati wa utafiti wetu. Kwa sababu tulihitaji kusafiri kila wakati kwenda maktabani hasa maktaba ambazo makala hitajika yangepatikana. Pesa za usafiri pamoja na masurufu zilifanya gharama ya utafiti wetu kuwa juu. Pili, hela za machapisho pamoja na za kupiga chapa kazi hii mara kwa mara ilikuwa ni changamoto pia. Hili lililazimu kutekelezwa kwa lengo la kuboresha utafiti wetu. Changamoto hii tulipata suluhu kwa kufanya bajeti ya mapema na kutenga fedha hizo kulingana na ratiba yetu ya matukio.

Changamoto ya kupata muda wa kutosha kwani nilifanya utafiti huu sambamba na kazi yangu ya ualimu. Wakati mwingine majukumu ya kazi yangu yalinilemea ijapokuwa nilijikaza kisabuni na kuhakikisha yaliyonihusu niliyatekeleza kwa wakati. Vile vile, niliamua kujikakamua na kuzamia kazi yangu ya utafiti aghalabu siku za wikendi, nyakati za usiku na majira ya alfajiri.

Tulikumbana na changamoto ya kupata makala za kudurusu. Ilikuwa vigumu wakati mwingine kupata nakala zenyewe kwa sababu ilikuwa ni lazima kuzitafuta katika maktaba mbalimbali suala ambalo lilituwia changamoto kubwa ikizingatiwa kuwa mpangilio wa makala au vitabu katika

maktaba zetu wakati mwingine hauendani na data zilizokuwa katika katalogi zao. Shida hii ilisuluhika kwani tuliamua kutoa makala mbalimbali kutoka mtandaoni na kuhifadhi kazi hizo katika tarakilishi kwa marejeleo rahisi tulipokuwa nje ya maktaba. Pili, tulipata makala na vitabu mbalimbali katika mtandao vilivyorahisisha utafiti wetu.

### 6.4 Mapendekezo kwa tafiti za baadaye.

Tumehakiki *Utenzi wa Vita vya Uhud* kimtindo ambapo tumeangazia baadhi ya vipengele kama vile: wahusika, tamathali za usemi, mbinu rejeshi, usimulizi, taswira, muundo na mandhari tukijikita katika nadharia ya umtindo. Hata hivyo umtindo ni sehemu ndogo tuliyoihakiki katika utenzi huu kwa vile utenzi huu unaweza kuhakikiwa kwa kuangazia vipengele vingine vilivyobakia kama vile dini na historia. Katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya mtindo kuhakiki utenzi huu. Tunapendekeza kuwa watafiti wa baadaye watumie nadharia ya umuundo, uhalisia au nadharia nyingine tofauti kuhakiki utenzi huu.

## MAREJELEO


Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki.* Nairobi. Oxford University Press.

Abdalla, S. A. (2016). "Changamoto za kutumia Istilahi Mbili kwa Dhana Moja katika Kufundisha Isimu na Fasihi katika Shule za Sekondari:" Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Abedi, K. A (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Ali, A. M. (2013). "Kuchunguza Vipengele vya Fani katika Mashairi ya Kiswahili: Ulinganishi na Ulinganuzi wa Mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji." Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Aloo, R. O. (2018). "Matumizi ya Tamathali za Usemi Teule katika Utenzi wa Qiyama." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Hijachapishwa)

Atternbernd, L. na Lewis, L. L. (wah.) (1963). *Introduction to Literature: Stories*. New York. Macmillan Company.

Boakes R. A. na Halliday, M. S. (1972). *Inhibition and Learning.* London. Academic Press.

Bradford, R. (1997). *The New Critical Idiom: Stylistics.* London and New York. Routledge.

Chaniro, C. U. (2017). "Matumizi ya Lugha katika Maulidi ya Jambeni:" Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Hijachapishwa)

Chum, H. (mha.) (1970). *Utenzi wa Vita vya Uhud:* Dar es Salaam. East African Literature Bureau.

Crystal, D. (1971). "Intonation and Metrical Theory 1. Translations of the Philological society," 70(1), 1-33

Faki, A. M. (2015). "Kuchunguza Sifa za Kifani za Utendi wa Kiswahili: Utendi wa Fumo Liyongo." Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).

Gichamba, J. M. (2005). "Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao kwa Jamii zao:

Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Halliday, M. A. K. (1971). " Language in a Social Perspective: *The context of Languages."* Vol. 23(3), pp 165-188.

Hamad, A. M. (2017). "Muundo wa Lugha katika Mashairi ya- Watungaji Wateule wa Zanzibar." Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. (Haijachapishwa).

Ilomo, L. F. (2017). "Mbinu za Ujenzi wa Wahusika na Usawiri wa Sifa zao: Uhakiki wa Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo ya E. Kezilahabi." *Jarida la Mulika,* 34(1).

Kanema, S. A. (2015). "Mchango wa Andanenga katika Ushairi wa Kiswahili." Tasnifu ya Uzamifu. Chuo kikuu cha Dodoma.

Karanja, M. W. (2014). "Matumizi ya Istiari, Tashbihi- na Taashira katika Diwani ya Sauti ya Dhiki." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Katamba, F. (1978). "How Agglutinating is Bantu Morphology? *Linguistics,"* 16(210), 77-84.

Katikiro, E. G. (2018). "Tathmini ya maana katika maneno ambatani ya Kiswahili." *Jarida la Mulika,* 36(1).

Kazungu, K. (1982). "Deviation and Foregrounding in Chosen Swahili Texts." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kemunto, J. (2015). "Uhakiki Linganishi wa Sifa za Mashujaa. Sakawa na Fumo Liyongo."Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kezilahabi, E. (1972). "The Development of Swahili Poetry: 18th- 20th Century." Kiswahili, 42(2-1), 62-67.

King'ei, K. na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Limited.

Kiptum, J. T. (2017). "Uyakinifu wa Maudhui Makuu katika Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kithuku, Z. M. (2017). "Maudhui na Mtindo katika Utenzi wa Vita vya Uhudi." Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kuvuna, S. M na wengine. (1992). *Nuru ya Ushairi: Mwongozo na Uchambuzi*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Leech G. (1979). *Semantics: The Study of Meaning.* New York. Penguin Books.

Leech, G and Short M. (2007). *Style of Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose.* New York. Pearson Longman 2nd Edition.

Lyimo, E. B. (2014). "Nadharia za Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto Nchini Tanzania." *Jarida la Mulika*. Juzuu la (33) 33-45. University of Dar es Salaam.

Lyons, J. na John, L. (1995). *Linguistics Semantics: An Introduction*. Cambridge University Press.

Makiri, K. A. (2018). "Uhakiki wa Wakati na Uwasilishaji Usemi kama Vipengele vya Usimulizi katika Utenzi wa Nabii Isa." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Massamba, D. P. (1983). "Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili. Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili." Juzuu la (3), 55-94.

Massoud, S.M.A. (2013). “Maudhui na Fani katika Tamthilia za Kiswahili:

Utafiti Linganishi wa Tamthilia za Mashetani na Kivuli Kinaishi.”

Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).

Mazrui, A.M., na wengine (2016). "An Analysis of Swahili Exegesis of Surat al Shams in Sheikh Abdulla Saleh al Farsy’s Qurani Takatifu. In cultural politics of translation: East Africa in a Global Context:" Juzuu (2)1–14. Tsehai Dar es Salaam.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi. Standard Textbooks Graphics and publishing.

Mbayi, L. K. (2009). "Uhakiki wa Fani katika Tenzi za Howani na

Mwana Kukuwa za Zaynab Himid Mohammed.

"Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mlacha, S. A. K (1991). "Point of view as Stylistics Device in Kiswahili Novels."

Kiswahili: Juzuu la (58). TUKI, Dar es Salaam.

Mnyampala, M. E. (1965). "Utenzi wa Zaburi". Ndanda Mission Press.

Mohammed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili:*

*Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohochi, E. S. (2000). "Usimulizi wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini."

*Nordic Journal of African Studies* 9(2): 49-59. University of Egerton, Kenya.

Momanyi, J. (1991). "Matumizi ya Taswira kama Kielelezo cha Uhalisi katika Utenzi wa Al-Inkishafi." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Murungi, G. K. (2013). "Mtindo Unavyoendeleza Maudhui katika Natala." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Muthoni, M. (2014). "Uhakiki wa Maudhui na Mtindo katika Tikitimaji.

Tasnifu ya Uzamili." Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani yetu*. Tanzania Publishing house.

Ndumbu, J. M. (2013). *Matumizi ya takriri na sitiari katika Utenzi wa Rasi'l ghuli*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Ngugi, E. (2018). "Maudhui na Mtindo katika Ushairi wa Watoto: Uchanganuzi wa Utenzi wa Haki za Watoto na Mashairi Bulbul." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Njogu, K. na Chimerah, R. (1998). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

Njuguna, S. M. (2016). Maudhui Yanayoimarishwa na Fani katika Riwaya ya Nguvu ya Sala. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Nyamari, R. K. (2016). ″Mtindo katika Utenzi wa Katirifu. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College, Rock Island, IL612 Publishers Ltd.

Omari, M. K. (2014). " Tamthali za Usemi katika Mashairi ya Magazetini: Uchunguzi Kifani wa Mashairi ya Ukimwi katika Magazeti ya Kiswahili." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Pribady, H. (2017). "Local Literature Revitalization in Older to Malay Language Endurance."*ADRI International Journal of Language, Literature and Culture*, 1(1).

Riffaterre, M. (2008). "The Interpretant in Literary Semiotics."

*The American Journal of Semiotics*, 3(4), 41-55.
Raffel, B. (1984). *How to Read a Poem.* New American Library.
Robert, S. (1958). *Wasifu wa Binti Saad: Mwimbaji wa Unguja.* London: Thomas.
Rono, (2013). "Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa Kidagaa Kimemwozea." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
Salem, M. (2019). Nyimbo za Taarab (huzuni) katika Zanzibar, Mwimbaji.
Senkoro, F. E. M. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam. Press and Publicity Centre.
Soud, Z. (2016). "Fani katika Maulidi ya Nuni. Tasnifu ya uzamili." Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
Starobinski, J. (1979). *Words upon Words. The Anagrams of Ferdinand de Saussure*. Yale University Press New Haven.
Topan, F. (mh.) (1973). *Aliyeonja Pepo.* Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.
TUKI, (1998). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi. Oxford University Press.
Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na vipengele vyake*. Nairobi. Phoenix Publishers.
_______________ (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Focus Publications.
_______________ (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Focus Publications Ltd.
Wanyama, T., Far, B. H. (2006). "Negotiation Coalitions in Group Choice Multi-Agent Systems. Proceedings of the Fifth International Joint Conference on Autonomous Agents and Multiagent Systems," 408- 410.
Wellek, R. (1933). *The Pearl: An Interpretation of the Middle-English Poem.* Prague: Stattni Tiskarna.

.